# Nipashe

Ijumaa Julai 5, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579962

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mbaroni tuhuma kulawiti mama mzazi, bibi kizee

UKURASA 3


Wakulima wa tumbaku wako hoi, wazidi kuwa maskini

Wasomi, Profesa Lipumba wanapotaka BoT ikopeshe zaidi

BUFE

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

Nipashe

Watanzania na mchango wa kipekee kuondoa joto duniani

Alizeti rasmi zao kila kaya, wakulima kuunganishwa na masoko

UCHUMI

Habari katika picha

UKURASA 13

# Pigo lingine kwa Mbowe



• **Mali** zake kunadiwa saa 24 zijazo kulipia deni la mamilioni... *Uk. 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**HESLB YAWAPA MBINU WASTAAFU MAKATO MAFAO**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imewataka wastaafu waliotarajiwa wanaodaiwa mikopo wailipe kwa...

**UKURASA WA 3**

**ALIYEJIFUNGUA MAPACHA WANNE AOMBA MSAADA**

MKAZI wa Mtaa wa Kameta, Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Felister Mwanyale (31), ambaye juzi alijifungua...

**UKURASA WA 4**

**MAGEREZA YATEKELEZA AGIZO LA RAIS MAGUFULI**

JESHI la Magereza limeanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli kwa kuhamisha wafungwa 1,535 kwenda kwenye magereza...




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akisalimiana na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alipomwakilisha Rais John Magufuli katika sherehe za miaka 25 ya Ukombozi wa nchi hiyo, jijini Kigali jana. Kushoto ni Rais wa Sierra Leone, Julius Maada Bio. **PICHA: OWM**

## Wema aachiwa kisha akamatwa

UKURASA 3



SAKATA LA UTEKAJI:

## Polisi sasa yaomba msaada Interpol

UK. 2


**MICHEZO** **COULIBALY ATUA KUJIFUNGA SIMBA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Pigo mali za Mbowe kunadiwa

**Na Romana Mallya**

NI pigo lingine. Ndivyo inavyoweza kuelezwa juu ya Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, kutokana na taarifa kuwa mali zake zinatarajiwa kupigwa mnada.

Mali za kigogo huyo ma Mbunge wa Hai, zimetangazwa kuuzwa kwa njia ya mnada kesho ili kulipa deni la miaka mitatu iliyopita la Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa jana na Dalali wa Mahakama, Kampuni ya Udalali ya Fosters Auctioneers and General Traders ya Dar es Salaam, Joshua Mwaituka, watauza kwa mnada vitu vyote vilivyokuwa mali za Mbowe Limited (Bilicanas).

Mnada huo unahusisha mali zilizokuwa kwenye ukumbi wa Bilicanas ambako mwaka 2016, NHC ilizichukua kwa maelezo kuwa kampuni hiyo ya Mbowe haijalipa kodi kwa miaka 20.

Tangazo la kampuni ya udalali, lilieleza kuwa mnada huo utafanyika asubuhi kwenye ghala la NHC lililoko jirani na ofisi za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) karibu na gati namba 3 la Bandari ya Dar es Salaam. Akizungumza na Nipashe, Mwaituka alisema kazi waliyopewa ni kuuza mali ambazo ni makochi, meza, kabati, friji na vitu vya alminium.

Alipoulizwa kuhusu deni ambalo inadaiwa kampuni hiyo ya Mbowe ni kiasi gani hadi sasa, Mwaituka alisema wanaohusika kujibu ni NHC wenyewe.

"Kazi yangu ni kuuza vitu vyote vilivyokuwa mali ya Mbowe Limited (Bilicanas). Kama amelipa au hajalipa waulizwe NHC. Sisi kazi yetu ni kupiga mnada ambao utafanyika Jumamosi (kesho)," alisema.

Gazeti hili lilipomtafuta Japhet Mwanasenga kutoka NHC, kwa lengo la kujua deni linalodaiwa hadi sasa ni kiasi gani, alisema anayeweza kujibu ni Meneja Mawasiliano wa NHC, Yahya Cherehani, ambaye naye alitafutwa bila mafanikio.

Mbowe ambaye pia ni Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, alipotafutwa kupitia simu yake ya mkononi, wakati wote ilikuwa imezimwa ndipo Mkuu wa Idara ya Habari wa Chadema, Tumaini Makene, aliliambia gazeti hili kuwa yuko mahakamani.

Mwaka 2016, NHC iliondoa vifaa vyote vilivyokuwa vinavyotumiwa na Kampuni ya Free Media na kufungua vifaa vyote vya muziki kwenye klabu ya Bilicanas kwa maelezo kuwa anadaiwa pango zaidi ya Sh. bilioni 1.7.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangala, akifungua mkutano wa mwaka wa wahariri na wanahabari waandamizi, ulioandaliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa), jijini Mwanza jana. **PICHA: GIFT THADEY**

# HESLB yawapa mbinu wastaafu makato mafao

**Na Romana Mallya**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), imewataka wastaafu watarajiwa wanaodaiwa mikopo wailipe kwa utaratibu wa kawaida, badala ya kusubiri hadi kustaafu, hivyo kusababisha kiinua mgongo chao kikatwe.

Mkurugenzi wa msaidizi Urejeshaji wa Mikopo kutoka HESLB, Fidelis Joseph, alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumzia ujereshaji mikopo kwa wanufaika akiwa kwenye kipindi cha East Africa Breakfast cha East Africa Radio,

Akizungumza kwenye kipindi hicho, Joseph alisema taratibu za kuwafuata wastaafu ni za kawaida na kwamba bodi haiendi kuchukua kiinua mgongo chao chote bali kumpa taarifa mhusika kuwa anadaiwa.

"Kwa hiyo atakuwa ana jukumu la kulipa deni hadi liishe. Deni litakuwa limeisha pale utakapokuwa umekufa au ukipata matatizo ya kudumu kama ugonjwa kwa hiyo kama ni mstaafu lazima ulipe deni kwa nia yeyote," alisema.

Akielezea kuhusiana na ongezeko la deni la bodi hiyo kwa wanafunzi kila mwaka kama ambavyo imekuwa ikidaiwa na wanufaika, Fidelis alisema wamewekewa sheria ambayo lengo lake ni kulinda thamani ya fedha kwa watu ambao wanachelewesha.

INAENDELEA UK.8


Hati ya kuitwa shaurini PCF6

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.

MCA/63

Katika Mahakama ya Mwanzo NYALIKUNGU

Wilaya ya MASWA

SHAURI LA MADAI/JINAI NO 29 LA 2018

MDAI: ..........................................................VISSION FUND

DHIDI YA

MDAIWA: ...........................................ANTHONY FELIX MIHAYO

KWA ANTHONY FELIX MIHAYO- MWABAYANDA
K.K MWENYEKITI WA KITONGOJI CHA MWABAYANDA.
SOLA

KWA KUWA imelazimika uhudhurie ili ujibu dai la pesa sh. 6,125,000/= Marejesho ya mkopo na riba.
UNAAMRISHWA NA JAMHURI uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya JUMATATU Tarehe 15/07/2019 saa 2:30 asubuhi mara baada ya hapo shauri liweze kusikilizwa.

Usikose kuhudhuria.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 27/06/2019.

Hakimu Mahakama ya Mwanzo

Mwombaji Hati hii: MDAI VISSION FUND

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA MASWA NYALIKUNGU

215310202


# Polisi yaomba msaada Interpol

**Na Beatrice Moses**

JESHI la Polisi limesema linaunganisha nguvu na Polisi Kenya kupitia Shirika la Kimataifa la Polisi (Interpol) kuchunguza tukio linalomhusu mfanyabiashara wa Kenya, Raphael Ongangi, aliyedaiwa kutekwa hivi karibuni.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, alisema wanachunguza mazingira ya kupatikana kwa Ongangi ambaye alidaiwa kutekwa nyara nchini Tanzania wiki iliyopita na kupatikana juzi Mombasa, Kenya. Tukio hilo linahusishwa na mambo ya kisiasa.

"Nilizungumza na afande IGP kuna maagizo amenipa tunayafanyia kazi. Tunaendelea kuwasiliana na wenzetu Interpol, tutawafikia wenzetu wa Kenya ili kujua mazingira yaani mtekaji akuteke Tanzania akuchukue hadi Mombasa, ukutwe karibu na shangazi yako!" Alisema.

"Hatuelewi chanzo cha habari hii maana taarifa zenyewe zilikuwa zinatia shaka, tunachunguza kama ni tukio la kutengeneza muhusika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Mambosasa alibainisha kuwa taarifa zenyewe zilitolewa kwa shaka kubwa hasa kwa kuwa mtoa taarifa pia aliwahi kutoa madai ya kutaka kutekwa.

"Mwaka juzi nilipokuwa kule Dodoma yeye mwenyewe aliwahi kuzua kuwa yeye anataka kutekwa, lakini nilimwambia kuwa Jeshi la Polisi linafuatilia hilo. Hakuna yeyote aliyesema hayo labda kama anataka kujiteka ajiteke mwenyewe," alisema Mambosasa bila kumtaja jina mtoa taarifa huyo.

Ongangi alidaiwa kutekwa akiwa na mkewe, Veronica Kundya, Jumatatu usiku katika maeneo ya Oysterbay jijini Dar es Salaam na watu wenye silaha ambao baadaye walimshusha mkewe na kuondoka naye. Wakati huo huo, Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, wamewaua watu wawili wanaodaiwa kuwa majambazi.

Hata hivyo, Kamanda Mambosasa alisema kuwa majina ya watu hao bado hayajafahamika.

Alisema Julai Mosi, mwaka huu, majira ya saa 8:30 mchana katika maeneo ya Kitunda Machimbo, kikosi kazi maalum cha kuzuia na kupambana na majambazi kikiwa maeneo hayo kwa ajili ya kufuatilia majambazi sugu, kilikutana uso kwa uso na watu wawili ambao walianza kuwarushia risasi baada ya kubaini kuwa wamezingirwa na askari.

Mambosasa alisema baada ya mapambano hayo, majambazi hao walijeruhiwa na kupelekwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na baada ya daktari kuwachunguza, alithibitisha wamefariki dunia na miili ya marehemu imehifadhiwa hospitalini hapo.

Alibainisha kuwa polisi walipata silaha walizokuwa wakitumia majambazi hao ambazo ni bastola mbili aina ya Browning yenye namba A.558816 ikiwa na risasi tatu ndani ya magazine na nyingine yenye namba A.963815 TZCAR 101418 ikiwa na risasi mbili.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa (kulia), akipata maelezo kuhusu hatua zilizofikiwa kukifufua kiwanda cha kutengeneza vipuri cha Kilimanjaro Mashine Tools Ltd (KMTC), kutoka kwa Meneja Mkuu, Andriano Nyaluke, alipokitembelea wilayani Hai, mkoani Kilimanjaro. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Mbaroni tuhuma kulawiti mama mzazi na bibi kizee

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, linawashikilia watu wawili akiwamo mkazi wa Manchali, Mizengo Chilatu (28) anayetuhumiwa kumbaka mama yake mzazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Gilles Muroto, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa Chilatu anadaiwa kumbaka mama yake mzazi baada ya kumvizia chumbani akiwa amelala.

"Chanzo ni ulevi wa kupindukia na imani za kishirikina. Mtuhumiwa amekamatwa na atafikishwa mahakamani,"alisema Muroto.

Katika tukio lingine, Muroto alisema Mkazi wa Nzuguni jijini hapa, Donald Justine (25) anashikiliwa kwa kumbaka kikongwe wa miaka 95.

Alisema tukio hilo lilitokea maeneo ya Nanenane, Nzugunina mbinu aliyoitumia mtuhumiwa huyo ni kumvizia chumbani wakati amelala, akamkaba shingoni asipige kelele na kumbaka kwa nguvu.

Kadhalika alisema mtu mmoja anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 25 hadi 30 ambaye majina yake hayajafahamika, ameuawa baada ya kubaka watu watatu kwa nyakati tofauti mtaa wa Maili Mbili jijini hapa.

Kwa mujibu wa Muroto, baada ya kudaiwa kufanya matukio hayo, wananchi walimkamata na kumshambulia kwa kipigo na kuokolewa na askari polisi lakini alifikishwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma akiwa amefariki dunia.

"Tukio la kwanza alitenda Juni 23, mwaka huu, saa moja asubuhi kwa kumbaka bibi kizee wa miaka 80 baada ya kumvizia akiwa chooni na kumkaba shingo," alisema.

Kamanda huyo alisema tukio la pili anadaiwa kulifanya Julai 3, mwaka huu, saa 2:00 asubuhi kwa kumbaka mtoto wa miaka minne baada ya kumshika kwa nguvu na kumvutia kichakani.

"Tukio la tatu alilifanya Julai 3, mwaka huu, majira ya 4:00 asubuhi. Alimbaka mtoto wa miaka minane ambaye ni mwanafunzi wa darasa la pili baada ya kumkamata kwa nguvu na kumvutia kwenye pagala la nyumba,"alisema.

Kutokana na matukio hayo, Muroto alisema wananchi walimkamata na kumshambulia kwa kipigo kilichosababisha kufariki dunia.

# Wema aachiwa huru, kisha akamatwa tena

**Na Hellen Mwango**

SAKATA la kesi ya kuchapisha picha za ngono iliyokuwa inamkabili msanii wa filamu nchini, Wema Sepetu (30), limechukua sura mpya baada ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, kumwachia huru kutokana na upande wa Jamhuri kushindwa kuita mashahidi.

Mahakama hiyo ilimwachia Wema jana chini ya Kifungu cha Mwenendo wa Sheria ya Makosa ya Jinai (CPA) 225 kifungu kidogo cha (5) sura ya 20, lakini alikamatwa tena.

Uamuzi huo ulitolewa jana saa 4:40 asubuhi katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde.

Kabla ya uamuzi huo, upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Glory Mwenda, ulidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kusikilizwa na kwamba shahidi waliyemtegemea, mpelelezi Koplo Safi ni mgonjwa.

Alidai kuwa wanawategemea mashahidi wawili na kwamba mbali ya Koplo Safi, shahidi mwingine yuko jijini Arusha, hivyo kuiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kusikiliza.

Hata hivyo, upande wa utetezi ukiongozwa na Mawakili Albart Msando na Rubern Semwanza, ulipinga ombi la Jamhuri.

Msando alidai kuwa kwa mujibu wa maelekezo ya mahakama hiyo, ilipotoa uamuzi wake mwezi uliopita, ilisema kwamba katika kutenda haki inazingatia hoja za pande zote mbili yaani Jamhuri na utetezi.

Alidai kuwa upande wa Jamhuri ulipaswa kuwasilisha vielelezo kuthibitisha kwamba shahidi ni mgonjwa na lini atahudhuria kesi hiyo.

Pia alidai kuwa mpaka sasa hakuna hati ya kiapo cha Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (RCO) cha kuomba kuongezewa siku 60.

"Mahakama hii haiwezi kumnyima haki mshtakiwa chini ya kifungu cha 225 kidogo (5) cha CPA na uamuzi huo hauwezi kuunyima haki upande wa Jamhuri kumfungulia upya mashtaka pale watakapokuwa tayari kuendesha kesi hii," alidai Msando wakati akiwasilisha hoja za kuomba mteja wake kuondolewa mashtaka.

Akijibu hoja za utetezi, Wakili Mwenda alidai kuwa suala la ugonjwa ni la kibinadamu, shahidi alipokea hati ya wito wa mahakama lakini ameshindwa kwenda mahakamani kwa sababu ya ugonjwa.

Kuhusu kiapo cha RCO cha kuongeza muda, alidai kuwa kinatumika pale upelelezi unapokuwa haujakamilika lakini kesi hiyo inasikilizwa.

Akisoma uamuzi wake, Hakimu Kasonde alisema amesikia hoja za pande zote mbili, kifungu kinachomtaka RCO kuongeza siku 60 kinatumika kabla ya upelelezi na wakati wa usikilizwaji wa kesi.

Alisema Machi 19, mwaka huu, kesi hiyo ilipangwa kusikilizwa lakini ilipigwa danadana mpaka Aprili 18, mwaka huu na mahakama yake ilitoa ahirisho la mwisho.

"Tangu mahakama yangu itoe ahirisho la mwisho mpaka leo (jana) ni miezi miwili. Maofisa wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) walibaini tukio la mshtakiwa kupitia mtandao wa Instagram wakalijulisha Jeshi la Polisi lakini mpaka leo (jana) hawajafika kutoa ushahidi," alisema na kuongeza:

"Mahakama ina muda wake wa kusikiliza kesi kuendelea kumshikilia mshtakiwa wakati ana majukumu mengine kama kilimo, biashara na mambo mengine yanayoongeza uchumi na ujenzi wa taifa si sahihi. Nakubaliana na

INAENDELEA UK.8

# Aliyejifungua mapacha wanne aomba msaada

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKAZI wa Mtaa wa Kameta, Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, Felister Mwanyale (31), ambaye juzi alijifungua watoto wanne, anaiomba serikali na wadau kumsaidia kumudu mahitaji ya msingi ya watoto hao.

Akizungumza jana katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Rukwa, mjini hapa, Mwanyale alisema anahitaji msaada kuwalea watoto hao kutokana na hali ngumu ya maisha inayomkabili.

Alisema huo ni uzazi wake wa saba na amejifungua mapacha mara sita isipokuwa uzazi wake wa kwanza alijifungua mtoto mmoja.

Katika uzazi wa pili, alijifungua watoto watatu na mmoja alifariki dunia, uzazi wa tatu watoto wawili lakini wote walipoteza maisha, uzazi wa nne watoto wawili ambao wapo, wa tano wawili wako hai na ule wa watoto wawili ambao pia wapo. Uzazi wa sasa amejifungua katika Kituo cha Afya cha Mazwi, Sumbawanga mjini.

Alisema mpaka hivi sasa amekuwa akiwalea watoto hao peke yake kwa kusaidiwa na mama yake mdogo baada ya wanaume wanaozaa naye kumtelekeza bila kumsaidia kuwalea.

Mwanyale alisema yeye na mama yake mdogo ambaye ni mkulima, wanaishi kwenye nyumba ya kupanga na wanakabiliwa na maisha duni kiasi kwamba hata hao watoto wengine ameshindwa kuwapeleka shuleni kutokana na ugumu wa maisha.

Mhudumu wa Afya Kitengo cha Watoto Wachanga katika hospitali hiyo, Subira Wilson, anayemhudumia mama huyo mzazi alisema walimpokea juzi majira ya saa 8:00 mchana baada ya kupewa rufani kutoka Mazwi na kwamba yuko chini ya uangalizi maalumu pamoja na watoto wake lakini wanaendelea vizuri.

Alisema kuwa changamoto aliyo nayo mama huyo na watoto wake ni ukosefu wa mahitaji kama vile chakula cha mama, nguo za kuwafunika watoto, poda, maziwa na mafuta ya kupaka.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Rukwa, Dk. Kelly Msafiri, alisema watoto hao baada ya kupokewa hospitalini hapo walihudumiwa na daktari bingwa wa kinamama na wametunzwa katika chumba cha joto.

Alisema watoto hao walizaliwa na uzazi mdogo kwa kuwa wa kwanza alikuwa na uzito wa kilo 1.4, wa pili kilo 1.2, watatu kilo 1.3 na wa nne kilo moja.

Dk. Msafiri alisema kuwa watoto hao wamezaliwa wakiwa njiti ambao ujauzito ulikuwa umefikisha miezi minane, hivyo wanahitaji uangalizi maalumu ili wapete joto na kuwakinga na maambukizi. Alisema kuwa mama huyo anahitaji msaada wa serikali na wadau mbalimbali kwa kuwa kuwalea watoto hao ni changamoto kubwa kwa sababu wana mahitaji mengi ikiwamo ni pamoja na mavazi, mafuta na maziwa kwa vile ya mama pekee hayatoshi kuwanyonyesha wote. Dk. Msafiri alisema kwa sasa mama huyo anapatiwa chakula na hospitali hiyo lakini changamoto kubwa ni pale atakaporuhusiwa kurudi nyumbani kwa sababu suala la lishe kwake na watoto wake ni muhimu ili kuendelea vizuri pamoja na mama yao.

## HABARI KITAIFA

# 46 washikiliwa madai ya wizi, unyang'anyi

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WATU zaidi ya 46 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza, kwa tuhuma za wizi na unyang'anyi.

Watuhumiwa hao walikamatwa katika operesheni maalum iliyofanyika kuanzia Juni 4, mwaka huu. Watu hao wanadaiwa kujihusisha na makosa mbalimbali yakiwamo unyang'anyi, kukutwa na fedha za kigeni bandia (dola za Marekani), wizi wa vifaa vya magari, usafirishaji, uuzaji na utumiaji wa dawa ya kulevya na uhalifu wa kuvunja nyumba usiku na kuiba.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Jumanne Murilo, alithibitisha kukamatwa kwa watuhumiwa hao, na kueleza kuwa walifanya matukio hayo nyakati tofauti katika maeneo ya Ziwa Victoria ya Kunene, Bwiro, Kweru na Irugwa wilayani Ukerewe, visiwa vya Bezi na Makobe wilayani Ilemela na Sengerema katika visiwa vya Kasarazi, Ziragura Iyonze na Maisome. Kamanda Murilo alisema kwamba watuhumiwa waliokamatwa katika maeneo hayo ni 21.

"Watuhumiwa hao walikutwa wakiwa na injini 21 za mitumbwi, nyavu 195, pikipiki mbili aina ya San LG na Nisani ambazo namba zake zilikuwa zimefutwa na watuhumiwa sita wanojihusisha na noti bandia 100 za dola zenye na walikatwa wilayani Nyamagana na kati yao mmoja alikatwa wilayani Sengerema akiwa na noti bandia 32 za shilingi 10,000," alisema Murilo.

Walisema watuhumiwa wengine watano ambao wanadaiwa kuvunja nyumba usiku na kuiba TV saba za aina mbalimbali pamoja na majiko na mitungi ya gesi, laptop ambavyo baadhi vimeshatambuliwa pamoja na watuhumiwa tisa wa vifaa vya magari (vipuri) kwenye makazi ya watu.

"Watuhumiwa wengine watano katika maeneo ya Magu na Igoma kwa nyakati tofauti tulifanikiwa kuwakamata wakiwa na jumla ya kilogramu78.28 za dawa za kulevya aina ya mirungi," alisema Murilo.

Kwa mujibu wa Murilo, Jeshi hilo la Polisi linaendelea kuwahoji watuhumiwa, na mahojiano yatakapokamilika watafikishwa mahakamani.



Mamalishe akivuka barabara ya Shekilango, wakati akienda kuhudumia wateja wake katika eneo la Sinza Mugabe, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**






# RC aeleza sababu umaskini Simiyu

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Antony Mtaka, ameeleza sababu za mkoa huo kushika nafasi ya pili kutoka mwisho katika mikoa inayoongoza kwa kiwango cha umaskini wa kipato Tanzania Bara.

Amesema sababu kubwa ya kufikia hatua hiyo ni kutokuwapo kwa mwamko wa elimu kwa wananchi tangu zamani na kufanya idadi kubwa ya wananchi wasio na elimu.

Mtaka alisema hayo jana wakati akizungumza na madiwani wa Halmashuari ya Wilaya ya Bariadi kwenye kikao cha baraza kujadili taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kilichofanyika mjini hapa.

Alisema bila wananchi wa mkoa na viongozi wote kubadilika na kuwekeza katika elimu, Simiyu itaendelea kushika nafasi za mwisho kwa umaskini wa kipato.

Kiongozi huyo alisema mikoa yote ambayo imeongoza kwa kiwango kidogo cha umaskini, imewekeza katika elimu huku zikiwako shule nyingi za kidato cha tano na sita pamoja na vyuo.

"Lazima tuwekeze sana katika elimu, bila ya kufanya hivyo hatuwezi kuvuka hapa. Lazima watu wabadilike, elimu ndiyo kila kitu. Hizi nguvu ambazo tunazifanya hapa hazitafanikiwa kama tutakuwa na watu ambao hawana elimu," alisema.

"Watu wanatakiwa kubadilika na kuona elimu ndiyo mkombozi wa maisha yetu, tuachane na mila potovu, kuozesha watoto katika umri mdogo, kuwakatisha masomo na kuwaozesha," aliongeza.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka viongozi kuungana na serikali katika juhudi zake za kuongeza shule nyingi za kidato cha tano na sita na vyuo mbalimbali vya ufundi na taaluma.

Hivi karibuni, Ofisi ya Taifa Takwimu (NBS) ilitoa takwimu za mikoa yenye kiwango cha umaskini na kipato zilizoonyesha kuwa mkoa wa Simiyu umeshika nafasi ya pili kutoka mwisho ukiwa na asilimia 39.2 nyuma ya Rukwa wenye asilimia 45.

# Magereza yatekeleza agizo la JPM

**Na Mwandishi Wetu**

JESHI la Magereza limeanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli kwa kuhamisha wafungwa 1,535 kwenda kwenye magereza 10 ya kimkakati kwa ajili ya kuzalisha chakula kutosheleza mahitaji yake na ziada kuuzwa.

Msemaji wa Jeshi hilo, Mrakibu (SP) Amina Kavirondo, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa wafungwa hao wamepelekwa katika magereza hayo ikiwa ni kutekeleza agizo la Rais Magufuli la kutaka rasilimali waliyo nayo itumike ipasavyo ili kuleta tija na kupunguza utegemezi kwa serikali.

Kavirondo aliyataja magereza walikohamishiwa wafungwa hao kuwa ni Songwe, Kitai, Ludewa, Kitengule, Mollo, Pawaga, Idete, Kiberege, Kitete na Nkasi. Pia alisema gereza la Arusha halikupokea nguvu kazi mpya kwa kuwa wafungwa walioko wanajitosheleza katika uzalishaji.

Mwishoni mwa mwaka jana, Rais Magufuli alifanya ziara ya kushtukiza katika Gereza Kuu la Ukonga, Dar es Salaam na kuagiza jeshi hilo kujitathmini kwa kuwa wana rasilimali nyingi ambazo zikitumika vizuri, halitakuwa na haja ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini.

Rais Magufuli alisema Magereza ni kati ya taasisi za serikali zenye maeneo makubwa kuliko taasisi nyingine yoyote ya uzalishaji lakini cha ajabu inasubiri fedha za serikali ili kulisha wafungwa badala ya wafungwa kuzalisha chakula chao na ziada kuuzwa kwa ajili ya kupata fedha kwa ajili ya kununulia mahitaji mbalimbali na hata kujenga majengo yake yenyewe.

Alisema ni aibu kwa serikali kupanga bajeti

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Waziri atahadharisha tishio ongezeko la watu uhifadhi

**Na Elizabeth Faustine,**
MWANZA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangalla, ametahadharisha kuhusu ongezeko la watu nchini, akitaka mikakati kabambe kuhakikisha hifadhi za taifa na maeneo tengefu yanalindwa dhidi ya tishio hilo.

Dk. Kigwangalla aliyasema hayo jana jijini Mwanza alipofungua mkutano wa mwaka wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) na wahariri na waandishi waandamizi nchini.

Katika mkutano huo uliokwenda sambamba na maadhimisho ya miaka 60 ya Tanapa, waziri huyo alisema ustawi wa uhifadhi uko hatarini kutokana na changamoto mbalimbali, ikiwa ni pamoja na ongezeko la watu.

Alisema idadi ya watu Tanzania kwa sasa inakadiriwa kuwa kati ya milioni 50 na 60, lakini katika miaka 10 ijayo, idadi hiyo inatarajiwa kufikia watu milioni 100, hivyo akashauri kuwe na mikakati ya kulinda hifadhi dhidi ya uvamizi.

"Baada ya miaka 50 ijayo, idadi ya watu nchini inatarajiwa kuwa zaidi ya milioni 200, lakini ardhi inabaki kuwa ile ile. Hii ni changamoto kwa sababu presha itakuwa kubwa kwenye maeneo ya hifadhi na ikolojia kwa sababu ardhi haitatosha watu wote.

"Sasa, kwa kuzingatia hilo, ni lazima tulinde hifadhi zetu ili ziendelee kuchangia uchumi wa nchi kwa kuingiza fedha za kigeni, hifadhi zetu pia ni chanzo cha hewa muhimu kwa maana ya oksijeni, maji na hata mbao.

"Lazima tuhakikishe usalama wa taifa letu unakuwapo na jambo hili sharti tuliwekee mikakati leo maana Tanzania bila hifadhi, haiwezi kuwa na hadhi iliyonayo kwa sasa kiuchumi.

"Tusiangalie maslahi yetu tu sisi tuliopo kwa sasa, tuache ubinafsi, tuchukue hatua kwa pamoja kuhakikisha hifadhi zetu zinaendelea kuwepo kwa maslahi ya kizazi cha sasa na kijacho," Dk. Kigwangalla alisema.

Waziri huyo aliongeza kuwa sekta ya utalii na uhifadhi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi, akibainisha kuwa kwa sasa inachangia asilimia 17 ya Pato la Taifa, asilimia 25 ya fedha za kigeni na imetoa ajira za moja kwa moja zaidi ya 600,000 na zisizo rasmi zaidi ya milioni mbili.

Alisema wabunge wengi kwa sasa 'wanalia' na changamoto ya

INAENDELEA UK. 8

# Waziri akaribisha meli za kimataifa Bandari ya Dar

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amewataka wamiliki wa meli duniani kuleta meli zao katika Bandari Kuu ya Dar es Salaam kwa sababu imefanyiwa ukarabati mkubwa na kuwa na kina kirefu kinachoweza kupokea meli kubwa zote duniani.

Kwa mara ya kwanza juzi meli kubwa yenye shehena ya mbolea imetia nanga katika gati namba mbili ya bandari hiyo, ambalo ujenzi wake umekamilika na kuwa na urefu wa kina cha mita 15.

Waziri Kamwelwe alitoa wito huo jana, wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wake na wamiliki wa meli kubwa za kubeba mizigo duniani kwa lengo la kujadili changamoto zilizopo katika bandari hiyo ili ziweze kufanyiwa kazi.

Alitaja kampuni walizokutana nazo ni Maersk, MSC, CMA na PIL inayoleta mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam moja kwa moja ambao kwa pamoja walishauriana namna ya kuboresha huduma ili meli zao ziweze kutia nanga katika Bandari ya Dar es Salaam.

"Leo (jana) tumefanya mkutano mwingine na wamiliki wa meli kubwa duniani ikiwa ni mwendelezo wa mkutano wetu na wachimbaji wakubwa wa madini duniani uliofanyika jana (juzi) wito wetu kwa matajiri hawa ni kuwaomba watumie bandari yetu ya Dar es

INAENDELEA UK. 8


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**TAARIFA KWA MAFUNDI SIMU ZA MKONONI NA VIFAA VYA KIELEKTRONIKI**

Kumekuwa na mwitikio mzuri sana kwa Mafundi wa simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki katika kupata mafunzo maalum ya kitaalamu tangu mafunzo hayo yaanze kutolewa kuanzia tarehe 23/07/2018 hadi sasa. Ni dhahiri kuna uhitaji mkubwa wa kuwa na Mafundi wa simu za mkononi waliofundishwa vema na wenye kuzingatia taratibu na sheria katika kazi zao, ili kuwa na uhakika wa mawasiliano salama kwa watumiaji wa vifaa hivyo.

Kwa kipindi cha mwaka mmoja Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania **(TCRA)** kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam **(DIT)** na Vyuo vya Ufundi Stadi **(VETA)** wamekuwa wakitoa mafunzo kwa Mafundi simu hao ambapo wanafunzi 144 wamehitimu mafunzo hayo na kati yao wanafunzi 110 wamefanikiwa kupata vyeti vya usajili kutoka **TCRA.**

Mafunzo haya yataendelea kutolewa tena kikanda kama ifuatavyo; **Kanda ya Ziwa** (Mwanza, Simiyu, Mara, Shinyanga, Geita na Kagera), **Kanda ya Kaskazini** (Arusha, Kilimanjaro, Manyara na Tanga), **Kanda ya Kati** (Dodoma, Tabora, Kigoma na Singida), **Kanda ya Mashariki** (Dar es Salaam, Mtwara, Pwani na Morogoro), **Kanda ya Nyanda za Juu Kusini** (Mbeya, Songwe, Njombe, Ruvuma, Iringa, Rukwa na Katavi) na **Ofisi ya Zanzibar** (Unguja Mjini Magharibi, Unguja Kaskazini, Unguja Kusini, Pemba Kaskazini, Pemba Kusini).

Aidha, tumeshuhudia pia mwitikio mzuri wa Mafundi simu na vifaa vya kielektroniki katika kujisajili na kupata cheti cha **TCRA** ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kuwa na Mafundi simu wenye ujuzi, **TCRA** inapenda kuwatangazia kuwa kuanzia tarehe **1 Julai 2020** Mafundi wote wa simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki **ambao hawajasajiliwa na TCRA** hawataruhusiwa kutoa huduma ya kutengeneza simu za Kiganjani na vifaa vya kielekroniki. Sharti kubwa la kupata usajili wa **TCRA** ni kuwa wamepitia mafunzo ya awali ya ufundi wa simu za kiganjani na vifaa vya kielekroniki yanayotolewa na **DIT** au **VETA.**

Imetolewa na:

MKURUGENZI MKUU

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA (TCRA)**

215302601

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Homa Dengue bado tishio, tusibweteke wagonjwa kupungua

**MARA** nyingi kuna tabia ya jamii kubweteka na kuacha kuchukua tahadhari pale tatizo linalowakabili linapopungua au kwisha kabisa.

Hali hiyo ya jamii kubweteka imekuwa ikitokea kwa changamoto mbalimbali, yakiwamo magonjwa. Kwa miezi kadhaa mwaka huu, uliibuka ugonjwa wa homa ya Dengue katika mikoa mbalimbali nchini.

Ugonjwa huo umesababisha athari kubwa kwa familia kadhaa, vikiwamo vifo, hali iliyoifanya serikali kuchukua hatua mbalimbali kuhakikisha kwamba hayatokei madhara zaidi.

Miongoni mwa hatua hizo ni kutoa elimu kwa umma kuhusiana na chanzo cha homa ya Dengue, hatua za kuchukua hususan kuwahi katika vituo vya huduma za afya kwenda kupima pamoja na kutengwa kwa vituo rasmi vya huduma kwa ajili hiyo.

Elimu kwa umma kuhusiana na tahadhari ya kuchukua pia imekuwa ikiendana na hatua za serikali za kupulizia dawa katika maeneo ya makazi hususan yenye mazalia ya mbu. Kadhalika, serikali imewawekea mazingira mazuri wananchi ya kupima homa hiyo bila malipo.

Kimsingi, tunathubutu kusema kuwa ugonjwa huo umekuwa janga kubwa kwa Watanzania, kutokana na familia kadhaa kupoteza wapendwa wao.

Katika hali inayotoa matumaini, serikali imesema kuwa sasa kuna ahueni kutokana na kupungua kwa wagonjwa wanaougua Dengue.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ndiye aliyesema hayo juzi jijini Dar es Salaam alipokuwa anawaongoza wakazi Manispaa ya Ilala kupulizia dawa ya kuua mazalia ya mbu aina ya Dengue, na kueleza kuwa idadi ya waliougua imepungua kutoka watu 2,759 mwezi Mei hadi wagonjwa 790 mwezi uliopita.

Hakika hizi ni habari njema na ni za kutia moyo na matumaini kwamba hatua za tahadhari zilizochukuliwa zimewezesha kupunguza makali ya ugonjwa huo.

Hilo pia linapaswa kutupa funzo kwamba yanapotokea majanga kama hayo, jamii nzima iwe na mwitikio chanya kwa kuchukua hatua haraka bila kusubiri athari kuwa kubwa zaidi.

Jambo la msingi ni jamii kuendelea kuchukua tahadhari na kutochukulia kuwa ugonjwa huo umetokomea kabisa, kwa kuwa kwa kufanya hivyo ni kuukaribisha upya.

Wananchi waendelee kusafisha mazingira yao hususan kuhakikisha kwamba mazao ya mbu yahabaribiwa ili mbu aina ya Dengu wasiweze kutaga mayai pamoja na kuhakikisha wanatumia vyandarua.

Kwa upande wake, mamlaka zetu ikiwamo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na halmashauri zote ziendelee kutoa elimu na kuhamasisha umma kuchukua hatua za tahadhari.

Mamlaka hizo pia ziendelee kusimamia usafi hususan unyunyiziaji dawa za kuua mazalia ya mbu na kuhakikisha kwamba vituo vya kutolea huduma za afya vinaendelea kupiga homa ya Dengue bila malipo, lengo kuwawezesha wananchi wengi kujitokeza kupoma mapema kabla ya kupata madhara makubwa.

Wito wetu kwa wananchi ni kwamba pamoja na kauli ya Waziri Ummy kuwa wagonjwa wa homa ya Dengue wamepungua, lakini wasibweteke, bali tahadhari iwe endelevu.

Pamoja na kuchukua tahadhari, tunawashauri pia mtu akisikia dalili za homa hiyo, jambo la kufanya ni kukimbilia katika vituo vya huduma za afya kupima.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Pipi, biskuti hizi shuleni zifuatiliwe

Na Sabato Kasika

**BAADHI** ya walimu katika shule za jijini Dar es Salaam, wanadai kwamba kumekuwapo na pipi na biskuti zinazouzwa karibu na maeneo ya shule, wanazodhani huenda, zinatengenezwa kwa vitu ambavyo si salama kwa afya na ustawi wa wanafunzi.

Kutokana na hali hiyo, walimu hao wanaiomba serikali kufuatilia kwa karibu viwanda vinavyozalisha pipi hizo na biskuti ili kuhakikisha kama zinafaa kutumiwa na wanafunzi au ni hatari kwa afya zao.

Maombi hayo waliyatoa hivi karibuni kwenye warsha ya kutoa taarifa ya utendaji kazi wa kamati za kuzuia ukatili dhidi ya watoto shuleni ilioandaliwa na asasi ya kiraia ya Ekama Development Tanzania.

Walimu hao wanasema karibu maeneo yote ya shule kuna vibanda vinauza vitu mbalimbali zikiwamo pipi na biskuti ambazo nyingine zina harufu ya kahawa au sigara, hali ambayo wanadhani siyo salama kwa watoto.

Warsha hiyo ilishirikisha wadau zaidi ya 150 wakiwamo maofisa wa ustawi wa jamii, polisi walimu, wanafunzi, wazazi na viongozi wa dini, ambao kila upande ulitoa maoni kuhusu mambo mbalimbali.

"Inawezekana hata wauzaji wakawa hawajui kuhusu pipi na biskuti hizo, lakini kuna haja serikali kufuatilia ili kubaini kama zina madhara au hazina ili watoto wetu wawe salama," anasema mmoja wa walimu.

Anaeleza kuwa anajua watoto wanakumbana na changamoto nyingi zikiwamo za kuingia katika vibanda vya video mitaani, ambavyo vinachangia ukatili kwao, lakini pia suala la biashara katika maeneo ya shule ni la kufuatiliwa kwa karibu.

Mwalimu huyo anataka biashara holela kwenye maeneo ya shule idhibitiwe ili kulinda afya za wanafunzi kuliko kuacha kila mtu akifanya anavyotaka na mwisho wa siku wanaweza kusababisha madhara.

Vilevile anawashauri wazazi kuwa makini kwa kuwapa watoto wao maelekezo ya kutambua ni vitu gani vya kununua wawapo shuleni kuliko kununua kila wanachotaka, kwa vile wanaweza kujikuta wakinunua visivyofaa.

Anataka ikiwezekana, mtoto apewe chakula kutoka nyumbani kuliko pesa ambazo anajikuta ananunua hata vitu visivyofaa na kwamba anajua watoto wanapenda pipi na biskuti, lakini pia ni muhimu wakaelezwa madhara yake.

Kutokana na ushauri wa mwalimu huyo ni vyema mamlaka husika zikafuatilia biashara hiyo na pia wazazi kuwa makini wanapowapa watoto wao pesa za kutumia shuleni ili kuepuka kuwaingiza kwenye hatari.

Wakati mwalimu huyo akisema hayo, bado pia kuna haja ya kufuatilia maji yanayofungwa kwenye mifuko myeupe ya nailoni, ambayo ni maarufu kwa jina la 'Kandoro', nayo yanadaiwa kuwa hatari.

Maji hayo yamekuwa yakiuzwa mitaani na hata kwenye maeneo ya shule yatakuwa yanapatikana, kwani huchangamkiwa sana na watoto kutokana na kuuzwa kwa bei nafuu.

Jambo la kuzingatia ni kwamba maji hayo huwa hayachemshwi, hivyo si salama kwa wanywaji, ndio maana nikasema kuwa biashara hiyo nayo ifuatiliwe na kupigwa marufuku ili kulinda afya za watu.

Ni muhimu wanaofanya biashara hiyo wakawa makini ili kubaini taarifa ambazo zinalalamikiwa na walimu ili kulinda afya za wanafunzi kuliko kufanya kiholela na kusababisha wasiwe salama.

Waswahili wana msemo usemao; lisemwalo lipo, kama halipo, laja, hivyo inawezekana kinacholalamikiwa na walimu kina ukweli na kama hakipo, basi kinaweza kujitokeza baadaye.

Hii inatokana na ukweli kwamba hata baadhi ya wabunge walishawahi kulalamika kwamba kuna baadhi ya pipi zenye dawa za kulevya zilizokuwa zikiuzwa kwenye maeneo ya shule huku wanafunzi wakitumia bila kujua.

Kwa hali kama hiyo ni wazi kwamba inawezekana hata wauzaji nao wasijue kwamba wanauza pipi au biskuti zenye dawa za kulevya, hivyo ni vyema wakawa makini wanapochukua bidhaa za kuuza.

Bila kufanya hivyo, wataendelea kuweka rehani afya za wanafunzi kwa kutojua au kwa kujua ili mradi tu wapate pesa hata kwa njia ambayo inahatarisha afya za wengine.

## BARUA/MJADALA

### Barua ya wazi kwa mkurugenzi Mkuu wa Veta

**Chuo cha Veta Oljoro kimulikwe.**

*TUNAOMBA chuo hiki kiangaliwe mwenendo wake, kwani kuna masuala kadhaa yanayotia shaka katika utendaji wake.*

*Mojawapo ni matumizi mabaya ya fedha na rasilimali za umma. Mfano mwaka huu wa 2019, mnamo msimu wa kilimo, chuo kilitumia fedha nyingi kulima eneo lote la mashamba ya chuo yapatayo ekari 1000 hivi.*

*Lakini kikapanda mazao eneo dogo tu la karibia ekari 100 hadi 150, huku eneo jingine likiachwa bila ya kupandwa chochote, wakati fedha nyingi imetumika kuliandaa.*

*Aidha, sehemu ya eneo hilo imekuwa ikigawanywa na kupewa wananchi walime ili kujikimu kwa chakula. Lakini mwaka huu hawakupewa kwa madai ya kuwa chuo kimeamua kulilima eneo lake lote, lakini matokeo yake eneo kubwa likaachwa bila kupandwa zao lolote. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za umma.*

*Tatizo jingine ni matumizi mabaya ya ofisi na utendaji usiozingatia na mifumo na taratibu zilizowekwa. Mfano, hata maamuzi ya kulima eneo lote la mashamba ya chuo, hayakuzingatia taratibu zilizowekwa. Kwamba kamati ya shamba iliyopo kwa mujibu wa taratibu na ile ya uzalishaji mali, hazikuhusishwa kikamilifu katika kufikia uamuzi wa kulima shamba lote, badala yake watu wachache tu ndio waliamua kufanya hivyo.*

*Suala lingine ni ubadhirifu wa fedha za umma. Mathalani hivi karibuni mwaka huu ulifanyika ukarabati wa majengo kadhaa (bwalo la chakula pamoja na tangi la maji kwa ajili ya akiba). Kazi hizo ambazo zote zingaliweza kufanywa kwa kutumia rasilimali watu wa ndani, badala yake mafundi waliajiriwa kutoka nje kukarabati majengo ya chuo, wakati chuo chenyewe ni chuo cha ufundi.*

*Kwa kutumia ujuzi wa ndani, chuo kingeliweza kutumia gharama ndogo, lakini kwa vile mafundi wa nje hutoa chochote kwa mtoa kazi, walipewa kazi hizo ambavyo hata hivyo zilifanyika chini ya kiwango.*

*Yaani hata miezi mitatu haijaisha, tayari sakafu iliyowekwa upya bwaloni imeshaanza kubomoka.*

*Aidha, tangi la maji ya akiba hadi sasa bado halina msaada wowote wa kuhifadhi maji ya akiba kwani bado linavuja, licha ya kukarabatiwa, hali ambayo huchangia shida ya maji chuoni hasa pale maji yanapokatika tu kwa muda mfupi.*

*Hali hii mara kadhaa imeathiri mwenendo wa mafunzo. Ni vema mamlaka husika zikamulika taasisi hii ya mafunzo ya ufundi stadi kwa ajili ya maslahi mapana ya taifa.*

**Mzalendo Mwananchi, Arusha.**

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Serikali imulike mazingira duni ya utoaji elimu



Baadhi ya wanafunzi wa shule ya msingi jijini Dar es Salaam wakiwa kwenye mkutano. Majukwaa kama hayo yatumike kujadili changamoto za wanafunzi. **PICHA: BEATRICE MOSES**

**Na Beatrice Moses**

**SHULE** nyingi zinatarajiwa kufunguliwa wiki ijayo japo nyingine chache zimefunguliwa juma hili, tunaamini wanafunzi na walimu wamepata nafasi ya kupumzika kwa namna tofauti kulingana na taratibu walizojiwekea.

Pongezi kwa wanafunzi wa darasa la nne, saba pamoja na wa vidato vya pili nne na sita kwa kutopumzika kama wengine wa madarasa mengine kwa kuwa wapo kwenye madarasa ambayo wanakabiliwa na mtihani wa taifa.

Wanafunzi hao wakisaidiwa na walimu wao katika baadhi ya shule walitumia nafasi hiyo kuendelea kujiandaa kukabili mitihani yao na hatimaye waweze kufaulu.

Katika mazingira haya ya kufungua shule wiki ijayo, kuna mambo kadhaa yanajitokeza ambayo yanaweza kuwa ni changamoto au matatizo yanayoweza kusababisha shida kwa mwanafunzi binafsi au jamii kwa ujumla.

Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na mazingira mabaya ya shule, michango isiyokuwa na tija, milo isiyozingatia kanuni za afya, malazi hatarishi na waangalizi wasio na sifa za malezi.

Hivi karibuni gazeti la Nipashe limeripoti kuhusu uwepo wa kunguni katika baadhi ya shule, licha ya Wizara ya Afya kubainisha kuwa wadudu hao hawasababishi magonjwa bali maudhi ni jambo linalopasua vichwa vya wazazi wengi.

Ni wazi kwamba wanafunzi wa shule za bweni zilizo na wadudu hao wanakosa usingizi mzuri hivyo hawana utulivu unaotakiwa, hali ambayo inaweza kuwasababishia kufanya vibaya katika masomo yao kwani umakini katika kujisomea unapungua badala yake wanajikuna kutokana na miwasho. Ni vyema wakaguzi wa shule wakajiridhisha na usafi wa mabweni ili kuwawezesha wanafunzi kuishi katika mazingira ambayo ni rafiki badala ya kuteseka kwa maumivu na miwasho.

Michango baadhi ya shule zimekuwa na michango isiyokuwa na tija badala yake ni mzigo kwa wazazi, licha ya kwamba kwa shule binafsi elimu imekuwa ni biashara siyo huduma ni vyema wakaguzi wakijiridhisha na michango hiyo ikiwamo uagizaji vifaa vingi tofauti na matumizi husika.

Pia baadhi ya viongozi wa shule wamekuwa wakikosa utu wa kushindwa kuzungumza na wazazi inapotokea amekwama kulipa ada kwa wakati licha ya kuwa na historia nzuri ya ulipaji wa ada.

Februari mwaka jana Ofisa Elimu Taaluma mkoani wa Dar es Salaam, Janeth Nsunza, alizungumzia suala hili la michango na ada akiwa kwenye mkutano wa wakuu wa shule zote.

Aliwasihi wakuu wa shule binafsi za Dar es Salaam kuwa na moyo wa huruma kwa kutowafukuza shuleni watoto wanaokwama kulipa ada kwa wakati.

Nsunza alisema inasikitisha baadhi ya wamiliki na wakuu wa shule hushindwa kuwavumilia wazazi wanapokwama kiuchumi, hivyo huwafukuza watoto na wengine kuwataka wale viapo mahakamani.

Alifafanua kuwa kuna mzazi alifika ofisini kwetu, mwanaye alikuwa kidato cha nne mwaka jana, hakuwa na ada akafukuzwa, lakini akaandika barua kwa Kamishna wa Elimu kuomba aruhusiwe kufanya mtihani huo.

Wazazi pia kwa upande wao wanapaswa kujipanga kwa kuhakikisha kuwa wana uwezo wa kulipa ada na michango husika ya shule wanazosoma watoto wao, badala ya kuendekeza starehe na anasa, huku mtoto akisumbuliwa shuleni.

**Chakula, Uangalizi**

Katika suala la mlo wa wanafunzi wa bweni baadhi wamekuwa wakiugua kutokana na ukosefu wa virutubisho kwenye vyakula vya aina mbalimbali.

Mboga za majani zimegeuzwa kuwa vyakula vya anasa kwa baadhi ya shule hupewa wanafunzi wanaoumwa vidonda vya tumbo au wasiokula nyama, wengine wamekuwa wakilishwa maharage kwa wingi na mchuzi wa nyama.

Baadhi ya shule zimekuwa na waangalizi (patron na matron) wazee ambao kutokana na umri wao hushindwa kumudu kuwafuatilia wanafunzi ambao baadhi hutumia mwanya huo kutoroka shule au kufanya vitendo vya kujamiana hivyo kukuza mmomonyoko wa maadili kwa ujumla.

**Sera ya Elimu**

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, inaeleza jinsi usimamiaji, mazingira ya kutolea elimu na mafunzo, tathmini na rasilimali zilizopo, unavyotakiwa kufanyika.

Inaeleza kuwa taifa kwa sasa linakabiliwa na changamoto mbalimbali katika suala la ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote," inabainishwa.

Sera inaeleza kuwa tathmini zinaonyesha kwamba, ili kuimarisha ubora na ufanisi wa elimu na mafunzo nchini, kuna ulazima wa kuinua ubora wa mitaala, ukaguzi wa shule, tathmini, ithibati, na mamlaka zinazohusika na masuala hayo. Idara ya ukaguzi wa shule ina jukumu la kufuatilia ubora wa elimu ya msingi na sekondari kwa kuzingatia mitaala na viwango vilivyowekwa.

Ukweli ni kwamba utendaji wa idara hii umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali na hivyo kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Changamoto hizo ni pamoja na kuendelea kutumia falsafa ya ukaguzi iliyokuwa na tija wakati shule zikiwa chache tofauti na sasa ambapo shule ni nyingi," inaeleza sera hiyo.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Wema aachiwa huru, kisha akamatwa tena

INATOKA UK. 3

ombi la utetezi, namwachia chini ya kifungu cha 225 kidogo cha (5) cha CPA," alisema Hakimu Kasonde Msando.

Hata hivyo, saa 4:43 baada ya kuachiwa, alikamatwa na askari polisi kisha alipandishwa kwenye gari lenye namba za usajili SKA 535 M aina ya Toyota Landcruser na kupelekwa Kituo Kikuu cha Polisi Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (ZCO) Kanda Maalum ya Dar es Salaam.

Saa 6:15 mchana akizungumza na Nipashe, Wakili Msando alisema polisi wamemwachia huru na kwamba watakapomhitaji watamjulisha.

Akiwa nje ya viunga vya Mahakama ya Kisutu, baada ya kuachiwa, Wema alisema anamshukuru Mungu amefurahi ameachiwa dhidi ya kesi hiyo.

Wema aliyekuwa ametinga suti ya suruali ya rangi ya kaki na shati jeupe lenye vidoti vya rangi ya zambarau na viatu vya mchuchumio vyeusi, alifurahia kuwa huru dhidi ya tuhuma hizo.

Katika kesi ya msingi, alikuwa anatuhumiwa kuwa Oktoba 15, mwaka jana katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, alichapisha video ya ngono na kuisambaza katika mtandao wake wa kijamii wa Instagram.



Mafundi wakichora alama ya kutenganisha Barabara ya Mandela, katika eneo la Tabata Matumbi, jijini Dar es Salaam jana.
**PICHA: JOHN BADI**

# Magereza yatekeleza agizo la JPM

INATOKA UK. 4

ya kulisha wafungwa wakati wafungwa wanaweza kufanya kazi na wakazalisha, hivyo akaagiza wafungwa wafanye kazi kwa kuwa hawafanyi kazi vya kutosha.

Kavirondo alisema yako magereza 11 ya kimkakati ambayo wamepelekewa wafungwa ambako kuna miradi 23 ya uzalishaji iliyo chini ya Shirika la Uzalishaji la Jeshi la Magereza la Corporation Sole, ambalo hujishughulisha na kilimo, ufugaji, uvuvi na viwanda.

Alisema baadhi ya viwanda vinavyoendeshwa na Magereza ni vile vya usindikaji wa ngozi za mifugo, utengenezaji wa viatu kwa ajili ya askari na biashara, uzalishaji kokoto na ufyatuaji matofali yanayotumia saruji na udongo.

Pia alisema Jeshi la Magereza lina ardhi yenye ukubwa wa hekta 130,482 na 60,540 kati ya hizo, zimetengwa kwa shughuli za kilimo, hekta 3,000 kwa ajili ya makazi, hekta 47,459 malisho ya mifugo na 50,459 kwa matumizi mengineyo.

Mpaka sasa Tanzania ina magereza makuu 12, magereza ya wilaya 75 na magereza ya wazi 42 yanye uwezo wa kuhifadhi wastani wa wahalifu 380,000 kwa siku. Kwa sasa jumla ya wahalifu wote wanaoshikiliwa nchi nzima ni 36,544 wakiwamo wafungwa 18,205 na mahabusu 18,339.

# Waziri akaribisha meli za kimataifa Bandari ya Dar

INATOKA UK. 5

Salaam kwa sababu sasa tumeboresha huduma," alisema Kamwelwe.

Akielezea meli iliyotia nanga juzi katika bandari hiyo alisema, imesajiliwa Panama kwa jina la Kouyou Tonnage 33126 yenye urefu wa mita 197 na upana mita 32.26, imeleta shehena ya mbolea ambayo itasafirishwa kwenda nchi nyingine ikiwamo Zambia.

Naye Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Prof. Paramagamba Kabudi, aliwataka wafanyabiashara hao wakubwa duniani kupitisha mizigo yao katika bandari za Dar es Salaam na Tanga kwa sababu zina kina kirefu. Aidha, alisema amehudhuria mkutano huo kwa sababu Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na wanashirikiana katika nyanja mbalimbali za kukuza uchumi wa mataifa yao.

"Niko hapa kuwahakikishia usalama wao wamiliki wa meli na wafanyabiashara wanaopitisha mizigo yao katika bandari zetu. Kwanza tumefanya jitihada kubwa za kuboresha bandari pamoja na kumaliza changamoto, jambo lingine amani na usalama ulipo katika nchi yetu," alieleza Prof. Kabudi. Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Bandari Tanzania (TPA), Deusdadus Kakoko, alisema magati matatu yamekamilika katika bandari hiyo yenye kina cha mita 15 kila moja, ambayo yanawezesha meli kubwa duniani kuweza kutua.

"Tayari gati namba moja, namba saba na namba mbili limekamilika jana (juzi) na tayari meli imetua yenye mzigo wa mbolea ambayo itasafirishwa kwenda nchi nyingine kuanzia hapa, tofauti na kipindi cha nyumba bandari zetu zilikuwa zikitumika kupitishia mizigo kwa sababu tulikuwa na kina kifupi," alisema.

# HESLB yawapa mbinu wastaafu

INATOKA UK. 2

"Madeni ya serikali hayana riba, ila yana tozo ili kulinda thamani ya fedha mfano kama unadaiwa Sh. milioni 10 utalipa Sh. milioni 10.6 na kama ulilipa Sh. milioni 5 ukifika mwisho wa mwaka unadaiwa asilimia 6 ya Sh. milioni 5, lengo lake ni kweli kwamba fedha huwa inabadilika thamani lakini siyo kweli kwamba deni la bodi huwa haliishi," alisema.

Meneja wa Habari, Elimu na Mawasiliano wa bodi hiyo, Omega Ngole, aliliambia Nipashe kuwa HESLB haikopeshi mkopo mtu mwenye umri zaidi ya miaka 35, hivyo hata kama mtu atasoma taaluma ambayo inachukua miaka mitano kama udaktari akiwa na umri huo, hadi anamaliza atakuwa na miaka 40 au 41.

"Kama mtu amemaliza chuo akiwa na umri huo tunamshauri ni vyema alipe mkopo wake mapema kwa sababu kadri unavyoendelea kuacha kuna penati, kwa nini usubiri hadi ustaafu ndo uanze kukatwa, lipa mapema na hutakumbana na penati, lipa ili kuruhusu wengine nao wanufaike na mikopo tunayotoa," alisema.

Aliongeza kuwa, "Ukimaliza chuo lipa mkopo wako, usisubiri hadi utafutwe. Ukikimbia utakutana na penati kwenye mkopo uliokopa, ukistaafu ujue tutakupata tu," alisema.

Bodi ya Mikopo ilianzishwa kwa sheria ya Bunge namba 9 ya mwaka 2004 na kuanza rasmi mwezi Julai 2005 kwa majukumu ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu pamoja kukusanya marejesho ya mikopo yote iliyotolewa tangu mwaka 1994.

Hadi mwezi Machi mwaka huu Bodi hiyo ilikuwa imekusanya zaidi ya Sh. bilioni 120 kutoka kwa wanufaika wa mikopo nchini, ikiwa ni madeni ya miezi minane.

Akizungumza Machi mwaka huu jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Ukusanyaji Mikopo wa HESLB, Ignatus Oscar, alisema bodi ilipanga kukusanya zaidi ya Sh. Bilioni 180 ifikapo mwezi Juni mwaka huu.

# Waziri atahadharisha tishio ongezeko la watu uhifadhi

INATOKA UK. 5

upatikanaji wa maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, lakini katika miaka 50 ijayo, watunga sera hao hawatalilia maji kwa ajili hiyo, bali wataibana serikali kuhusu upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Dk. Kigwangalla aliipongeza Tanapa kwa kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi wa shule, zahanati na vituo vya afya kwa lengo la kusaidia jamii, akieleza kuwa suala hilo litaongeza hamasa kwa wananchi kushiriki katika ulinzi wa hifadhi.

Dk. Kigwangalla pia alitumia mkutano huo kumshukuru Rais John Magufuli kwa kukubali kushiriki uzinduzi wa hifadhi mpya ya taifa utakaofanyika Jumanne mkoani Kagera.

Kamishna wa Tanapa, Dk. Allan Kijazi, alisema wamekuwa wakiitumia mikutano hiyo ya kila mwaka na wahariri na waandishi wa habari waandamizi kupata mrejesho na kufanya maboresho katika sekta ya utalii na uhifadhi.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, aliipongeza Tanapa kwa kupeleka mkutano huo mkoani mwake na kuishauri kuishiriki mikoa na wilaya katika kuhamasisha utalii na ulinzi wa hifadhi nchini.

# Pikipiki kutaifishwa kisa magendo ya kahawa

**Na Lilian Lugakingira,**
KARAGWE

SERIKALI ya Wilaya ya Karagwe mkoani Kagera, imewaonya vijana wanaosafirisha abiria kwa kutumia bodaboda, kuacha tabia ya kuvusha kahawa kimagendo kwenda Uganda kwa kutumia bodaboda hizo.

Imesema watakaokamatwa pikipiki zao zitataifishwa, watachukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Onyo hilo lilitolewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Godfrey Mheruka, wakati wa kukabidhi pikipiki 22 zenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 270 zilizotolewa kwa waendesha bodaboda wilayani humo, kupitia chama cha kuweka na kukopa cha umoja wa vijana Karagwe, kilichoanzishwa mwaka 2009 na aliyekuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) mkoa wa Kagera, Yahaya Kateme.

Mheruka alisema mbali na kuvusha kahawa kimagendo, pia baadhi yao wanafaulisha viroba vya pombe na maeneo yanajulikana ikiwamo la Kihanga, na kuwa wote watakamatwa na kuwajibishwa kwa mujibu wa sheria.

"Hata wale mnaovusha kahawa kwa magendo baadhi yenu tunawajua, lakini mfahamu kufanya hivyo mnawaathiri wazee wenu, mnaiba kahawa kwenye miti, mnaweka kwenye magunia na kwenda kuuza kimagendo Uganda, ole wenu ikikamatwa pikipiki yoyote inafanya magendo ya kahawa, mhusika atakwenda rumande, pikipiki na kahawa vinataifishwa na serikali," alisema. N Alisema kuwa serikali haitakuwa tayari kuwavumilia watu wa namna hiyo, na kuwataka vijana waliokopeshwa pikipiki hizo kufanya kazi halali na kwa bidii ili waweze kurejesha kwa wakati na kuwezesha wenzao ambao hawajapata fursa hiyo kukopa.

Kwa upande wake mwanzilishi wa SACCOS hiyo ya vijana Yahya Kateme alisema kuwa kabla ya kuanzisha mradi huo wa "Kijana miliki pikipiki yako" walifanya utafiti na kugundua kuwa vijana walio wengi wanaendesha pikipiki za mabosi na kutakiwa kurejesha shilingi 10,000 kwa siku, na kuwa kupitia mradi huo vijana watamiliki pikipiki zao.

"Malengo makubwa ya Saccos hii ni kuwainua vijana kiuchumi, kwa hiyo tuliona ni bora kijana akakopeshwa pikipiki, na atakapomaliza mkopo inakuwa ya kwake na anaweza kuitumia kufanya shughuli nyingine," alisema Kateme.

Naye Mhasibu Msaidizi wa Saccos hiyo, Johaiven John, alisema tangu kuanzishwa kwake wameshatoa mikopo kwa vijana yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni mbili.



Meneja wa Masuala Endelevu wa TBL, Irene Mutiganzi, akizungumza wakati wa mafunzo ya elimu ya afya na lishe kwa wajawazito na ugonjwa wa selimundo kwa wauguzi kutoka hospitali za Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tembo wawili waliokwama shimo la tope sasa waokolewa

**Na Joseph Mchekadona**

TEMBO wawili waliokwama katika shimo lenye tope kwa siku mbili katika Pori Tengefu la Muhesi wilayani Manyoni Mkoa wa Singida wameopolewa na Kampuni ya Ujenzi ya China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC).

CCECC ilituma wahandisi wake na tingatinga katika eneo la kuhifadhi wanyama pori la Muhesi, kijiji cha Doroto , mkoani Tabora ili kuwaokoa tembo hao.

Mmoja wa wafanyakazi wa Taasisi ya Wanyamapori (TAWA), Peter Marcely, alisema waliwaita wafanyakazi wa kampuni hiyo kuwasaidia tembo hao yapata kilomita 70 kutoka katika hifadhi hiyo.

"Tunawashukuru wafanyakazi wa CCECC kwa kuja kusaidia kuwaokoa tembo waliokwama kwenye shimo hilo, sisi kama serikali tulijitahidi lakini tukashindwa ndipo tulipoomba msaada kutoka kwao, " alisema Marcely .

Naye Meneja wa CCECC eneo la Karangasi, Bai Cunxian, alisema kampuni yake ilisaidia kuokoa tembo hao kama njia moja wapo ya kufanya kazi na serikali ya Tanzania.

"Sisi CCECC tunafanya kazi na Serikali ya Tanzania, tulipopata wito kuja kusaidia uokoaji wa hao tembo, hatukusita kuja hapa, na kwa bahati nzuri tumefanikiwa kuwaokoa tembo wote wawili," alisema na kuongeza:

" Kampuni yetu ipo tayari kufanya kazi na Watanzania wote kwa wakati wowote."

Kampuni ya CCECC imekuwapo nchini tangu mwanzo wa miaka ya 60, moja ya kazi yao kubwa ni ujenzi wa reli ya Tazara, na sasa wanajenga Ubungo Interchange.

## Serikali yapiga jeki shule mbili

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI imetoa Sh. milioni 59.1 kupitia Mradi wa Education Programme for Results (EP4R), ili kuezeka madarasa katika shule za msingi Chimati na Chirorwe zilizopo Musoma Vijijini, mkoani Mara.

Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Michael Hasunga, alisema shule yake imepokea Sh. milioni 12.5 ambazo zitatumika kuezeka maboma matatu ili kupunguza mrundikano wa wanafunzi madarasani na pia kuwaepusha kusomea chini ya miti.

"Shule yetu ina wanafunzi 437, vyumba vya madarasa vilivyopo ni vitatu, mahitaji ni vyumba 10...wapo wanafunzi wanaosemea chini ya miti, lakini hivyo vingine vitatu zikiezekwa kutakuwa na unafuu," alisema Hasunga.

Alisema, kwa sasa chumba cha darasa kinachukuwa wanafunzi kati ya 37 hadi 87, na kwamba hatua ya serikali kutoa kiasi hicho ya pesa itasaidia angalau kupunguza adha kwa wanafunzi.

Naye upande wake mwenyekiti wa kijiji cha Chimati, Masinde Bwire alisema wananchi wamejitolea kuchangia shilingi 5,000 kila kaya ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu.

"Kwa niaba ya wananchi wa Chimati, niwashukuru wadau wote waliofanikisha ujenzi huu ikiwa ni pamoja na Mbunge, Profesa Sospeter Muhongo aliyechangia saruji mifuko 110 na madawati na vitabu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema Mfuko wa Jimbo umechangia mabati 54 kwa ajili ya kufanikisha ujenzi wa vyumba hivyo ili kupunguzia wanafunzi adha ya kusomea chini ya miti.

Kwa upande wake Diwani wa Kata ya Suguti, Denis Ekwabi alisema Shule ya Msingi Chirorwe imepokea Sh. milioni 46.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa mawili, ofisi moja na matundu saba ya vyoo.

"Mwenyekiti wa Kijiji cha Chirorwe, Msai Maingu amesema kuwa wananchi wameishachangia mawe tripu 22, mchanga tripu 28, kokoto tripu nne na wanasomba maji kwa ajili ya ujenzi," alisema Ekwabi.

Diwani huyo alisema Shule ya Chirorwe nayo imefaidika kwa mchango wa mbunge aliyetoa mifuko 60 ya saruji, maboksi 0 ya vitabu zaidi ya 1,000 na madawati 60.

# TIRDO yabuni mtambo maalumu kudhibiti sumukuvu kwenye mazao

SHIRIKA la Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), katika kuhakikisha mazao mbalimbali nchini yanakaushwa kwa kiwango kinachokubalika kitaalamu ili kuepuka magonjwa, limebuni mtambo maalum wa kuondoa sumukuvu.

Akizungumza na Nipashe katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba, Mtafiti wa TIRDO, Ester Lazaro, alisema mtambo huo ambao unatumika sambamba na biogesi utasaidia kukausha mazao hayo hasa mahindi na karanga na kuepukana na unyevunyevu.

Alisema mazao mengi yamekuwa hayakauki vizuri kwa sababu ya hali ya hewa jambo ambalo lina athari kiafya.

"Ili kuondoa tatizo hili tumeona ni vyema tukapanga mikakati na kuunda mfumo ambao ni rafiki unaotumia masalia ya mimea kukaushia mazao," alisema Ester.

Ester alisema kadri siku zinavyokwenda, mtambo huo wa kijani kibichi umejizolea wateja wengi kwani wanaamini utasaidia kuondoa changamoto ya ukaushaji mazao kwa wakati.

Alisema wanaendelea kutengeneza mtambo huo ili uwe mkubwa ambao utakidhi mahitaji ya wananchi wengi hapa nchini.

Pia alisema wamegundua dawa nyingine inayojulikana kama Leather Processing Enzemy yenye uwezo wa kuondoa manyoya kwenye ngozi ya mnyama bila kumwathiri. Alisema dawa hiyo imetengenezwa kwa vitu vya asili na haina madhara isipokuwa inaua pia viluilui vya malaria.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikabidhi kikombe cha ushindi wa jumla katika uunganishaji wa magari na uuzaji wa mitambo, kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya GF Trucks, Ali Jawad Karmali, wakati wa ufunguzi wa Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Abuni mtambo kufua umeme

**Na Elizabeth Zaya**

MKAZI wa Sumbawanga mkoani Rukwa, George Ulaya, amebuni mtambo wa kufua umeme unaotumia upepo wenye kilovoti 50,000, ambao utatumika kuendesha viwanda na matumizi ya nyumbani.

Ulaya akiwa chini ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) aliweza kuelezea jinsi alivyoanza ubunifu huo akiwa Sumbawanga na sasa anasambaza teknolojia hiyo katika mikoa mbalimbali nchini.

Akiwa katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba banda la COSTECH alisema alianza na kutengeneza mashine ya kufua umeme kwa njia ya upepo wa kilovoti 300, lakini baada ya kuwezeshwa na COSTECH anatengeneza pia mashine ya kisasa inayotoa umeme wa kilovoti 50,000.

Alisema umeme wake unatumiwa na idadi kubwa ya watu na kwamba hata umeme wa gridi ya taifa ukikatika mashine yake ina uwezo wa kutunza nguvu ya umeme kwa muda mrefu.

"Nawashukuru COSTECH baada ya mwaka 2010 kunipa tuzo ya ubunifu huu na kunisaidia sasa nimepaa nipo kiteknolojia zaidi kwa maana natumia nyenzo mbalimbali za kisasa na nimekuwa mbunifu mkubwa wa kutengeneza mashine mbalimbali," alisema Ulaya.

Alisema mashine hiyo ina uwezo wa kutumika hata viwandani mbali na matumizi ya majumbani na inaweza kutumiwa na takribani na watu 400 kwa wakati mmoja.

## Wito kuwezesha vijana teknolojia

JAMII imetakiwa kuwawezesha vijana kwa kuwajengea uelewa kuhusu teknolojia mbalimbali ili kupata wataalamu wanaokidhi soko la uchumi wa kati kupitia viwanda.

Akizungumzia na Nipashe, Mratibu wa Mafunzo ya Ujenzi wa Kituo cha Intergrated Mining Technical Training Project (IMTT), Theresia Mosha, alisema, chuo hicho kimekuwa kikitua mafunzo mbalimbali kwa vijana kwa sababu ya mahusiano mazuri waliyojiwekea baina yao, kampuni za madini na chakula. Alisema kwa sababu ya mahusiano hayo, kampuni zaidi ya 12 huwawezesha wafanyakazi wao kwa kuwagharamia mafunzo ili kuwajengea uwezo zaidi.

"Kituo chetu kila mwaka huchaguliwa kuwa kituo cha Mafunzo IMTT Tanzania kwa sababu kimejijengea mazingira bora ya miundombinu ya chuo pamoja na ufundishaji," alisema Theresia.

Alitaja kozi wanazofundishwa kuwa ni pamoja na utengenezaji mfumo wa magari, umeme wa viwandani, ufundi wa magari pamoja na uchongaji vifaa vya magari.

Alisema kwa mwaka huu wamekuja na teknolojia mpya ya umeme wa magari ya dizeli ambayo imekuwa kivutio kwa watu wengi.

Aidha, alisema malengo yao makuu ni kuhakikisha jamii kubwa ya vijana wa Kitanzania wanapata elimu ya ufundi ambayo itachagiza kuibuliwa kwa viwanda vingi hapa nchini na hatimaye kufikia uchumi wa kati.

## Posta yaanzisha duka jipya la biashara kwa mtandao

KATIKA kuendana na soko la ushindani, Shirika la Posta Tanzania, limeanzisha duka jipya la biashara za kimtandao maarufu kama 'Posta Shop Tz'.

Akizungumza katika Viwanja vya Maonesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) yanayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Meneja wa Biashara za Kielektroniki (E-commerce), Amina Salum, alisema ni duka ambalo linauwezo wa kuuza, kununua na kutangaza biashara kwa wateja ambao wamejisajili.

"Mjasiriamali yeyote anaweza kujiunga kupitia website yetu au kuingia kwenye website ya shirika," alisema Salum.

Alisema wameamua kuanzisha mfumo huo kwa sababu biashara za kimtandao kwa sasa ndio zinatumika kwa kiwango kikubwa.

"Vijana wengi sasa hivi wananunua bidhaa online, kwa kuwa shirika linafanya biashara na linaaminika zaidi hivyo tukaona na sisi tuje na duka hili, ambapo mtu yeyote anaweza kujiunga nasi bure na lengo ni kutoa fursa kwa idadi kubwa ya watu kufanya biashara," alisema.

Aliongeza kuwa katika maonyesho ya mwaka huu mwamko umekuwa mkubwa kwa Watanzania kutembelea banda lao na kutaka kujifunza mambo mbalimbali ya shirika hilo.

Alisema kuwa shirika hilo limejipanga kiushindani kama ilivyo kwa kampuni nyingine na kwamba wanafanya kazi na kampuni zote za simu nchini kwa sasa katika kurahisisha kufanyika kwa miamala ya kifedha kwa ajili ya biashara.

HABARI ZOTE NA ELIZBETH ZAYA

**HABARI ARUSHA**

# Alazwa baada ya kung'atwa na mama

**Na Jaliwason Jasson,M**
MANYARA

MTOTO wa miaka minane, jina tunalo anayesoma darasa la tatu katika Halmashauri ya Mji wa Babati ameng'atwa na mama yake (jina linahifadhiwa pia) na kupata majeraha sehemu mbalimbali, kisa ameshindwa kuosha vyombo.

Mtoto huyo ambaye amepigwa kipigo cha kinyama na mama yake, akizungumza na Nipashe jana katika wodi ya watoto Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara alisema alimpiga kwa kuwa hakuosha vyombo kama alivyoagizwa na mama yake.

"Mama yangu alinipiga na nilikuwa nina siku tatu sijala chakula na mara nyingi ananipiga sana na kuning'ata hasa fimbo ikikatika. Walionisaidia kuniokoa ni majirani zetu ambao walinipeleka kwao na kunipa chai baadaye wakainileta hapa hospitalini," alisema mtoto huyo.

Aidha, mtoto huyo alisema mama yake alimchapa kwa kutumia mwiko wa kusongea ugali na ulipokatika, alitafuta kanga na kuanza kumnyonga akiwa anamfunga shingoni akimtishia kuwa atamvunjavunja miguu.

Alisema hali yake inaimarika ni tofauti na alivyofikishwa hospitalini hapo, maana kipindi anafikishwa hospitalini na wasamalia alikuwa na maumivu makali ya mikono, begani, shingoni na maeneo mengine aliyojeruhiwa.

Mtoto huyo alisema, mama huyo sababu nyingine ya kumwadhibu nikumtuhumu kuwa anamdharau kila anapomwambia kufanya kazi yoyote anaiacha na mama yake akirejea anakuta kazi haijafanyika na ndipo anaanza kumcharaza viboko na kuanza kumng'ata.

Alipoulizwa kipindi anapigwa baba yake alikuwa wapi alisema alishafariki na kuhusu kumsamehe mama yake aliyempiga hakujibu.

Dk. Christogono Hangu wa hospitali hiyo, alisema walimpokea mtoto huyo saa 12 jioni, alipofikishwa hospitalini na majirani. Alisema mtoto huyo alikuwa na alama ya kung'atwa na kupigwa na vitu visivyokuwa na ncha kali, hivyo alipewa matibabu ya dawa za kutuliza maumivu na sasa hivi anaendelea vizuri.

Matukio ya ukatili wa namna hiyo kwa watoto, alisema huripotiwa katika hospitali hiyo, lakini hajawahi kuyaona ila kwenye jamii yapo na yakimpata mtu kama hajachanjwa chanjo ya kichaa cha mbwa yanaweza kumwathiri.

Mmoja wa aliyemwokoa mtoto huyo, Isaria Mrema, alisema alipomwona alimsalimia na kumwomba dada mmoja kumkagua na kukuta amepigwa ndipo alipoamua kwenda polisi kuomba fomu ya kumruhusu kwenda kutibiwa. Ofisa Ustawi wa Jamii wa Hospitali ya Mji wa Babati, Mrara Christina Mfune, akizungumzia tukio hilo alisema sharia inaelekeza wanaowakatili watoto kuripotiwa kituo cha polisi.

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi mkoani Manyara Augustino Senga, akizungumza kwa njia ya simu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na mama wa mtoto huyo amekamatwa.

Alisema kwa tukio hilo ni tukio la jinai hivyo atafikishwa mahakamani iwapo atapatikana na hatia anaweza kufungwa kifungo au kulipa faini, kulingana na maelekezo ya sheria.



Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima (wa pili kushoto), akikagua mgodi wa madini ya Green, unaomilikiwa na Charles Shoo (kushoto), ulioko machimbo ya Lemshuku juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Taifa kuadhimisha miaka 60 ya fuvu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WIZARA ya Maliasili na Utalii kupitia Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), itaadhimisha miaka 60 ya ugunduzi wa fuvu la binadamu wa kale anayejulikana kama Zinjanthropus Boisei. maadhimisho hayo yatafanyika Julai 17 mwaka huu, ili kuendeleza utafiti, uhifadhi, utalii pamoja na matumizi bora na sahihi ya urithi wa kitamaduni.

Akizungumza jana jijini Arusha na waandishi wa habari, Kaimu Kamishna wa Uhifadhi Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, (NCAA), Hillary Mushi, alisema fuvu hilo lenye umri wa miaka milioni 1.75, iliyopita liligunduliwa Julai 17 mwaka 1959 na wataalamu wa akiolojia Dk. Leakey na mkewe Dk. Mary Leakey.

Alisema lengo la maadhimisho hayo ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa urithi wa asili na utamaduni walionao, kuendeleza na kufanya utafiti zaidi, uhifadhi endelevu, matumizi bora na sahihi ya urithi wa Mtanzania kuboresha utalii.

Kamishna Mushi alisema katika maadhimisho hayo NCCA Makumbusho ya Taifa, Idara za Mambo ya Kale na Akiolojia na Urithi wa Utamaduni, Chuo Kikuu cha Dares Salaam ndiyo waandaaji.

Aidha, alisema kutakuwa na warsha mbalimbali zitakazofanyika Julai 16 mwaka huu ambazo watafiti wanaofanya kazi kwenye mabonde ya Olduvai na Laetoli watatoa mada.

Aidha, ngoma za utamaduni za jamii ya hifadhi hiyo zitatoa burudani pia.

Alisema Julai 17 mwaka huu watu watapata fursa ya kutembelea bonde la Olduvai akiwapo mgeni rasmi na kuona fuvu la Zinjanthropus lililogunduliwa na kuona kazi zinazoendelea za watafiti na kuzuru Makumbusho ya Dk. Mary Leakey.

Mhifadhi wa Makumbusho ya Taifa Dk.Agnes Gidna, alisema , ugunduzi wa fuvu hilo ulisaidia kubadilisha uelewa wa wanasayansi kuhusu mchango wa Afrika katika historia na chimbuko la binadamu duniani.

Alisema masalia ya Zinjanthropus boisei pamoja na masalia mengine ya binadamu wa kale, zana zao za mawe na masalia ya mifupa ya wanyama waliyokutwa katika bonde la Olduvai miaka milioni 2.0 iliyopita vinaithibitisha dunia kuwa Tanzania ndio nchi pekee yenye taarifa bora na sahihi kuhusu chimbuko la binadamu.

Si chimbuko pekee hata na utamaduni wake, chakula na namna ya kupata chakula hicho katika kipindi hicho.

"Na kwamba bonde la Olduvai ndilo chimbuko la binadamu wote duniani (the Cradle of humankind)," alisema Dk. Gdina.

Aliongeza kuwa pia watu watajionea nyumba, meza, vyombo, kamera, vitanda, gari na vifaa mbalimbali alivyotumia Dk. Leakey katika utafiti wake ambavyo vitakuwa sehemu ya makumbusho hiyo maana ni tofauti na vifaa vya sasa wanavyotumia watafiti wa kisasa.

## Wadau waomba wataalamu wa alama

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WATU wenye ulemavu wa kutosikia na watoa huduma, wameiomba serikali kupeleka wakalimani katika maeneo muhimu ya huduma, ili waweze kurahisisha mawasiliano kwa wahitaji hao.

Akizungumza jana mmoja wa wanachama wa Chama cha Viziwi Tanzania Tawi la Arusha (Chavita), Jenifer Mbagga, alisema kwenye warsha ya mafunzo ya kukuza uelewa kuhusu uziwi na mchakato wa kutumia lugha ya alama.

Alitaka vyombo vya usalama kuwa na wataalamu hao kwani wanateseka kwa kukosa mawasiliano wanapokwenda hospitali, mahakamani, magereza na polisi.

Alisema hilo limekuwa tatizo kubwa kwa sababu maeneo hayo ya kutolea huduma hayana wakalimani, hivyo hujikuta wanapopata matatizo ya kukosa mawasiliano na kuishia kukosa huduma na stahiki.

"Mfano Juni mwaka huu nimeugua ziwa limepata uvimbe, nikaenda Hospitali ya Kaloleni, lakini kwa kukosa mawasiliano daktari aliishia kuniambia niende Mount Meru."

Anasema hata alipokwenda huko nako hakupata huduma alizostahili, mbali na kupewa dawa , hadi sasa maumivu yanaongezeka.

Alisema endapo angekuwapo mkalimani angepata huduma stahili, hivyo vema serikali ikawawekea watu hao wa kutafsiri lugha za alama, ili waweze kupata haki zao zinavyostahili kama watu wengine wanavyohudumiwa.

Kwa upande wake mwezeshaji wa mafunzo hayo, Jonathan Livingstone, alisema lengo la semina ni kuongeza ufahamu na uelewa kwa watoa huduma hususani wanaotoka katika vyombo hivyo, ili wawahudumie wahitaji hao kikamilifu. "Pia nawaelimisha kuhusiana na mkataba wa kimataifa wa Umoja wa Mataifa wa Watu Wenye Ulemavu na Sheria namba 9 ya mwaka 2010 ya watu wenye ulemavu, lengo hasa ni kuwezesha uboreshaji wa utoaji na upatikanaji wa huduma na haki kwa viziwi, sababu wengi hawaujui mkataba huu, sheria zao, sera na kanuni iliyotolewa mwaka 2000 na sasa inatumika," alisema. Kwa upande wake Msaidizi wa Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Monduli na Polisi Jamii, Gervas Mbowe, aliomba serikali kuweka wakalimani ngazi za mafunzo kama vyuo vya polisi, magereza ili waweze kufundisha watoa huduma lugha za alama.

# Tembo walioingia makazi ya watu Same waanza kurejeshwa hifadhini

**Na Paul William,** SAME

MAOFISA wa Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi iliyopo katika mikoa ya Kilimanjaro na Tanga, wameanza kazi ya kuwarudisha hifadhini tembo wawili wanaodaiwa kuvamia makazi ya watu na kuua mtu mmoja.

Hadi kufikia jana jioni, tembo hao walikuwa wamevamia ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Same na Bar ya Nice Park na kuzua taharuki kubwa kwa wananchi wa Same mjini.

Mkuu wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, amethibitisha kuwa tembo hao wamesababisha kifo cha Hans Hedes (47), mkulima na mkazi wa Kijiji cha Muheza.

Alipotafutwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro (ACP), Hamisi Issah, kuzungumzia tukio hilo alisema tukio la mauaji hayo limetokea juzi katika Kata ya Maore, Jimbo la Same Mashariki.

Kwa mujibu wa Kamanda Issah, mkazi huyo alifariki dunia baada ya kujeruhiwa kichwani na tembo ambao wamezagaa katika baadhi ya maeneo ya wilaya hiyo.

Kamanda Issah, alisema Julai mosi mwaka huu, majira ya asubuhi marehemu Hans akiwa shambani kwake akilinda mazao yake, ndipo walipotokea tembo wawili na kumshambulia.

"Marehemu kabla hajachukua tahadhari ya kukabiliana na tembo, mmoja wa tembo hao alimnyanyua na kumrusha juu na mkonga wake na kisha kuangukia kichwa na kusababisha majeraha yaliyosababisha kifo chake papo hapo," alisema Kamanda Issah.

Alisema mwili wa marehemu huyo umehifadhiwa katika Hospitali ya Wilaya ya Same, ukisubiri taratibu nyingine za mazishi.

Kamanda huyo alisema kuwa maofisa wa uhifadhi wa wanyamapori kutoka Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi wanaendelea kutoa elimu kwa wananchi wa Wilaya ya Same kujua mbinu za kujihami wanapomuona tembo, kwa kuwa hawezi kufukuzwa kama ng'ombe.

"Tembo ni mnyama wa porini anahisia na namna ya kujilinda mwenyewe, sasa anapoona mtu yeyote anataka kumletea hatari, hutumia nguvu."



Mkurugenzi wa Tehama wa Benki ya TPB, Jema Msuya, akikabidhi mifuko 100 ya saruji kwa Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Sinyamule, kwa lengo la kujenga maabara ya kisasa ya kompyuta kwa vijana wa Same. Katika hafla iliyofanyika wilayani humo Mkoa wa Kilimanjaro juzi. **PICHA: MARY MOSHA**

# Wakazi wasikitishwa mkwamo kiuchumi kuathiri umwagiliaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WAKULIMA wa vijiji vya Mkalama, Rundugai na Kawaya katika Wilaya ya Hai, wameeleza kusikitishwa na mkwamo wa shughuli za kiuchumi kwenye eneo hilo, namna unavyoathiri uzalishaji wa chakula licha ya kuwapo kwa fursa za kilimo cha umwagiliaji.

Baadhi ya wakulima wa vijiji hivyo akiwamo Ofisa Mtendaji mstaafu wa Kijiji cha Kawaya, Ridhiwan Kisumo, wameeleza kuwa sababu zinazosababisha mkwamo huo ni pamoja na kukosekana kwa miundo mbinu ya umwagiliaji na serikali kutoona kipaumbele hicho.

Kutokana na hali hiyo, wakulima wa vijiji hivyo wameitaka Wizara ya Kilimo na Halmashauri ya Wilaya ya Hai kuwasaidia kujengewa miundombinu ya maji ya umwagiliaji kwa kuuhuisha mfereji wa asili unaosambaza maji katika vijiji hivyo.

Mkulima wa Kijiji cha Mkalama, Hilda Massawe, alisema ili waweze kuimarisha kilimo cha umwagiliaji na kufanikiwa kuongeza uzalishaji wa chakula cha kutosha na ziada kwa ajili ya biashara, kuna kila sababu ya serikali kuelekeza nguvu kwa kupeleka mradi wa ujenzi wa mfereji huo.

Mfereji huo wa asili una urefu wa kilometa 15 kuanzia kwenye chanzo cha maji hadi katika Kijiji cha Mkalama.

Alisema kutokana na maji mengi ya mfereji huo kupotea bure, wakulima sasa wanalazimika kulima kwa kupokezana na hivyo kupoteza muda mwingi wa uzalishaji na kusababisha vijana wengi kukosa kazi, licha ya kujiingiza katika kilimo.

Pamoja na mambo mengine, mfereji huo unawanufaisha wakulima zaidi ya 856.

Wakulima katika vijiji hivyo wanaweza kutumia mfereji huo kwa kuimarisha kilimo cha mpunga, maharage, mahindi na mboga mboga ambazo zimekuwa zikilisha Wilaya ya Hai na sehemu kubwa ya Moshi Mjini.

Akizungumzia madai hayo ya wakulima, mwenyekiti wa chama cha wakulima wanaotumia mfereji huo, Thabit Mushi, alisema mfereji huo, tangu nchi imepata uhuru wake mfereji huo haujawahi kujengewa na sasa unakabiliwa na uchakavu mkubwa hali inayosababisha maji mengi kupotea bure.

Alisema mfereji huo unapitisha kiwango cha maji lita 5000 kwa sekunde na kwamba Wizara ya Kilimo tayari wameanza kuandaa michoro na bajeti ya kukarabati mfereji huo ili kuweza kuongeza uzalishaji na kilimo katika vijiji hivyo.

## Mhitimu udaktari aomba msaada

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

MHITIMU wa shahada ya kwanza udaktari wa binadamu, Godliving William (25), mkazi wa Kata ya Mji Mpya katika Manispaa ya Moshi ambaye anakabiliwa na tatizo la kuvuja damu kichwani, yuko katika wakati mgumu kutokana na kushindwa kupata zaidi ya Sh. milioni 40 kwa ajili ya kutetea uhai wake.

Jana, familia ya daktari huyo kupitia kwa bibi yake, Hilda Assey ilithibitisha kuwa ili Godliving apate matibabu na kurejea katika hali ya kawaida, anahitaji kiasi hicho cha fedha kupelekwa nchini India.Aidha, mhitimu huyo, anatakiwa kufanyiwa upasuaji katika kichwa chake baada ya kuonekana katika ubongo wake kuna mshipa umepasuka na kuvuja damu, hali iliyomsababishia kushindwa kuona ghafla, kupata ugonjwa wa kiharusi, degedege pamoja na kuuondoa mshipa mwingine ulioota ndani ya ubongo.~ Akitoa ufafanuzi kuhusu hali aliyonayo mjukuu wake, Assey alisema amepambana na tatizo lililompata Godliving kwa muda mrefu, lakini ameshindwa kuendelea kutokana na gharama kubwa za matibabu yake. "Gharama zinazohitajika nchini India ni kubwa na kama familia hatuna uwezo wa kuwa nazo, naiomba serikali, watu wenye uwezo kiuchumi pamoja na wasamaria wema, watusaidie kijana huyu aweze kutibiwa na kurudi kutoa mchango wake wa huduma kwa jamii," alisema Assey.

Aidha, akielezea namna jamii inavyowajibika kutafuta msaada kumsaidia daktari huyo, Diwani wa Kata ya Mji Mpya, Abuu Shayo, alisema tayari ameanza kuhamasisha wananchi wake na kila mmoja kwa uwezo wake kuangalia namna ya kuchangia gharama za matibabu ya kijana huyo.

Godliving ambaye ameugua kwa muda mrefu na kupatiwa matibabu katika hospitali mbalimbali za rufani nchini ikiwamo Hospitali ya Rufani ya KCMC na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), bado hali yake si nzuri.



Ukurasa 18

Wakulima wa tumbaku wako hoi, wazidi kuwa maskini



Ukurasa 19

Wasomi, Profesa Lipumba wanapotaka BoT ikopeshe zaidi



## Watanzania na mchango wa kipekee kuondoa joto duniani

Ukurasa 15


# BUFE

Ijumaa Julai 5, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# Alizeti rasmi zao kila kaya, wakulima kuunganishwa na masoko

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA Manyara umejikita kwenye uzalishaji wa kisasa wa alizeti unaofanywa kupitia mradi wa 'Alizeti Maendeleo Endelevu; unaolenga kulikuza zao hilo la biashara kwa kutumia mbegu na utaalamu wa kisasa.

Mbegu za kisasa za H Hysun 33 zenye ukinzani na magonjwa na mabadiliko ya tabianchi, ndizo zinazotumika na kwa mujibu wa watalaamu zinatoa maguni 16 kwa heka wakati mbegu za asili mkulima huvuna magunia nane.,

Mradi huo wa alizeti maendeleo endelevu unafadhiliwa na asasi ya Agricultural Markets Development Trust (AMDT), kwa mujibu wa meneja mradi huo ulio chini ya asasi ya Farm Africa, Tumain Elibariki.

Elibariki anasema kuwa uzalishaji wa alizeti kwa kilimo cha kisasa, unalenga kuwahamasisha wakulima kulima zao hilo kibiashara na kuunganishwa moja kwa moja na soko moja.

Anasema katika utekelezaji wa mradi huo, hawafanyi kazi ya kufundisha wakulima, wanabaki kiungo kati ya wakulima na wadau mbalimbali, wakiwamo wataalamu wa kilimo na watoa huduma kama vile asasi za mbegu, mbolea, bima za kilimo, wasindikaji wa mafuta ya alizeti, taasisi za fedha na wakulima wenyewe ambao wao ndio walengwa wakuu.

**INAENDELEA UK.16**

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

## G20 inavyokumbusha kuwa na tahadhari nyakati hatarishi

Ukurasa 20

BIASHARA

# TPA inavyoisuka Kigoma kuinua uchumi M/ Makuu



Wafanyakazi wa TPA wakihudumia shehena katika bandari ya Kigoma. **PICHA: MARY GEOFREY**

**Na Mary Geofrey,** KIGOMA

***WIKI iliyopita tulikuwa na makala inayoelezea utendaji kazi wa bandari za Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma ambayo ni kitovu cha biashara na uchumi wa mkoa huo tuendelee...***

Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) katika mkoa wa Kigoma imepiga hatua za ukuzaji wa uchumi pamoja na kuwekeza katika miradi mbalimbali ya maendeleo ambayo inatekelezwa kwa lengo la kuongeza ufanisi wa sekta hiyo muhimu nchini.

Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, ambayo ni sehemu ya Bandari Kuu ya Kigoma, Ajuaye Msese, anabainisha miradi inayoendelea na kutekelezwa katika mwambao wa ziwa hilo kuwa ni mipango mikakati ya muda mrefu na muda mfupi ya TPA wakati akizungumza na waandishi wa habari, waliozuru mkoa huo kwa lengo la kujionea mafanikio ya TPA.

Anawaeleza wanahabari hao waliopata fursa ya kuzuru katika miradi hiyo kuwa, TPA katika mipango yake ya muda mrefu imepanga kufanya maboresho ya gati la mizigo na la abiria katika bandari ya Kigoma. Upembuzi yakinifu umefanyika na kukamilika katika gati la mizigo.

Anasema Shirika la Misaada la Japan (Jica), litaboresha gati la abiria na ghala la shehena ambapo ujenzi wake unatarajiwa kuanza mwezi huu.

> **Tunalenga nchi za Burundi na Kongo (DRC) kwa lengo la kuwezesha mizigo kuchukuliwa Kigoma badala ya safari kuanzia Dar es Salaam.**



Meneja wa Bandari za Ziwa Tanganyika, Ajuaye Msese.

Kuhusu bandari ya Katosho, Msese anasema TPA imechukua eneo lenye ukubwa wa hekta 68 kwa ajili ya ujenzi wa bandari kavu, itakayotumika kupunguza mlundikano wa shehena bandarini katika jitihada za kuimarisha miundombinu ya reli na barabara, kupunguza mlundikano bandarini Dar es Salaam na kusogeza huduma karibu na nchi majirani wanaowahudumia.

"Tunalenga nchi za Burundi na Kongo (DRC) kwa lengo la kuwezesha mizigo kuchukuliwa Kigoma badala ya safari kuanzia Dar es Salaam," Msese anaeleza.

Anaongeza kuwa, ujenzi wa bandari hiyo unaenda sambamba na uendelezaji wa ukanda wa biashara wa Kigoma Special Economic Zone.

Msimamizi huyo wa bandari ya Kigoma anasema, pia wana mpango wa kujenga ukuta na walishafanya tathimini mwezi Aprili mwaka jana.

Anasema kwa sasa TPA imeanza na ujenzi wa ukuta na mkandarasi amepatikana na utajengwa kwa miezi tisa.

"Mkandarasi ameanza ujenzi huo kuanzia Machi 28, mwaka



huu na mradi na amefikia asilimia 13 mpaka sasa," anasema Msese.

Kadhalika anasema wana mradi wa ujenzi wa gati la Kagunga unaohusisha ujenzi wa gati lenyewe, jengo la kupumzikia abiria, ghala la kuhifadhi shehena , vyoo, ofisi na uzio.

Anasema mradi huo umetekelezwa kwa asilimia 100 na gharama yake ni zaidi ya Sh. bilioni 3.356.

Msese anasema mradi mwingine mkubwa ni ujenzi wa barabara ya kuunganisha bandari na soko la kimataifa ambao ujenzi wake unaendelea.

Anasema gharama za kazi hiyo ni Sh. milioni 553. 791, mradi ambao utachukua miezi sita hadi kukamilika kwake.

"Mkandarasi ameanza kazi ya ujenzi Mei Mosi mwaka huu na hadi sasa umetekelezwa kwa asilimia tano," anasema.

Kiongozi huyo anasema pia wana mradi wa ujenzi wa soko la kimataifa unaotarajiwa kugharamia Sh. milioni 190.

Anasema muda wa mradi huo ni miezi sita na mkandarasi alianza kazi Januari 31 mwaka huu na hadi sasa mradi huo umetekelezwa kwa asilimia 25. Msese anasema mradi mwingine ni ujenzi wa gati la Sibwesa (Kakya) ambao pia unahusisha kujenga gati, ofisi, jengo la kupumzikia abiria, ghala la shehena

Anataja gharama ya mradi huo kuwa ni Sh. bilioni 3.452 na hadi sasa utekelezaji wake umefika asilimia 96 na unatarajia kukamilika mwezi huu.

"Kama ilivyo katika mradi wa ujenzi wa gati la Kagunga na mradi huu pia unahusisha ujenzi wa gati, ofisi, jengo la kupumzikia abiria, ghala mizigo na uzio kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa TPA katika bandari hii muhimu," anasema Msese.

Mradi mwingine wa TPA katika mwambao wa Ziwa Tanganyika ni ujenzi wa gati la Lagosa unaohusisha usanifu na ujenzi wa gati.

Msese anasema ujenzi huo unafanywa na kampuni mbili unagharimu Sh. bilioni 12. 459 na kazi ilianza Mei 17 mwaka huu na umeshafikia kiwango cha asilimia 25.

Kadhalika anasema kuna mradi wa ujenzi gati katika bandari ndogo za Kibirizi, Ujiji na ofisi ya mkuu wa bandari na gati la kibirizi, kwa gharama ya Sh. bilioni 32.525 na kazi ilianza Februari 28 mwaka huu ambapo ujenzi umefika asilimia 15.

Msese anasema pia wanatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa gati katika bandari ya Kabwe, barabara na maegesho ya magari katika bandari ya Kipili kazi inayogharamiwa na TPA.

Anasema huo unahusisha usanifu, ujenzi wa gati, jengo la kupumzikia abiria, jengo la mgahawa, ofisi, ghala la kuhifadhia mizigo, nyumba za wafanyakazi na uzio.

Anataja gharama ya mradi huo ni Sh. bilioni 7.498 na mradi huo ni wa miaka miwili ambapo kazi ya ujenzi ilianza Aprili Mosi mwaka hana na umefika asilimia 40.

Msese anasema mradi mwingine ni wa ujenzi wa bandari ya Kasanga uliotiwa saini Aprili 15 mwaka huu.

"Mradi huu unahusisha upanuzi wa gati kutoka mita 20 za sasa na kufikia urefu wa mita 120 ambalo litakuwa na uwezo wa kuhudumia meli mbili kwa wakati mmoja," anaeleza Msese.

Anasema gharama za mradi huo Sh. bilioni 4.764 na mkandarasi alikabidhiwa eneo la mradi Aprili 28 mwaka huu.

Msese anasema pia wana mradi wa ujenzi wa bandari ya Karema ambao umehusisha ujenzi wa gati, majengo, njia za reli na 'wind breakers' ndani ya bandari kwa gharama ya Sh. bilioni 63.

**MIKAKATI**

Msese anasema mbali na utekelezaji wa miradi hiyo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika wana changamoto ambazo wameziwekea mikakati ya kuzitatua ili kuboresha usafiri katika bandari zote.

Anasema kuna changamoto ya kupungua kwa shehena inayoenda nchi jirani za Kidemokrasi ya Kongo (DRC) na Burundi.

Anaeleza mkakati walioweka wa kukabiliana na tatizo hilo ni kutafuta masoko mapya na kuvutia ya lipo.

Pia anasema wanakabiliana na changamoto ya ufanisi mdogo wa Kampuni ya Reli (TRC) na kwamba wapo katika mazungumzo ya pamoja kati ya Bandari ya Kigoma na TRC.

"Lengo la kuwapo kwa mazungumzo haya ya pamoja ni kuweza kuboresha miundombinu ya reli kwa nia ya kuboresha huduma ya usafirishaji," anasema Msese.

Anaeleza pia uwapo wa bandari bubu ambao wameweka mikakati ya kuzichambua ili zirasimishwe na kufunga zile ambazo hazipo kwa mujibu wa sheria.

"Tukifunga hizi bubu zile zilizopo zifanye kazi kulingana na kanuni na taratibu za kiesheria na hivyo kuimarisha ulinzi na usalama kwenye mipaka ya nchi na kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato.

**YATENGA BILIONI 500**

Kwa upande wake Mkurugenzi wa TPA, Deusdedit Kakoko, anasema kwa mwaka mamlaka hiyo inatenga Sh. bilioni 400 hadi 500 kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ya maendeleo.

Anasema wanatumia fedha za TPA kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo ikiwamo ya ujenzi wa gati za kisasa, upanuzi wa bandari zote nchini, ujenzi wa ofisi na maghala ya kuhifadhia mizigo ili kufungua milango ya kibiashara na nchi za jirani.

Anasema miradi hiyo inatumia zaidi ya Sh. bilioni 500 ya fedha za ndani na hufika hadi Sh. bilioni 600 kama wakipata na fedha za nje. Kakoko anasema kati ya fedha hizo ambazo zinatumika kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati ya TPA asilimia 30 ya fedha hizo wanalipa mrahaba serikalini.

"Kukamilika kwa miradi yote ya kimkakati ya TPA kutasaidia kwa kiasi kikubwa kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za bandari mara dufu," anasema Kakoko.

# Watanzania na mchango wa kipekee kuondoa joto duniani



Ukataji miti ovyo kama huu utakwamisha malengo ya kimataifa ya kupunguza joto duniani. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

NI wazi kuwa usalama wa dunia, unaowezesha uzalishaji mali na ukuzaji uchumi unategemea afya ya mazingira.

Wiki iliyopita Mkutano wa Kimataifa wa Mazingira umemalizika karibuni huko Bonn nchini Ujerumani na kuibua masuala mengi yanayolielekeza kila taifa kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Ripoti ya tathmini ya mabadiliko ya tabianchi iliyotolewa na jopo la kiserikali la kimataifa linalotathimini hali hiyo (IPCC), inasema kuwa kufikia mwaka 2030 joto la dunia linaweza kuongezeka na hadi nyuzi joto 1.5 jambo ambalo ni hatari zaidi kwa afya ya baharí na viumbe wengine na kuhatarisha maendeleo na uchumi wa dunia.

Hali hiyo kama haitadhibitiwa ikiachwa kuendelea kama ilivyo itakapofika mwaka 2052 nyuzi joto duniani zitapanda hadi mbili (2) kutoka 1.5 na kuhatarisha maisha ya viumbe baharí ikiwa ni pamoja na visima kama Zanzibar, Mafia na Pemba kutoweka.

Ongezeko la joto duniani linaathiri nchi kavu na bahari, hii inamaanisha kuwa kuna kupanda zaidi kwa kina cha bahari kunakotokana na kuyeyuka kwa mabonge ya theluji yanayojaza kina cha bahari. Hivyo bila kuhakikisha matumizi na ulinzi endelevu wa bahari ni wazi eneo hilo litakuwa limeathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabianchi.

Kwa mujibu wa mtandao wa global watch, tafiti zinaonyesha kuwa kina cha bahari kinajaa kwa kasi kutokana na barafu iliyoko kwenye bahari ya Arctic kuyeyuka.

Mtandao unaeleza kuwa theluji hiyo yenye ukubwa sawa na taifa la Marekani, kuanzia mwaka 1978 hadi 1996, imesinyaa na kuyeyuka na kiasi cha kilometa za mraba 34,300 zinayeyuka kila mwaka.

Aidha, barafu ya Greenland, ambayo ni kubwa kuliko zote duniani nayo imeendelea kuyeyuka na athari zinaishia kwenye kujaza kina cha bahari ikiwamo ya Hindi.

Pamoja na hofu hiyo, si wakati wa kuhofishana zaidi, bali kutafuta njia na ufumbuzi. Mbinu mojawapo kubwa ya kupunguza ongezeko la joto duniani ni kuotesha miti na kutunza misitu ambayo kama mimea inatoa hewa ya oksjeni na kutumia karbon au hewa ukaa, iliyo chanzo cha joto duniani.

Wakati mkutano huo ukimalizika huko Bonn, jambo la msingi kwa Tanzania sasa ni kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa elimu ya kutosha kuhusu utunzaji wa mazingira na kulinda miti ili kuzuia athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Kwani hali ilivyo ni kwamba ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu utunzaji wa mazingira miongoni mwa wanavijiji wanaoishi jirani na misitu ya asili, unatajwa kuwa moja ya vyanzo vya uharibifu wa misitu katika maeneo ya mikoa mingi.

Katika mkutano wa Bonn kinachosisitizwa ni kupunguza ongezeko la joto ambalo sasa kama wataalamu wanavyosema limefikia nyuzijoto 1.5. Lakini wananchi wengi hawajatambua kuwa misitu ni rasilimali ambayo wakitumia kwa namna endelevu inawaondolea umaskini wa kipato na pia inaokoa dunia kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Uharibifu wa mazingira unaotishia uhai wa misitu unahusisha kuvuna mbao, kuchoma mkaa na kukata magogo na kuni.

Misitu mingi iko vijijini. Huko kuna Kamati za Misitu za Kijiji, zinazoundwa na viongozi mbalimbali wakiwamo wa wilaya, ni wakati wa kuzitathimini na kujiuliza zinawashirikisha kikamilifu wana vijiji kutunza mazingira?

Kama sivyo juhudi zianze sasa ili wadhibiti kila aina ya uharibifu na unyong'onyezaji wa misitu ambayo ni muhimu zama hizi katika juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Misitu ya Tanzania inaweza kumalizika kwa sababu mamlaka za kusimamia misitu zinashindwa kutoa elimu kwa wanavijiji ambao bado hawajaelimishwa ipasavyo kuhusu faida za utunzaji wa misitu.

Ni vyema serikali kuwekeza kwenye kuwapa elimu wana kamati za misitu kuhusu umuhimu wa uhifadhi wa mazingira ili wawafahamishe wanakijiji umuhimu wa rasilimali hiyo.

Kamati za maliasili za vijiji zisaidiwe na wadau kama Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), Idara ya Maliasili na asasi za kiraia za kutunza mazingira ili ziwe na elimu ya kutosha ili ziwafahamishe wananchi kuhusu umuhimu wa misitu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na kupunguza joto duniani ili kulinda usalama wa dunia na viumbe wa bahari.

Juhudi zifanywe kuhamasisha wananchi kuacha uharibifu wa kuvuna misitu hiyo ovyo, wafuate utaratibu na kufanyakazi za kuvuna miti, mbao, mkaa , kuni na hata kufungua mashamba kwa taratibu za kisheria ili zikiwamo kulipia gharama zinazowezesha kupata fedha kwa njia ya kulipia tozo, ushuru na kodi yote hayo yataleta fedha zinazochangia kulinda rasilimali hiyo pamoja na maendeleo ya vijiji.

Kutowashirikisha wananchi walioko karibu na misitu ni hasara kwani hawataweza kunufaika na rasilimali hizo hivyo kuchangia kuumiza taifa ambalo nalo linahitaji kujilinda na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Wataalum wa Idara ya Maliasili watoe elimu kuanzia ngazi za kitongoji, vijiji na kushirikiana na kamati za mazingira na uhifadhi ili makundi hayo yatambue wajibu wao katika kulinda misitu kwani ndiyo pekee ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi yanayotokana na ongezeko la joto duniani.

BIASHARA

# Alizeti rasmi zao kila kaya Manyara, wakulima kuunganishwa na masoko

**INATOKA UK.13**

Elibariki anasema, ili kuhakikisha mradi unafanikiwa, wamelenga kuwafikia wakulima 10,000 mkoa mzima kwa kutumia mbinu ya wakulima kwenye vikundi vya shamba darasa, wakiamini itawaongezea uzalishaji wa alizeti na kukuza kipato cha wakulima, pia ajira ya kudumu baada ya kuwa na uhakika wa soko.

Akizungumza Siku ya Mkulima Shambani iliyofanyika Kata ya Mulbadaw wilayani Hanan'g anasema, mradi umeazisha vikundi vya wakulima 489 mkoa mzima na vinanolewa wataalamu kilimo, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji alizeti, huku wakisisitizwa kupanda mbegu ya Hysun 33 ambayo inayovumilia ukame.

Mtaalamu huyo anasema hata wakulima wasiojiunga katika vikundi watafuata ushauri wa wataalamu na kupanda mbegu ya kisasa ya alizeti.

Elibariki, anayesimamia mradi huo, anasema kadri wakulima watakavyozalisha ndivyo wanavyosaidia viwanda vya kukamua mafuta ya alizeti kupata malighafi za uhakika.

Meneja huyo anasema, iwapo wakulima watathubutu na kuamua kulima alizeti hasa ile mbegu ya Hysun 33 watasaidia serikali kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta ya kula nje ya nchi kwa asilimia 60, huku Tanzania ikizalisha alizeti yenye kuwapatia mafuta ya kula kwa asilimia 40.

Anafafanua kuwa, alizeti ya asili inaweza kutoa lita 15 hadi 18 za mafuta ndiyo maana wataalamu wanasisitiza kupanda mbegu ya kisasa ya Hysun 33.

Anatoa angalizo, iwapo mkulima atafuata kanuni bora za kilimo mavuno yake kwa mbegu ya Hysun 33 anaweza kupata magunia 12 mpaka 14 kwa ekari moja na zile mbegu za asili anaweza kuambulia magunia matano hadi nane kwa eka moja.

**USINDIKAJI**

Meneja Elibariki anasema lengo jingine la mradi ni kuwasaidia wakulima kuondokana na changamoto ya usindikaji, kwani walioko huwapunja kupitia kwa madalali jambo ambalo Elibariki anasema asasi yake imeamua kuwajengea uwezo wakulima na wasindikaji.

Kwa mujibu wa shirika la Farm Africa iwapo wakulima wataitikia wito wa kulima zao la alizeti watajiongezea kipato na watapata ajira kutokana na uzalishaji mkubwa wa alizeti ambao una ukinzani na mabadiriko ya tabianchi ambayo yamekuwa ni kichomi kwa wakulima wengi licha ya kutokukata tamaa na kuwakumbusha kuwa kilimo ni mkombozi pekee anayeweza kuinua maisha yao.



Katibu Mtendaji wa Chama Cha Wasindikaji wa Mafuta ya alizeti (MASUPA) Julian Kambayta akionyeshwa na mtoto na wakulima Alizeti ilivyokubali katika Kijiji Cha Enguselo wilayani Kiteto kwenye shamba darasa.

> **Bado kiasi cha alizeti kinachozalishwa ni kidogo, hakiwawezeshi wasindikaji kufanya kazi kwenye viwanda msimu mzima, wanaishia kufanya kazi kazi Julai hadi Desemba.**



Wakulima wa alizeti wilayani Kiteto wakipewa elimu na wataalam wa kilimo wa Farm Africa juu ya zao Hilo kwenye shamba la mfano katika Kijiji Cha Enguselo.

Mtaalamu wa kilimo Makilina Simon, kutoka taasisi ya AMDT, anasema alipohudhuria Siku ya Mkulima Shambani katika Kata ya Mulbadaw, Hanang' wanakoletwa waataalamu wa kilimo na wadau wengine, kuwa wananchi wanafurahishwa kutangaziwa uhakika wa masoko.

**MAONI YA WATAALAMU**

Ofisa kilimo wa Kata ya Mulbadaw, Hanan'g, Flavia Ninga, anasema kilimo kilionekana kama adhabu, ila kwa sasa ni fursa na anasema wana vikundi 10 katika kata hiyo ambavyo ni vya vijana na wanawake.

"Alizeti hii inapandwa kwa kuchelewa ila inastawi vizuri na hii mbegu ya Hysun 33 inafanya vizuri hapa na nje ya kata yetu katika maeneo ya Hanan'g na vikundi hivi tunavipatia elimu ya ushirika na tunatoa kwa wakulima wetu," anasema Ninga

Ofisa huyo anawahakikishia wakulima kuwa alizeti yao itanunuliwa kwa bei watakayoipanga wenyewe na siyo wakulima kupangiwa bei na wanunuzi, anawaambia alizeti siyo zao la kuoza bali kadri linavyozidi kuhifadhiwa ndipo linaongeza ubora zaidi.

Anasema katika zao hili halina cha kutupa, kwa kuwa hata makapi yake wanayatumia kutengeneza mkaa, hivyo anawataka kulima kujitokeza kwa wingi kadri wawezavyo ili wajikwamue kiuchumi.

Ofisa Kilimo wa Kata ya Qash, wilaya ya Babati Adelta Macha, anasema Siku ya Mkulima Shambani, iliyofanyika katika wilaya yake, ni mfumo wa wawezeshaji wa kata hiyo, Farm Africa, na kwamba haiwapi wakulima fedha, bali inawapa elimu ya kuitumia.

"Wakulima zaidi ya 170 wamepewa mbegu za kisasa kwa ajili ya kupanda ila wengi wao wameogopa kupanda mbegu hizo kutokana na hali mbaya ya hewa iliyojitokeza ya jua kuwaka kwa kipindi kirefu ila msimu ujao tunatarajia wataipanda hii mbegu," anasema Macha

Mhandisi Kilimo wa Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Norbet Kyomushula, aliyekuwa mgeni rasmi kwenye sherehe hiyo iliyofanyika Hanan'g, Babati na Kiteto, anaeleza kufurahishwa na wanawake na vijana kuwa kwenye mradi huo mkombozi.

Kyomushula, anasema Manyara inalima hekta 56,000 hadi 75,000 kwa mwaka alizeti na mkulima anayelima alizeti asili wastani wa ekari moja anavuna magunia manne mpaka nane na napotumia mbegu ya kisasa anavuna magunia 16 mpaka 20.

**WADAU**

Mtaalamu wa alizeti kutoka kampuni ya By Trade Dudi Yamagaji, anasema katika miaka ya nyuma lilikuwa halipewi kipao mbele ila kwa sasa kulilima ni fursa kubwa kwa wakulima na nchi pia.

Yamagaji anasema: "Mbegu hii ina uzao wenye tija kuanzia kilo 800 yaani magunia 12 kwa eka kwa mbegu za asili na hapo mkulima amekosa ila kama amefuata masharti yote ya kitaalamu na akapanda mbegu hii anaweza kupata magunia 16."

Pia, anafafanua kuwa, hata kunapotokea ukame, mkulima aliyepanda mbegu hiyo, ana uwezo wa kupata walau asilimia 50 ya mavuno aliyotarajia.

**KUTOKA BENKI**

Meneja wa Benki ya CRDB tawi la Babati, Donald Paul, anayesimamia matawi yote ya Manyara, anasema wana dirisha linalosimamia wakulima kwa ajili ya mikopo kuwasaidie kilimo cha alizeti.

Paul anasema benki yake imeshakopesha wakulima wa alizeti zaidi ya 30 na wengine wamewakopesha fedha ya kununua mazao na malori ya kusafirisha mazao ya wakulima.

Anataja masharti ya wakulima ni lazima shamba lihakikiwe na wako tayari kufuatwa shambani kupewa elimu ya mkopo, huku akiwahimiza kujiunga katika vikundi.

Alitumia fursa hiyo kuwataka wakulima kuomba mikopo mapema ili washughulikiwe haraka kuwezesha miradi yao.

**UMOJA WASINDIKAJI**

Mwenyekiti wa chama cha wasindikaji wa mafuta ya alizeti mkoa wa Manyara (Masupa) Athuman Kalunde, anasema mkoa huo una jumla ya wasindikaji 234 wanaohitaji malighafi, ambayo ni alizeti, hivyo wakulima watakaolima zao hilo wana uhakika wa soko.

Kalunde anasema, mkoa unaitaji alizeti kwa ajili ya kusindika tani 120,000 hadi 150,000 kwa mwaka, kukidhi mahitaji ya viwanda na kuisaidia serikali kuokoa fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta nje.

Anawahakikishia wakulima kuwa walime alizeti kwa wingi maana Masupa iko tayari kununua alizeti yote itakayozalishwa katika wilaya zote na kwa bei wakulima watakayoipanga. Anawashauri kulima mbegu ya kisasa ambayo inayotoa mavuno mengi hata kama kuna ukame.

Anaongezea kuwa, bado kiasi cha alizeti kinachozalishwa ni kidogo, hakiwawezeshi wasindikaji kufanya kazi kwenye viwanda msimu mzima, wanaishia kufanya kazi kazi Julai hadi Desemba.

Mweka Hazina wa Masupa, Rashid Iruma, kutoka wilayani Kiteto, anahakikisha soko kwa kutaja uhitaji wa alizeti wilayani Kiteto ni 30,000 mpaka 40,000.

Anasema muda wowote kuanzia sasa wanafungua msimu na watanunua kwa bei Sh. 800 kwa kilo alizeti ya Hysun 33

Meneja wa kampuni ya bima ya mazao ya Acre Africa, Christopher Mazali, anawashauri wakulima kuwa na bima ya kilimo wanapolima mazao yao ili kujikinga na majanga yanayoweza kujitokeza kama vile ukame, mafuliko au mazao kushambuliwa na wadudu .

Anasema mkulima anayekata bima ya kilimo, huwa haumii sana na majanga ya kilimo, kwa kuwa bima inafidia hasara anayoipata na kuepuka kukosa mwelekeo kama ambavyo wakulima wengine wanavyoumia.

**WALIMA ALIZETI**

Mkulima wa alizeti kutoka kijiji cha Sangara kata ya Riroda wilaya ya Babati, Linus Naghali anasema kutokana na elimu wanayoitoa Farm Africa amekubali kubadirika kutoka kilimo cha mazoea cha kupanda mbegu ya asili ambayo mavuno yake ni kidogo na hivyo ataanza kulima mbegu ya alizeti ya kisasa inayovumilia ukame maana hata ukame ukitokea anavuna.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Gallapo, Lohay Langay, anasema kuna haja ya wakulima wabadilike na kuacha kupanda mbegu ya asili, ambayo haina tija kutokana na mabadliko ya hali ya hewa.

Langay anasema, inabidi wakulima wafikie hatua ya mapinduzi ya kulima mbegu ya kisasa kwa ajili ya kilimo cha biashara, kinachowezesha kuwatoa kwenye lindi la umaskini.

Mkazi wa Kijiji cha Chemchem, mkulima Timoth Stowe, anayetumia mbegu ya kisasa, anakiri ni mbegu nzuri maana yeye alipanda ekari mbili na mvua haikuwepo ya kutosha ila amevuna magunia 14, wakati sehemu nyingine alipanda ekari sita mbegu ya asili akaambulia gunia moja tu.

Kilio chake kwa serikali ni kuiomba iwasaidie bei ya mbegu ya Hysun 33 inayouzwa Sh. 35,000 kwa kilo ni kubwa wakulima wengi hawawezi.

# Biashara katika picha



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akimkabidhi Cheti na Tuzo Meneja Biashara na Mkakati wa Mauzo wa Vodacom Tanzania kanda ya Pwani, Caleb Majo, kwa kutambua udhamini waliotoa katika kipindi hiki cha maonesho ya 43 ya sabasaba 2019, jijini Dar es Salaam jana. Kwa miaka mingi Vodacom Tanzania imekuwa ikidhamini maonyesho ya sabasaba upande wa mawasiliano na mwaka huu wamewaandalia wateja wao huduma za kidijitali katika banda lao kwenye maonyesho hayo yanayoendelea. **NA MPIGAPICHA WETU**



Meneja wa Tigo Tanzania, Kanda ya Pwani kusini, Pwani Kaskazini na Kinondoni, Deogratius Daud, akiongea na wakazi wa Chalinze (hawapo pichani ) wakati wa hafla ya uzinduzi wa utoaji wa huduma ya 4G, katika eneo la Chalinze na Vitongoji vyake ikiwa ni sehemu ya kuboresha mawasiliano ya mtandao huo, hafla hiyo ilifanyika katika eneo la soko la Chalinze Wilaya ya Bagamoyo mkoa wa Pwani. **NA MPIGAPICHA WETU**



Watumiaji wa mtandao wa kampuni ya simu za mkononi Airtel, wakisajili simu kwa njia ya vidole katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yanayoendelea katika viwanja vya JK Nyerere barabara ya Kilwa

BIASHARA

# Wakulima wa tumbaku wako Hoi, wazidi kuwa maskini



Wakulima wakiuza tumbaku yao kwenye Chama cha Msingi cha Ushirika (AMCOS) wilayani Kahama. **PICHA : MTANDAO**

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

KINACHOWALIZA wakulima wa tumbaku wa wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga leo ni hiki: "Tumbaku badala ya kuwa mwarobaini na suluhu ya janga la umasikini linalowakabili inakuwa mwiba unaowatesa kila siku."

Wakulima hao kila leo wanajiuliza maswali mengi ya namna wanavyokwenda kulipa madeni ya pembejeo na mikopo ya mabenki yenye riba kubwa inayowakabili na kujikuta kwenye lindi la umaskini .

Wakizungumza kwenye mahojiano maalumu hivi karibuni na Nipashe, wakulima wa zao hilo safari Manjara na Jonas Mponya walisema waliamua kwa dhati kuwekeza rasilimali fedha na nguvu kwenye zao hilo kwa lengo la kuongeza uzalishaji ili kujikwamua kiuchumi na kuongeza kasi ya maendeleo katika mkoa wa kitumbaku wa Kahama , lakini badala ya furaha ni kilio.

Wanaongeza kuwa pamoja na dhamira ya serikali ya awamu ya tano ya Rais John Magufuli

> **"Tumbaku ina madaraja 45, la kwanza mpaka la 45, Kwa mtazamo wangu kumekuwepo na mashinikizo kutoka kwenye kampuni ya ununuzi.**

ya kuwa na Tanzania ya viwanda ili wakulima nao wanufaike kupitia mazao yao ikiwamo tumbaku, hawana tumaini kwa kuwa bei ya kinachozalishwa ni ndogo na gharama ni kubwa.

Jonas Mponya, anasema mpango huo na juhudi za serikali zinakwamishwa na baadhi ya kampuni zinayojihusisha na ununuzi wa tumbaku, ambazo zimekuwa zikitoa na kununua bei za chini ya wastani wa kitaifa dola 1.73 kwa kilo ambayo hailingani na gharama za uzalishaji ambayo iko chini ya bei ya kitaifa iliyopagwa.

Safari Manjala ambaye anawakilisha kilio cha wakulima hao anasema sera ya viwanda haiwezi kufikiwa kwasababu mzalishaji wa malighafi ambaye ni mkulima atakuwa hapati bei stahiki kwa zao la tumbaku .

"Tumbaku ina madaraja 45, la kwanza mpaka la 45, Kwa mtazamo wangu kumekuwepo na mashinikizo kutoka kwenye kampuni ya ununuzi wa tumbaku mfano TLTC na Alliance One tumbaku ya daraja la kwanza na la pili hawataki kuziona zikinunuliwa wanatafuta sababu mpaka zifutwe na wanunuzi wa kampuni huwalazimisha," wanunuzi wa serikali ambao ni Bodi ya Tumbaku (TTB), kuondoa madaraja hayo..."Anadai.

"Baada ya kuondoa madaraja hayo na kushusha bei yake ndipo kampuni zinaanza kuinunua, wanunuzi wananunua kwa bei ya chini ya wastani wa kitaifa , hali ambayo inampelekea mkulima kuishia kulipa madeni ya gharama za pembejeo alizokopa na baadhi yao kushidwa kulipa madeni" anasema Safari .

Jambo ambalo wanaona ni kitu kigeni na hali hiyo sasa inawafanya wakulima kuwa wanafanya kazi bure sawa na kugawa tumbaku zao kwa kampuni wanunuzi.

Anaomba serikali iliangalie suala hili kwa upana pamoja na kuzisimamia na kuzirekebisha sheria za tumbaku kwani kwenye masoko hali imebadilika na inakuwa mwamuzi wa mwisho ni kampuni.

Japo bei ya wastani wa kitaifa ni Dola 1.73 lakini wakulima wanauza masoko yanayosimamia watani wa Dola 1.5 kwa kilo na hiyo inasababishwa na wanunuzi kutokuzitendea haki tumbaku za madaraja ya kwanza na ya pili.

Wao wanapenda wakute daraja la tatu kushuka chini hali inayomkwamisha mkulima kujikwamua kiuchumi.

"Sababu kubwa ni kutaka kumkandamiza mkulima na kumnyonya kwa lengo la kujipatia faida kubwa na hali hiyo iko kwenye kampuni kadhaa (majina tunayo) na kwenye Chama cha Msingi cha Mkwawa Amcos, wameuza zaidi ya kilo 200,000 kwa wastani wa Dola 1.5 jambo ambalo halilingani na gharama za uzalishaji"alisema Safari Manjala .

**MAELEZO YA BODI**

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Tumbaku, Stanley Mnozya, alisema jumla ya kilo milioni 61 za tumbaku zimezalishwa nchi nzima.

Mnozya alipotakiwa kuzungumzia changamoto hiyo alikiri kuwapo kwa changamoto hiyo kwenye baadhi ya kampuni za ununuzi wa tumbaku na kuongeza Kuwa TLTC ilionywa na bodi kuhusu kununua bei ya chini ya wastani na kuwa na usumbufu kwenye masoko na kulazimisha dosari kwenye madaraja ya tumbaku.

Mnozya alisema mpaka sasa wakulima wamegomea zaidi ya masoko manne, akitoa ufafanuzi alisema mkulima ana uhuru wa kukubali ama kukataa kusaini kuuzia soko ambalo linampunja.

Alisema Chama cha Amcos Mishamo katika mkoa wa Katavi kiligomea masoko na Nsimbahiari na Msimba Amcos kutoka kampuni ya TLTC waligomea masoko yao yasisainiwe Tabora mpaka uongozi wa bodi ulipoingilia kati.

Kwa upande wake Meneja Uendeshaji wa Kampuni ya TLTC George Ibrahimu, anasema tumbaku inaweza ikanunuliwa hata kwa Sh. 300 au 200 na kuongeza kuwa Dola 1.73 kwa kilo ni bei ya wastani wa kitaifa lakini mambo yaliyoandikwa kwenye makaratasi tu .

Mkurugenzi wa Uzalishaji wa Alliance One, Mayunga David, alipotakiwa kujibu malalamiko hayo alisema wastani wa bei ya tumbaku unaendana na ubora wa tumbaku na kuongeza kuwa kuna vyama ambavyo viko chini na vimeuza kwa wastani wa bei ya chini sana, na vyama vingine kwa wastani wa juu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kaimu Mkurugenzi wa TCB, Stanley Mnozya, TLTC imenunua kilo milioni 9, Alliance One, milioni 12 na kampuni ya JTI ikinunua kilo milioni 5.5.

UCHUMI

# Wasomi, Profesa Lipumba wanapotaka BoT ikopeshe zaidi

**Na John Kimbute**


Profesa Ibrahim Lipumba. **PICHA: MTANDAO.**

KUNA usemi kuwa ndege wanaofanana huruka pamoja, hivyo wanakwenda njia moja. Ndivyo ilivyo kwa wasomi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na hasa Idara ya Uchumi ambayo imetoa wataalamu wengi walioshika nafasi muhimu za kuweka sera za uchumi serikalini, kuanzia awamu ya kwanza hadi sasa.

Baadhi walihamia upinzani lakini kuna utamaduni wa pamoja wa wana-UDSM ambao haupotei, hata katika ngazi ya mwalimu na mwanafunzi, kwa mfano Waziri wa Fedha Dk. Philip Mpango aliwahi kufundishwa miaka iliyopita na wabobezi kama Profesa Benno Ndulu aliyekuwa Gavana wa Benki Kuu, na Profesa Ibrahim Lipumba, aliyekuwa mshauri wa uchumi Ikulu awamu ya pili.

Hatua ya Profesa Lipumba kutoa rai kuhusu ukopeshaji inaweza kuwa ajenda huru ambayo kwa nafasi yake ya Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi CUF anaweza kuitoa, lakini mara nyingi hoja za vyama vya siasa hasa vinapoanza kampeni ya aina hii au ile ni 'kandarasi' yenye wadau eneo fulani.

Kwa mantiki hiyo kuna suala zaidi ya moja, kuwa ziko sauti serikalini zinazohitaji ajenda zao zitwaliwe na vyama vya siasa au angalau chama kimoja kinachofahamika, ambacho kinaongozwa na mchumi anayeheshimika kama Profesa Lipumba. Akitoa hoja hiyo wanaamini itakolea.

Vile vile kuna urafiki binafsi wa kusaidiana katika suala hili au lile, ila ni wazi kuwa kujenga hoja katika ngazi ya Baraza Kuu la CUF na kutoa tamko hadharani kwa jambo hilo kunahitaji mawasiliano na hata mifumo ya uwezeshaji ili kuwe na 'urasimishaji' wa hitaji la kujenga hoja hiyo au kuanzisha kampeni kama hiyo.

Ni sehemu ya mivutano ya upambanuaji sera serikalini hivi sasa, ambako mwelekeo wa kimapinduzi au wa kijamaa wa kukusanya kodi na serikali kuwa kiongozi kuinua uchumi sasa inaangaliwa upya, ili kukuza sekta binafsi iliyoonekana kuyumba. Suala ni mbinu za kuikuza sekta binafsi, na kwa wachumi wa mwelekeo wa jadi, hasa ni mikopo.

Kwa jinsi suala hilo lilivyotajwa katika vyombo vya habari, wenye kumbukumbu wangedhania ni marudio ya sera ya 'kujaza watu mapesa' iliyobuniwa na John Cheyo mwaka 1992 wakati vyama vingi vinaanzishwa na kupambanua mielekeo yao kiitikadi na kisera.

Si rahisi kusema kama iliwahi kuelezewa vizuri kujaza watu mapesa hasa ni nini, lakini kimsingi usemi huo ulibakia kichekesho kwa wasiokuwa wafuasi wa UDP aliyoiasisi. Ila katika mazingira ya sasa suala siyo 'kujaza watu mapesa' ila kupanua wigo wa kuhusika kwa Benki Kuu katika uchumi.

Kwa baadhi ya wachunguzi wa habari au wafuatiliaji wa sera za uchumi, uingiliaji huo wa sera au ushauri wa Profesa Lipumba unahitajiwa hivi sasa, lakini una mitego maridhawa uchukuliwe vipi. Si tatizo kukumbuka kuwa juhudi tofauti za uwezeshaji kiuchumi na kufikia mikataba ya kumaliza matatizo ya aina hii au ile kupitia Benki Kuu zilileta mitafaruku na zogo kisiasa katika nyakati tofauti. Malipo muhimu ya mikataba au uwezeshaji yanafanyika Benki Kuu, na siyo vigumu kuona mkakati wa aina hiyo, kama ni kificho kiasi fulani, kuwa ni mtiririko wa rushwa.

Kwa mazingira ya sasa, anachosema Profesa Lipumba ingefaa kiunganishwe na hatua ya serikali ya kuondoa amana za mashirika ya umma katika mabenki ya biashara nchini, kiasi cha Sh. bilioni 700 zilizopokonywa na kuhamishiwa Benki Kuu kama amana za serikali 2017. Baada ya hapo, mwaka mmoja baada ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi yakawa yameporomoka kwa asilimia 65 kwani makampuni yalikuwa yanategemea mikopo ya mabenki ya biashara kufikia viwango vya uzalishaji na hata ubora, halafu walipe wakishauza nje.

Biashara ya nje imekuwa ikipona kwa hatua za kutafuta, wakati ambapo mabadiliko ya matumizi serikalini yalikwamisha kulipwa mikopo ya mabenki kwa wafanyabiashara sekta tofauti, soko lao la bidhaa, huduma lilipokauka.

Kinachotakiwa hivi sasa siyo Benki Kuu kukopesha watu binafsi kama wakati wa EPA kwani hakuna njia yenye uwazi jinsi ya kuchagua makampuni 10 au 20 kutolewa mikopo ya Sh. bilioni 10 au zaidi kila kampuni, na lazima kutakuwa na harufu ya rushwa. Vile vile siyo suala tu la kukopesha mabenki kwani fedha kama hizo inabidi zitumike katika biashara kwa haraka ili zuridi benki, na licha ya mikakati ya Benki Kuu ya sasa kuacha kufuatilia mikopo yake katika mabenki ili yajenge mitaji, bado kuna tatizo. Inahitajiwa mfumo wa amana halisi za muda mrefu.

Kwa lugha nyingine, Benki Kuu inatakiwa irudishe zile Shilingi bilioni 700 na ikiwezekana ziwe trilioni moja ziingie katika mabenki ya biashara kama amana za muda mrefu, kwa mfano mikopo bila riba ya miaka 15 au 20.

Siyo rahisi hapa kutoa vielelezo vya sera kama hiyo, kuwa ni wapi mtindo huo ulitumika, ila kuoanisha na zilizokuwa dhamana za mashirika ya umma ambazo si rahisi kuzirudisha, kwani italeta zogo kisiasa. Lakini serikali ikibuni mfumo mpya, kwa mfano nusu ya `mgawo' au 'dividend' kwa kila mwaka kwenda serikalini, halafu iliyobaki mgawo utolewe kati ya utawala na wafanyakazi kwa upande mmoja, na wanahisa kwa upande wa pili.

Bado si rahisi kwa mfumo kama huo kukubaliwa katika kipindi hiki cha kupambana na ujanja na mianya ya kutengeneza fedha za ziada kiulaini, na kutoa rai kuwa Benki Kuu itumbukize Sh. trilioni moja zisizo na mwenyewe ila zitakazorudi katika miaka 20 ijayo kuna hatari zake, kwani zikitumiwa vibaya miongoni mwa wanahisa, bodi au utawala wa mabenki itakuwa vigumu kufuatilia.

> **Kwa lugha nyingine, Benki Kuu inatakiwa irudishe zile Shilingi bilioni 700 na ikiwezekana ziwe trilioni moja ziingie katika mabenki ya biashara kama amana za muda mrefu.**

Hivyo kuwapo kwa uwakala na serikali au Benki Kuu kwa jambo hilo ingeleta tija, kwa mfano kuhusisha fedha hizo kama amana za pamoja na mojawapo ya taasisi za uwekezaji Benki ya Dunia, au kuziweka katika soko la hisa endapo benki hizo zimeorodheshwa, n.k.

Kimsingi hoja ya Profesa Lipumba ina mantiki tofauti na ile ya Cheyo, ambayo haikuwahi kuwa mkakati wa kitaifa na mtoaji hoja hakuwa mchumi licha ya kuwa na uzoefu wa utawala taasisi tofauti. Umuhimu wake ni kuwa, kuondoa dhamana za taasisi za nchi katika mifumo ya mabenki ya biashara iliumiza mabenki, lakini wakiritimba Benki Kuu wakasema tatizo la mikopo isiyolipika lilikuwa udhaifu wa ukopeshaji na 'elimu' kwa wakopaji, wakati tatizo lilikuwa ni mabadiliko makubwa ya soko na mandhari ya kufanya biashara baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani.

Kwa mfano Bajeti ya Serikali ilikuwa inatoa asilimia 26 kwa miradi ya maendeleo awamu ya nne, ikavusha hadi asilimia 40 au pungufu kidogo awamu ya tano. Ni kupoteza asilimia 14 ya Bajeti ya Taifa katika mzunguko wa bidhaa za matanuzi ambako zilikuwa 'mafiga matatu' ya biashara lukuki, msingi wa ukopeshaji na kurejesha mikopo.

UCHUMI

# G20 inavyokumbusha kuwa na tahadhari nyakati hatarishi

**Na Anil Kija**




Baadhi ya vigogo wa mataifa yenye uchumi mkubwa duniani Rais Trump wa Marekani, Waziri Mkuu wa Japan Shinzo Abe na Rais wa China Xi Jinping, wakiwa Osaka wiki iliyopita. **PICHA: BBC**

WAKATI Rais Donald Trump wa Marekani alikuwa ndiye kiongozi anayetafutwa sana kupata nafasi ya kupiga picha naye au kufanya mazungumzo, kuelewa kilichotokea katika mkutano wa nchi 20 zenye uchumi mkubwa wa viwanda duniani, inabidi kutoka nje ya bashasha hizo.

Ni mkutano ambao baadhi ya wachunguzi wa habari walikejeli kuwa haukuwa na umuhimu ila kupata nafasi za kupiga picha za pamoja kwa kumbukumbu, lakini kwingineko wachambuzi walifuatilia ajenda muhimu zilizoinuliwa na jinsi zilivyofuatiliwa. Yako maeneo kadhaa yaliyoainishwa, kufafanuliwa katika mazungumzo kati ya viongozi, na kwingineko walifurahi kutoa misimamo, dunia ijue.

Baadhi ya viongozi waliohudhuria walitaka kumpa Rais Trump somo kuhusu tunu ya amani duniani na umuhimu wa kuilinda, lakini wakakuta yeye pia anafuata njia hiyo. Alizuru Korea Kusini, akafika Panmonjoun mpakani na Korea Kaskazini na kufanya mazungumzo ya dakika 15 na kiongozi mkuu Kim Jong Un wa Korea Kaskazini, ndani ya nchi hiyo, licha ya kuwa ni kituo cha mpakani. Ni tukio lililowasisimua wananchi wa Korea Kaskazini, waanze kuamini kuwa Marekani siyo adui bali inataka waache silaha za nyuklia, warekebishe mifumo ili wafaulu.

Hata hiyo, tukio kubwa zaidi lilikuwa nje ya majadiliano ya mparaganyiko unaoendelea mifumo ya biashara duniani baada ya Marekani kuanza kuinua vikwazo kushoto, kati na kulia ikitaka nchi zirekebise mifumo yao ili kampuni za Marekani ziweze kufanya biashara ipasavyo na mataifa yao.

Baadhi ya wakuu wa nchi na serikali waliohudhuria, hasa wale wa Umoja wa Ulaya walitumia nafasi hiyo kufika Nagasaki, mji wenye makumbusho ya kutisha ya jinsi bomu la atomiki lililoangushwa na Marekani dhidi ya utawala wa kifashisti wa Japan mwaka 1945 lilivyoacha athari za kutisha zinazoonekana hadi kizazi cha sasa.

Tatizo la kumbukumbu hizo ni kuwa hakuna wa 'kumfunga paka kengele,' kwa mfano katika hali hatarishi ya Marekani na Iran, anayetakiwa akumbuke kilichotokea Japan mwaka 1945 ni Iran au ni Marekani?

Hivi suala ni kutotumia tena bomu la atomiki, siku hizi ni mabomu ya nuklia, au kuondoa sababu, viashiria vya kufika hapo?

Mkutano wa Osaka ulifanyika wakati Iran ikimaliza muda wa tahadhari kwa Umoja wa Ulaya wa siku 10 kubadili mazingira kuhusu mkataba wa kimataifa wa udhibiti wa nguvu za nuklia nchini Iran, ikiwa ni pamoja na kuondolewa vikwazo vya Marekani iliyojitoa katika mkataba huo.

> **"Rais Trump alitoa kauli ya jumla kuwa 'hapatakuwa na hatua mpya za ongezeko la viwango ushuru wa forodha kwa sasa,' kauli iliyotuliza hali kwa kiasi fulani.**

Iran ilitangaza baada ya mkutano huo kumalizika mwishoni mwa wiki kuwa imeshafikia na inapitiliza kiwango cha urutubishi chini ya mkataba huo wa 2015, kwani hauwezi kutumika tena kama ulivyo. Rais Trump alitoa taarifa kuwa 'wanacheza na moto,' na wanatakiwa wajue hilo.

Nje ya maeneo hayo, mkutano wa G20 uliwezesha mazungumzo kuhusu maeneo nyeti katika hali ya uchumi na biashara kimataifa na Rais Trump kwa mfano alikuwa na mazungumzo na Rais Xi Jinping wa China, an ziko nchi kadhaa (kama India) zenye wasiwasi na ushuru zaidi wa forodha kuuza bidhaa Marekani.

Rais Trump alitoa kauli ya jumla kuwa 'hapatakuwa na hatua mpya za ongezeko la viwango ushuru wa forodha kwa sasa,' kauli iliyotuliza hali kwa kiasi fulani huku ikiruhusu nafasi kwa majadiliano katika mazingira ya uelewano kiasi fulani. Nje ya suala la Iran, inaelekea Marekani ilijitahidi kuelewana na nchi za G20 masuala nyeti tofauti.

Baadhi ya waliohudhuria kwa mfano Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini walisema mkutano huo ulikuwa wa mafanikio, moja ya sababu ikiwa ni nchi zilizobaki na hasa Umoja wa Ulaya, kusisitiza dhamira ya kutekeleza viwango vya kuzuia mabadiliko tabia nchi. Mkutano huo umefanyika wakati nchi kadhaa zina viwango vya joto vya kutisha, na wakati unamalizika, mafuriko yasiyo ya kawaida jiji la Mumbai nchini India yaliumiza mamilioni.

Na kwa upande wa Rais Cyril Ramaphosa wa Afrika Kusini, aliridhika zaidi na ufuatiliaji wa Benki ya Dunia na mashirika mengine ya kimataifa kufikia maendeleo endelevu Bara la Afrika hadi mwaka 2030, kuwa nchi za viwanda, uchumi wa kati.

Yako maeneo ambako licha ya viongozi kufanya mazungumzo, hapakuwa na jipya, mabadiliko katika misimamo inayoeleweka. Kwa mfano Rais Trump alizungumza na Rais Xi, lakini ni uendelezaji wa majadiliano ya kina kuhusuu urekebishaji mifumo ya biashara na uwekezaji kati ya nchi hizo mbili, na inawezekana hawakujadili kabisa suala la kampuni kubwa ya simu za mkononi ya Huawei, ambayo maofisa wa idara na mashirika yote ya kiserikali nchini Marekani wametakiwa kuelewa kuwa imepigwa marufuku kushirikiana nayo. Walisema ni 'blacklisted.'

Pia haikutazamiwa kuwa kungekuwa na maendeleo ya wazi katika ajenda nyeti kadhaa kati ya Marekani na Russia, ila tofauti na China ni kuwa Russia haina haraka ya kurekebisha uhusiano wake uliozorota na Marekani. Uvamizi na kumega Crimea ambayo ilikuwa sehemu ya Ukraine ilikuwa chanzo cha uhasama kupanda kiasi kikubwa na bado inaunga mkono makundi ya watu wanaozungumza Kirusi wanaotaka Ukraine Mashariki ijitawale, iwe karibu zaidi na Russia.

Ila Russia inaelewana kiasi fulani na Rais Trump kuhusu Russia kuingilia uchaguzi mkuu wa Marekani 2016 ambako Trump anawakingia kifua, lakini ameruhusu vita ya virusi wa kompyuta ambako inaelekea Russia ndiyo ilianza. Mengine yanafanywa bila Trump kujua ashtuke gazetini.

Unaweza kusema kuwa kati ya nchi zilizohudhuria mkutano wa G20, ni Umoja wa Ulaya ambao ulikuwa na malengo makubwa zaidi katika mkutano huo, na ni vigumu kusema walifanikiwa kiasi gani.

Ukiangalia katika mtandao ziko taarifa za msimamo uliochukuliwa na Rais wa Baraza la Mawaziri la EU, Donald Tusk (wa Poland) ambaye muda wake umeisha na mrithi wake (pamoja na nafasi zingine) ameshapatikana. Alisisitiza kuwa dunia iendeshwe kwa nchi kuwasiliana na mifumo kuheshimiwa, na siyo nchi moja kulazimisha dunia nzima ifuate kile inachokitaka. Hiyo kwa jumla ni hisia nzuri lakini kanuni za kuwekwa pamoja na jumuia ya kimataifa hazina uwezo wa kurekebisha nchi mifumo yao imejikita katika ukandamizaji, na ili tawala kama hizo zidumu, zinajipeleka katika vita ili kuamsha uzalendo. Kimsingi uzalendo huo ni dhidi ya Marekani, ndiyo inayoogopwa, kuchelewa, huku wengine ni kama wanadharauliwa.





# Wafa kwa kufukiwa na kifusi mgodini

**Na Grace Mwakalinga,**

CHUNYA

WATU wawili wamepoteza maisha baada ya kufunikwa na kifusi katika mgodi wa dhahabu unaomilikiwa na Mwembe Msemakweli katika kitongoji cha Izumbi Kijiji na Kata ya Sangambi, Chunya mkoani Mbeya.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sangambi, Lusekelo Lwesya, alisema alipata taarifa ya tukio hilo Julai 2, mwaka huu, kwamba Zakayo Myunga (30) na Ayoub Nelson (33) wamefariki dunia baada ya kufukiwa na kifusi wakati wakiendelea na shughuli za uchimbaji.

Alisema baada ya kupokea taarifa hizo, alizifikisha kwa Mtendaji wa Kijiji, Frola Chiwanga, na kupiga mbiu kuomba msaada kutoka kwa wananchi ambao walifanya juhudi za kuwatoa chini ya mgodi huo, umbali wa mita arobaini na tano kutoka juu.

"Baada ya kufanya jitihada za kuwatoa ambazo zilianza tangu majira ya asubuhi mpaka usiku wa saa mbili, wananchi na uongozi walipeleka miili ya marehemu katika zahanati ya Kijiji," alisema Lwasye.

Baada ya kuthibishwa na daktari kuwa tayari wamefariki dunia, n Mtendaji wa Kata ya Sangambi, Ntundu Chapa, alitoa taarifa polisi wilayani Chunya ambao walifika eneo la tukio na kwa kushirikiana na daktari, walifanyia uchunguzi miili hiyo kisha kuwakabidhi ndugu kwa ajili ya mazishi.

Mke wa Myunga, Anna Mwailondele (26), alisema wakati wa tukio hilo, alikuwa kwenye shughuli zake za ujasiriamali na kwamba mume alimuaga asubuhi kuwa anaenda kwenye kazi zake za uchimbaji madini.

Alisema kifo cha mume wake ni pigo kubwa kwa sababu walikuwa na ndoto nyingi za kutimiza na kwamba amemwachia watoto wawili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema chanzo cha vifo hivyo ni kukosa hewa na kujeruhiwa na mawe kichwani na maeneo mbalimbali ya miili.



Watumishi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kutoka idara mbalimbali wakiwa katika mafunzo ya namna ya kukabiliana na magonjwa ya mlipuko, yaliyotolewa na wataalamu kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Mbeya jana. **PICHA: KENNETH NGELESI**

# Viuatilifu bandia vya mil. 600/- vyanaswa

**Na Grace Mwakalinga,**

MBEYA

TUME ya Ushindani Tanzania kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, imekamata shehena ya viuatilifu vyenye nembo bandia na visivyoruhusiwa kuingizwa nchini vyenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 600.

Shehena hiyo ilikamatwa hivi karibuni na Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na FCC kwenye kituo kidogo cha polisi cha Inyala nje kidogo ya Jiji la Mbeya ikiwa inaingizwa na mfanyabiashara Yona Kalinga.

Mkurugenzi wa FCC, John Mduma, alisema walipata malalamiko kutoka kwa kampuni ya Rista Life Science Tanzania Limited kuwa kuna mfanyabiashara anatumia nembo yao kufanya biashara yake ya viuatilifu.

Alisema taarifa hizo walizifanya siri na kuanza kuzifanyia kazi na tume hiyo kwa kushirikiana na polisi, walimnasa mfanyabiashara huyo akisafirisha viuatilifu bandia ambavyo vimepigwa marufuku kuingizwa nchini akipeleka kuwauzia wananchi mkoani Mbeya.

Alisema viuatilifu hivyo vina thamani ya Sh. milioni 600 na kwamba baada ya kukamata gari lililobeba walilipeleka polisi kwa ajili ya usalama.

Alipohojiwa, Kalinga alikiri kuingiza bidhaa hizo nchini kinyume cha utaratibu lakini vikiwa vimepigwa marufuku.

Mkaguzi wa Viuatilifu kutoka Taasisi ya Utafiti ya Viuatilifu katika Ukanda wa Kitropiki (TPRI) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Emmanuel Mausi, alikiri kuwa viuatilifu hivyo vimepigwa marufuku kuingizwa nchini na kwamba bila jitihada za polisi na FCC kubaini mchezo huo, vingeuzwa kwa wakulima.

"Wafanyabiashara wasiokuwa waaminifu wamekuwa wakiwaingizia hasara kubwa wakulima ambao hununua viuatilifu hivyo ili kuhudumia mashamba yao. Jitihada za kuwafichua zinapaswa kuendelea ili kuwabaini na wengine na kumaliza tabia ya uingwizaji wa viuatilifu feki nchini," alisema Mausi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, amewatahadharisha wafanyabiashara kuzingatia sheria na taratibu za nchi na kwamba jeshi lake liko macho kuhakikisha wananchi wanapata bidhaa zilizokubalika.

Alisema Kalinga atashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na kwamba utaratibu wa kumfikisha mahakamani tayari umeanza.

# RC Mbeya awajia juu watumishi halmashauri

**Na Grace Mwakalinga,** TUKUYU

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, amewatahadharisha watumishi wa umma kutokuwa sehemu ya kukwamisha jitihada za serikali za kuleta maendeleo kwa wananchi.

Badala yake amewataka wahakikishe fedha zinazotolewa kwa ajili ya shughuli za miradi zinatumika kama ilivyokusudiwa.N Chalamila alisema hayo juzi kwenye kikao cha Baraza la Madiwani kilichokuwa kinajadili majibu ya hoja na mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2017/2018 katika Halmashauri za Wilaya ya Rungwe na Halmashauri ya Busokelo.

Alisema baadhi ya watumishi wamekuwa kikwazo katika kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutafuna fedha za serikali jambo ambalo alilikemea na kuwataka kuwajibika kwa mujibu wa sheria ya kazi na kiapo chao.

Mkuu huyo wa mkoa alisema mara kadhaa amekuwa akipokea malalamiko ya baadhi ya watumishi kutokuwa waadilifu na kupenda rushwa wakati wa kusimamia shughuli za maendeleo na baadhi hukiri na kwamba hali hiyo imechangia baadhi ya miradi kutokukamilika na mingine kujengwa chini ya kiwango.N "Vitendo vya rushwa bado vipo kwa baadhi ya watumishi wa umma. Nawaeleza serikali haitaki mchezo, kama una tamaa ya kujipatia fedha kwa udanganyifu bora ujiondoe mapema badala ya kusubiri utumbuliwe kwa aibu. Nawasisitiza watumikieni wananchi kwa mujibu wa kanuni na sheria na kuleta maendeleo," alisema.

Chalamila alionyesha kutoridhishwa na Wilaya ya Rungwe kupata hati isiyoridhisha kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Alisema kwa mujibu wa taarifa ya CAG, baadhi ni malipo yenye viambatisho pungufu ya Sh. milioni 114.4 na hati za malipo ambazo hazikuonekana kwenye ukaguzi ni Sh. milioni 8.6 pamoja na vitu vingine.


Kutokana na hali hiyo, Chalamila aliwataka watumishi kuongeza ufuatiliaji wa mara kwa mara kwenye makusanyo na matumizi ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inayotekelezwa na ununuzi wa umma unaofanyika unakuwa na thamani ya fedha iliyotumika.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Mariam Mtunguja, alisema kati ya wilaya tano za mkoa wa Mbeya, Rungwe pekee ndiyo imetia doa kwa kupata hati isiyoridhisha kitendo ambacho si kizuri kabisa.

Aliwataka viongozi wa Halmashauri ya Wilaya Rungwe kutoa ushirikiano kwa wakaguzi wanapofika na kwamba wasisite kutoa taarifa yoyote ambayo itahitajika na CAG.

Mkuu wa Wilaya Rungwe, Julius Charya, alikiri Wilaya ya Rungwe kupata hati isiyoridhisha mwaka jana na kwamba hali hiyo ilitokana na usimamizi hafifu kwenye miradi ya maendeleo iliyopita.

Alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya hiyo, Loema Peter, kuchukua hatua kwa mujibu wa sheria dhidi ya watendaji wasiowajibika na kuwakumbusha madiwani kuwa wasimamizi wazuri.





# Halmashauri zashauriwa fedha za vijana, wanawake

**Na Peter Mkwavila,**

CHAMWINO

HALMASHAURI za wilaya mkoani Dodoma zimetakiwa kuanzisha mfumo wa kuwa na miradi ya kudumu itakayosaidia makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambao wanakopeshwa kupitia mfuko wao.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Tawala Msaidizi wa Serikali za Mitaa Mkoa wa Dodoma, Emmanuel Kuboja, alipokuwa akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino ambacho kilikuwa kwa ajili ya kupitia taarifa ya ukaguzi wa hesabu za halmashauri za mwaka 2017/18 ambayo ilipata hati safi. Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa mkoa huo, Dk. Binilith Mahenge, Katibu huyo alisema mfumo unaotumika kwa hivi sasa wa kuwakopesha makundi hayo kupitia asilimia 10 ya mapato ya ndani inayotengwa kwa ajili yao ni vizuri ukabadilishwa kwa kuwajengea majengo ya miradi kama vile ya ufugaji.

Alisema halmashauri ni muhimu sasa wakabuni mfumo utakaowawezesha makundi hayo kuepukana na mikopo ya kupatiwa fedha taslimu.

Alibainisha kuwa wanufaika wa mikopo hiyo wajengewe majengo watakayotumika kwa kufanyia shughuli mbalimbali zikiwamo za ujasiriamali na ufugaji.

"Ninaziomba halmashauri zote badilisheni mfumo wa kuwakopesha fedha taslimu makundi yao, badala ya kuwapatia fedha, wajengeeni majengo ambayo yatakayo wasaidia kufanya ujasiriamali ikiwa na pamoja na shughuli za ufugaji wa kuku na mifugo," alisema.

Pamoja na hayo, aliwataka wanaokopeshwa fedha hizo wahakikishe wanazirejesha kwa wakati ili wengine waweze kupatiwa mikopo hiyo.

Awali, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Athumani Masasi, aliwataka watendaji wa idara mbalimbali wahakikishe wanafanya kazi kwa ushirikiano ili kuilinda hati hiyo safi iliyotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Akizungumza kuhusiano na taarifa ya matokeo ya ukaguzi wa hesabu za halmashauri hiyo, alisema aliwasilisha hesabu zake za mwaka 2017/18 kwa CAG kwa ajili ya ukaguzi septemba 30, mwaka jana.

Alisema kutokana na ukaguzi huo kukamilika CAG alitoa taarifa na maoni baada ya kukamilika kwa ukaguzi huo, huku akiipa hati safi kwa kuwa hesabu zake zilikuwa vizuri.



Majeruhi wa moto, Mkami Wambura (19), mkazi wa Kijiji cha Mlazo, Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma, akiwa amelazwa wodi namba 16 Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo juzi, akidaiwa kuunguzwa na mumewe. Wanaomhudumia ni wauguzi wa hospitali hiyo, Mary Komba na Samwel Tindwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wamlilia RC kuwaepusha kero kutembea kilomita 10

**Na Augusta Njoji,**

MPWAPWA

SERIKALI imeombwa kuwajengea shule ya sekondari wananchi wa kata ya Lufu wilayani Mpwampwa, kutokana na watoto wao kutembea umbali wa kilometa 10 kufuata elimu kata jirani ya Luwundwa.

Kilio hicho walikitoa kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ambaye ndiye mkuu wa mkoa wa kwanza kutembelea kata hiyo tangu kuanza kwake mwaka 1997.

Wananchi hao walisema wanafunzi wengine wanalazimika kupangiwa vyumba ili kuishi mazingira jirani na shule na kuwaepusha na mimba watoto wa kike. n "Wanapotembea umbali mrefu humo njiani vishawishi ni vingi, wazazi wenye uwezo wamewapangia vyumba watoto wao huko huko ili kuwaepusha na mimba, naomba serikali itusaidie kutujengea shule ya sekondari," alisema mkazi wa kata hiyo, Stephan Mtambulo.

Mtambulo alisema wanafunzi kutoka shule za msingi Ilala, Mlimo na Gomuhungilo wakifaulu inabidi wakasome shule katika kata ya Luwundwa ambayo ipo mbali.

Naye, Jurica Makuya aliomba serikali isikie kilio chao kwa kuwajengea sekondari ili watoto wao wasome karibu na kata yao.

Alisema kata hiyo ipo milimani hivyo wanafunzi wanateseka kwenda umbali mrefu kusoma sekondari.

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Paulo Sweya, alisema halmashauri hiyo imeshajipanga kusaidia ujenzi wa shule hiyo mara baada ya wananchi kuandaa eneo na kuchangia nguvu zao.

Akijibu kilio cha wananchi hao, Dk. Mahenge aliwaomba wananchi kuchangia nguvu ili kujenga shule hiyo hadi hatua ya lenta halmashauri itawapa vifaa vya kumalizia.

"Viongozi wa halmashauri orodhesheni shughuli ambazo wananchi wanaweza kuchangia katika kujenga shule yao ya kata yenye vijiji vitatu vya Mlimo, Gomuhungilo na Lufu," alisema.

Katika hatua nyingine, Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) umechonga barabara yenye urefu wa kilometa 17 kwenye kata hiyo, ambayo haikuwa na barabara kwa muda mrefu kutokana na kuwa milimani.

# W'biashara washauriwa mfumo Kaizen

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeshauriwa kuwahimiza wafanyabiashara wenye viwanda kutumia mfumo wan wa uimarishaji uwezo wa viwanda vya uzalishaji kupitia Uboreshaji wa Tija na Ubora (KAIZEN) ili kuzalisha bidhaa zenye ubora.

Akizungumza jana na Nipashe, Meneja wa Shirika la Viwanda nchini (SIDO), mkoani Dodoma, Sempeho Manongi, alisema mfumo huo utaongeza tija kwenye bidhaa zao na kuwawezesha kuleta ushindani katika soko la Afrika Mashariki na Kati.

Alisema mfumo huo asilia yake ni Japan na unatumiwa barani Asia na Ulaya unachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza hasara katika biashara ambazo zinafanywa na wawekezaji katika viwanda.

"Sasa hivi Tanzania imeingia katika soko la Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), wasipohimizwa kutumia mfumo huo itawawia vigumu kuleta ushindani wa bidhaa ambazo zitapelekwa kwenye masoko hayo.

"Tanzania tusipokuwa makini tutakuwa sehemu ya mapitisho ya bidhaa za wenzetu katika masoko hayo, naiomba serikali kwa kushirikiana na SIDO tuwahimize na kuwafundisha jinsi ya kutumia mfumo huo, walete ushindani wanapoingia kwenye masoko hayo," alisema Manongi.

Manongi alisema inapohimizwa uwekezaji wa viwanda pia itumike nafasi hiyo kuhimiza matumizi ya mfumo huo.

Alisema Sido imeanza kutoa elimu ya mfumo huo katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Morogoro na jijini Dodoma, lengo ni kutaka wajue faida ya mfumo huo pale unapoutumia.

Alifafanua zaidi ya kuwa mfumo huo ni muhimu sana japokuwa wenye viwanda wengi wanaukwepa kwa sababu inahitaji muda wa kufanya marekebisho katika kiwanda kabla ya kuanza kuutumia.

Alitolea mfano wa kiwanda cha A2Z ambacho kinatumia mfumo huo kimefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwa kupata matokeo mazuri ya bidhaa wanazozalisha zilizopelekea kutwaa tuzo ya ubora na kuzishinda nchi zaidi ya 14.

"Sido mkoani Dodoma inaendelea kuipa kipaumbele sekta ya uzalishaji wa vyakula kwa wajasiriamali wadogo hapa jijini ili waweze kuendana na kasi ya watu waliohamia jijini Dodoma na wanaoendelea kuhamia," alisema.







Mjasiriamali akipika vitumbua kwa ajili ya kuuza ili ajipatie riziki, katika eneo la Kigogo Luhanga, jijini Dar es Salaam jana. Hata hivyo, aina hii ya biashara si rafiki kwa afya kwa kuwa inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kutokana na kutofunika chakula chake. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Ataka elimu masuala ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,**
ZAN ZIBAR

MWENYEKITI wa Bodi ya Kamisheni ya Ardhi Zanzibar, Abdi Khamis Faki, amesema elimu inahitajika juu ya masuala ya ardhi ili kumaliza migogoro inayoikabili jamii katika sekta hiyo.

Akizungumza katika ziara iliyofanywa na bodi hiyo kwa ajili ya kukusanya taarifa na kuangalia hali halisi ya migogoro ya ardhi, alisema baadhi ya watu katika jamii bado hawataki kufuata utawala wa sheria juu ya masuala ya ardhi hali inayosababisha kuongezeka migogoro siku hadi siku.

Faki alisema utoaji na umiliki wa ardhi una taratibu na sheria zake lakini baadhi ya watu hukiuka taratibu hizo na kufanya wanavyotaka kwa makusudi hususani kufanya shughuli za ujenzi katika maeneo ya wazi.

Alisema baadhi ya watu wamekuwa wakiendesha shughuli za ujenzi au makazi ya kudumu katika maeneo ya wazi ambayo yametengwa na serikali, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

"Bado kuna changamoto ya jamii kujenga katika maeneo ya wazi. Changamoto hii inazua migogoro kila siku jambo linatakiwa itolewe elimu ya hali ya juu ili kuondosha kabisa migogoro ya ardhi," alisema.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema masheha wanapaswa kupewa elimu ya ardhi ili wajue wanahusika vipi katika kusimamia migogoro ya ardhi inayotokea katika shehia zao.

Mwenyekiti huyo pia alisema bodi hiyo bado inakusanya taarifa juu ya masuala ya ardhi na baadaye watajadili na kufanyiwa kazi taarifa hizo.

Nao baadhi ya wananchi walisema viongozi wa ngazi za juu wanapaswa kuwa watatuzi wakuu wa migogoro ya ardhi badala ya kuichochea na kwamba imekuwa ikizidi kutokana na kujihusisha nayo.

# Waandishi waonywa habari udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari nchini wametakiwa kuwa na utaratibu mzuri wa kutoa habari za udhalilishaji wa kijinsia ili kuepusha kuwadhalilisha waathirika wa vitendo hivyo.

Akifungua jana mafunzo kwa waandishi wa habari yanayohusu utetezi wa haki za watoto, Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mouldline Castico, alisema katika matumizi ya vifaa vya

kisasa (smartphone) kila mtu amekuwa mrusha habari au tukio lililotokea hata kama mtu anakata roho jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

Alisema inapotolewa taarifa ya mtoto amefanyiwa ukatili kwa kumwonyesha sura yake na sauti kama ilivyo au hata jamiii yake inayomzunguka, ni kuzidisha maumivu ya kiakili na kisaikolojia kwa mtoto na familia yake kwa ujumla.

Castiko alisema masuala ya udhalilishaji yana maumivu makali kwa wale wanaofanyiwa na ni mambo ya aibu. Alisema yasipodhibitiwa vizuri na waathirika wa vitendo hivyo wanapoona wamerushwa katika vyombo vya habari, hutamani kujidhuru na wengine kujiua kabisa.

Aidha, alitoa wito kwa mamlaka zinazohusika na mawasiliano, kuendelea na jitihada za kuwadhibiti wanaorusha matukio yalio kinyume cha sheria za mitandao ili hadhi ya mwanadamu iheshimiwe.

Waziri Castico aliwataka watendaji wanaoshughulikia matukio ya udhalilishaji yanayoripotiwa kuyafanyia kazi kwa taratibu zilizowekwa ili kutunza ushahidi utakaofanikisha kuwatia hatiani watakaobainika kufanya vitendo hivyo.

Naye Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (Unicef), Ahmed Rashid, alisema shirika hilo litashirikiana na Serikali ya Zanzibar katika kupambana na vitendo hivyo na kuhakikisha vinamalizwa.

Alisema watoto wengi wamekuwa wakiachwa nyuma kutokana na umaskini uliokithiri katika familia zao na kwamba kudhalilishwa kwa mtoto mchanga kunahatarisha makuzi yake.

Rashid alisema ukuaji wa mtoto chini ya miaka mitano unatakiwa uwe sawa kwa watoto wote, hivyo kutokuwapo kwa usawa huo kunahatarisha pia kufikiwa kwa malengo ya 2020 na serikali.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Wahamaza, Salim Said Salim, alisema kuwa hali za watoto inasikitisha na kwa kiasi fulani imekuwa ikitisha katika jamii.

# Watoto watakiwa kujilinda na ukatili

**Na Rahma Suleiman,**

ZANZIBAR

WATOTO wametakiwa kujitambua, kuwa na elimu ya udhalilishaji na kuwekewa mazingira salama ili kujikinga na vitendo viovu vinavyofanywa dhidi yao.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Kijiji cha Kulelea Watoto Zanzibar (SOS), Asha Salim Ali, katika kongamano la watoto lililofanyika kijiji cha SOS Mombasa.

Alisema bado watoto wanahitaji ulinzi na kushirikishwa katika mambo yanayowahusu ili kuhakikisha kuwa wanajengewa maisha mazuri kwa mustakabali wao wa maisha.

Akizungumza katika kongamano hilo, Meneja wa Huduma ya Simu kwa Mtoto, Fatma Ahmad, alisema watoto wengi wanadhalilishwa na kukosa msaada wakati wa matukio.

Fatma alisema kupitia kongamano hilo, watoto watapata fursa ya kuelezea changamoto zao ambazo baadaye zitafanyiwa kazi.

Hata hivyo, aliwataka watoto hao kuitumia huduma ya simu Na. 116 pale wanapohisi kuna matendo ya udhalilishaji wanafanyiwa au wanataka kufanyiwa.

Alisema njia hiyo ni salama kwao kwa vile kuna watoto wengine wanashindwa kuelezea namna wanavyofanyiwa vitendo vya udhalilishaji wakihofia kupigwa na wazazi wao.

Meneja huyo alisema kupitia huduma hiyo, watakuwa salama na kujieleza kwa namna yoyote bila ya kikwazo chochote.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Watoto Shehia ya Mahonda, Thureiya Hassan Mohammed, alisema mtoto ana haki ya kulindwa, kupewa elimu na kukingwa dhidi ya majanga yanayoweza kumwathiri.

# SABASABA PICHANI



Ofisa kutoka Bodi ya Usajili Wataalamu wa Mipangomiji, Irine Lihundi, akitoa maelezo kwa mmoja wa mwananchi aliyetembelea banda la Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) jijini Dar es Salaam.




Watoto wakicheza nje ya mabanda ya biashara.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Kituo cha Mikutano (AICC), Fred Maro, akiongea na mteja aliyetembelea banda la Mituo cha Mikutano cha JNICC katika Maonyesho ya Kimataifa ya Biashara (Sabasaba) Dar es Salaam jana.



Mkurungezi Mtendaji wa Sunshine Industrial ltd, Siddaraje Krishna, akimuhudumia mteja aliyetembelea katika banda hilo katika Maonyesho ya Kimataifa ya 43 ya Biashara (Sabasaba) Dar es Salaam jana.



Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakipumzika baada ya kutembelea maonyesho hayo.



Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wakiangalia farasi kwenye maonyesho hayo.

**PICHA ZOTE NA MIRAJI MSALA**

# Wafiwa wa ajali za ndege 'kulamba' dola milioni 100

**WASHINGTON,** Marekani

KAMPUNI ya kutengeneza ndege ya Boeing imesema kuwa itatoa Dola za Marekani milioni 100 kwa familia, serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali ya Ethiopia na Indonesia.

Imesema lengo la kutoa fedha hizo ni kusaidia familia na jamii za watu waliopoteza maisha yao kwenye ajali mbili za ndege muundo wa 737 MAX.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters, hatua hiyo ni katika juhudi za kuimarisha taswira ya kampuni

**Lengo la kutoa fedha hizo ni kusaidia familia za watu waliopoteza maisha yao kwenye ajali mbili za ndege muundo wa 737 MAX.**

hiyo ambayo hadhi yake imeshuka kwa kiwango kikubwa katika siku za karibuni.

Hii ni kufuatia ajali iliyotokea Machi mwaka huu iliyozua utata, na kwamba abiria wote 157 wa Ndege ya Shirika la Ethiopia Airlines waliokuwa safarini kutoka Addis Ababa, Ethiopia, kuelekea Nairobi Kenya na ile ya ndege ya Shirika la Indonesia Airlines iliyotokea mwaka wa 2018.

Mkurugenzi Mkuu wa kampuni hiyo, Dennis Mullenburgh, alisema kwamba pesa hizo zitatolewa kwa kipindi cha miaka kadhaa ijayo. Hata hivyo, hakutoa maelezo ya undani namna fedha hizo zitakavyolipwa, wala utaratibu utakaofuata.

Boeing inaendelea kuchunguzwa na taasisi mbalimbali na inakabiliwa na takriban kesi 100 zilizowasilishwa na familia za waathiriwa wa ajali hizo mbili.

Kwa jumla, watu 346 walipoteza maisha yao kwenye ajali hizo mbili. **VOA**

## Pasi ya kusafiria, namba za magari vyaadimika Zimbabwe

**HARARE,** Zimbabwe

ZIMBABWE inakabiliwa na upungufu wa pasi za kusafiria pamoja na vibao vya namba za magari hatua inayowafanya raia kusubiri muda mrefu ili kuvipata.

Mbali na uhaba wa vitu hivyo, pia taifa hilo linakumbwa na tishio la njaa.

Wakati haya yakiripotiwa, Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, alisema kwamba taifa hilo linahitaji kuagiza tani 800,000 za mahindi kutokana na ukame ulioathiri mazao na kupunguza zaidi ya nusu ya mavuno, lakini akiahidi hakuna mtu yeyote atakayekumbwa na njaa.

Wazimbabwe waliokuwa na matumaini makubwa ya mabadiliko ya hali baada ya Rais Mnangagwa kuchukua madaraka kutoka kwa Robert Mugabe baada ya mapinduzi ya mwaka 2017, bado hawajaweza kushuhudia mabadiliko hayo.

Zimbabwe imekumbwa na upungufu mkubwa wa dola ya Marekani, mafuta, mikate na umeme kukatika kwa saa 15. Jana, mamia ya watu walikuwa wamefurika kwenye ofisi za kutolea pasi hizo zilizopo mjini Harare, wengine wakiwa wamefika ofisini hapo kuanzia saa 11 za alfajiri, hata hivyo waliambiwa watazipata mwaka 2021.

Hali hiyo inatokana na kukosekana kwa karatasi maalumu na wino vinavyotumika kutengeneza pasi hizo. Vifaa hivyo huagizwa kutoka nje, lakini kwa sasa hakuna fedha za nje za kuagizia.

Mmoja ya wananchi aliyekuwa amepanga mstari wa kuomba pasi ya kusafiria, Bothwell Mhashu alisema anataka kutoroka kwenda Namibia kuishi na kaka yake mkubwa kutokana na hali mbali ya uchumi.

Alisema aliomba pasi tangu Juni 2018 na alitakiwa kuwa ameipata baada ya miezi mitatu.

Mwaka 2008 Wazimbabwe walilazimika kulala kwenye ofisi hizo za kutolea pasi ili wawe wa mwanzo ifikapo asubuhi kuanza mchakato wa maombi. **DW**



Rais wa Marekani, Donald Trump (kushoto), akipeana mkono na Kiongozi wa Korea Kaskazini, Kim Jong-Un, wakiashiria ishara ya amani baina ya nchi zao. **PICHA: REUTERS**

# Korea Kaskazini 'yaibwagia zigo' la lawama Marekani

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imeilaumu Marekani kwa kuendeleza uhasama licha ya nchi hizo mbili kukubaliana kurejelea mazungumzo ya nyuklia siku chache zilizopita.

Maofisa wa Pyongyang wametangaza kuwa Marekani bado ina mtizamo hasi dhidi ya taifa lao, licha ya mkutano wa kihistoria uliofanyika siku chache zilizopita kati ya Rais Donald Trump na kiongozi wao, Kim Jong-Un.

Wawakilishi wa Korea Kaskazini katika Umoja wa Mataifa wamesema Marekani inataka kuhujumu mazingira ya amani yaliyoko katika rasi ya Korea na kuzitaka nchi zote kuwa waangalifu.

Pyonyang pia imeilaumu Washington kwa kuhujumu hali ya amani inayoshuhudiwa katika rasi ya Korea.

Rais Trump siku ya Jumapili alikutana na mwenzake wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un katika eneo lisilokuwa na wanajeshi linalogawanya Korea Mbili.

Rais Trump alikuwa rais wa kwanza wa Marekani aliye madarakani kukanyaga Korea Kaskazini, na baada ya mazungumzo yaliyodumu kwa saa moja wawili hao walikubaliana tena kurejea mazungumzo ya nyuklia yaliokwama.

Lakini taarifa iliyotolewa na Korea Kaskazini siku ya Jumatano inaashiria mataifa hayo mawili huenda yakaanza tena kurushiana cheche za maneno kama ilivyoshuhudiwa siku za hivi karibuni.

Ujumbe wa Korea Kaskazini ulisema unajibu madai yaliotolewa na Marekani kuwa taifa hilo liliikuka sheria inayoangazia uingizaji wa bidhaa za petroli kutoka nje iliyowekwa mwaka 2017.

Pia, ilisema nchi hiyo imesema kuwa inajibu barua ya pamoja iliyotumwa na Marekani, Ufaransa, Ujerumani na Uingereza kwa nchi wanachama wote wa Umoja wa Mataifa ambayo ilitoa wito Korea Kaskazini kuwekewa vikwazo zaidi.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa barua hiyo iliyataka mataifa wanachama wa Umoja huo kuwaondoa wafanyikazi wa Korea Kaskazini kutoka nchini mwao.

"Kile ambacho hatuwezi kulifumbia macho ni ukweli kwamba barua hiyo ya pamoja iliandikwa siku ambayo Rais Trump alipendekeza tupange mkutano mwingine," taarifa hiyo ilieleza na kuongeza:

"Ukweli ulipo kuhusu mchezo unaoendelezwa na Marekani kuhusiana na suala la nyuklia na kwamba taifa hilo bado lina uhasama dhidi ya Korea Kaskazini."

"Mataifa yote wanachama wa Umoja wa Mataifa yatalazimika kuwa macho kupinga jaribio la Marekani la kuhujumu hali ya amani inayoendelea kushamiri katika rasi ya Korea," ilieleza barua hiyo.

Pyongyang ilieleza kuwa ni ajabu Marekani kuona vikwazo kama njia pekee ya kutatua matatizo yote.

Hata hivyo, Marekani haijatoa tamko lolote kuhusiana na taarifa hiyo.

Mazungumzo na Korea Kaskazini kujaribu kuishawishi kuachana na mradi wa nyuklia ambao ulifikia kilele mwaka jana wakati Rais Trump na Kim walipokutana nchini Singapore.

Marais hao kwa pamoja waliahidi kuachana na mpango wa kutengeneza silaha za nyukilia, lakini bila kufafanua walimaanisha nini.

Kulikuwa na matumaini kuwa mkutanno wa Hanoi uliofanyika Februari ungewafanya viongozi hao wafikie makubaliano ya Korea Kaskazini kuachana na mradi wa nyuklia ili kuondolewa vikwazo.

Lakini mazungumzo hayo hayakuwafanya kufikia makubaliano yoyote, kwa kuwa walishindwa kukubaliana kwa amani kuhusu vikwazo vipi vingepatiwa unafuu.

Tangu kukwama kwa mazungumzo, Rais Trump na Kim hivi karibuni wamekuwa wakiwasiliana kwa barua. **BBC**

# Madereva wanawake waitiwa fursa LATRA

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) kwa kushirikiana na Benki ya Dunia (WB), imeamua kuwajengea uwezo madereva wanawake 100 kwa kuwapa mafunzo ili waweze kuendesha mabasi ya mwendokasi na mengine.

Kwa mujibu wa taarifa LATRA, mafunzo hayo yatatolewa kwa madereva wanawake kwa miezi miwili ili waweze kuwa na sifa za kuendesha magari ya abiria.

"Lengo mahususi la mradi huu ni kutoa mafunzo ya nadharia na vitendo ili kuwajengea uwezo wanawake 100 ambao hivi sasa wana uwezo wa kuendesha magari madogo," ilieleza.

Taarifa hiyo ilifafanua kuwa madereva watakaofuzu wataweza kuendesha magari ya abiria ikiwa ni pamoja na mabasi ya mradi wa mabasi yaendayo haraka.

"Mafunzo haya yatatolewa na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT). Sifa zinazotakiwa, awe raia wa Tanzania mwenye umri usiopunga miaka 25, awe na leseni ya udereva kuanzia daraja D hadi C, awe na afya njema inayomwezesha kuendesha gari," ilisema.

Pia mwombaji anatakiwa awe na cheti cha kuzaliwa au Kitambulisho cha Taifa na anayejua kusoma na kuandika.

Kuhusu utaratibu wa kufanya maombi, taarifa hiyo ilisema kuwa barua ya maombi inatakiwa iambatanishwe na nakala ya cheti cha kuzaliwa au kitambulisho cha taifa.

"Barua ya maombi iambatanishwe pia na nakala ya leseni ya udereva na nakala ya vyeti vingine vinavyoendana na mafunzo hayo iwapo anavyo na nyaraka zinazoonyesha uzoefu wa mwombaji. Mwisho wa kupokea maombi ni mwishoni mwa mwezi huu," ilisema.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko cha Benki ya Biashara ya Afrika (CBA), Solomon Kawiche (katikati), akichezesha droo ya nne ya kumpata mshindi wa promosheni ya kuadhimisha miaka mitano ya huduma ya M-pawa ya Vodacom, iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mwakilishi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania, Abdallah Hemed na Meneja Biashara wa benki hiyo, Glory Njiu. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Ummy sasa ataka dengue itokomezwe

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewataka wananchi kushirikiana na serikali katika kutokomeza dengue nchini kwa kufanya usafi katika maeneo yao na kuondoa mazalia ya mbu.

Ummy (pichani chini) alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akiendelea na ziara yake mkoani humo kwa kutembelea Manispaa ya Kinondoni na kutoa hamasa kuhusu hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kudhibiti mbu.

Juzi, waziri huyo alitembelea Manispaa ya Ilala ambako alishiriki kupulizia dawa ya kuua mazalia ya mbu waenezao homa ya dengue.

Akiwa Kinondoni, Waziri Ummy alisema waliougua dengue wamepungua na takwimu zinaonyesha kuwa Mei walikuwa watu 604 na hadi mwezi uliopita walipungua na kufikia 450.

"Matokeo ya hatua zilizochukuliwa na Manispaa ya Kinondoni yanaonyesha wagonjwa wamepungua. Ninampongeza Mkuu wa Wilaya, Daniel Chongolo, Mstahiki Meya wa Kinondoni, Mbunge Maulid Mtulia na timu nzima ya uendeshaji afya," alisema.

Waziri Ummy aliwataka waendelee na mapambano dhidi ya ugonjwa huo huku akiwataka wananchi kushirikiana na serikali katika hilo.

Takwimu za mkoa mzima wa Dar es Salaam zinaonyesha wagonjwa wamepungua kutoka watu 2,759 Mei na kufikia 790 mwezi uliopita huku Manispaa ya Ilala, Mei ilikuwa na wagonjwa 527 na mwezi uliopita walipungua na kufikia 207.



# Ukatili wa kijinsia mkoa wa Dodoma ni tishio

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SIKU moja baada ya kuripotiwa mama na mwanaye kuunguzwa na moto na mumewe, Jeshi la Polisi mkoani Dodoma, limesema vitendo vya ukatili wa kijinsia vimeongezeka mkoani hapa kutoka matukio 174 hadi 517 ndani ya miezi sita, huku yakifanywa na ndugu.

Ongezeko hilo linaonesha wilaya ya Mpwapwa ni kinara wa matukio hayo ambapo mpaka sasa yameripotiwa matukio 220 ikilinganishwa na mwaka 2018 ambapo yalikuwa 10.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Gilles Muroto, alisema kwa kipindi cha miezi sita Januari hadi Juni mwaka huu makosa ya ukatili na unyanyasaji kijinsia yameongezeka.

Alifafanua kwa mwaka 2018 yaliripotiwa matukio 174 lakini kwa miezi hiyo sita ya mwaka huu yameripotiwa matukio 517.

Alitaja Wilaya ya Dodoma kwa mwaka 2018 yalikuwa 108, Chamwino (8), Kondoa (24), Mpwapwa(10), Kongwa(7), Bahi (7) na Chemba (9).

Muroto alisema kwa kipindi cha miezi sita mwaka huu, Dodoma yameripotiwa matukio 130, Chamwino (69), Kondoa (73), Mpwapwa (220), Kongwa (4), Bahi (10) na Chemba (8).

Sababu ya ongezeko hilo

Kamanda huyo alisema ukatili na unyanyasaji wa kijinsia umeongezeka kwa sababu mbalimbali ikiwamo msongo wa mawazo ambao unasababisha watu kufanya maamuzi mabaya ya kuwadhuru watu wengine.

Muroto alitaja sababu zingine kuwa hali duni ya maisha, kuvunjika kwa ndoa, migogoro ya familia, matumizi ya madawa ya kulevya, ulevi wa kupindukia, ndoa za wake wengi, mabadiliko ya teknolojia, kukosa usiri, mmonyoko wa maadili.

Zingine ni uvivu wa kutofanya kazi kwa bidii na kutowajibika ipasavyo hasa kwa makundi ya vijana, baadhi ya viongozi wa dini kuhubiri imani potofu kwa waumini wao, ushirikina na imani potofu.

"Pia tamaa ya mali na utajiri wa ghafla, kupora mali za wajane, kupora ardhi na kusababisha migogoro ya jamii, kukosa elimu bora, uvivu wa kufikiri," alisema Muroto.

Hata hivyo, Muroto alisema sehemu kubwa ya taarifa zinazopokelewa kwenye vituo vya polisi na madawati ya jinsia, watuhumiwa walio wengi wa makosa hayo ni watu wa karibu wa familia.

"Matukio haya yanafanywa na baba, mama, shemeji, baba mkwe, mama mkwe, shangazi, mjomba, dada, kaka na wengine, na kwa uchache sana watu wa mbali na familia," alisema.

Akizungumzia tukio la mama na mtoto waliounguzwa kwa moto, Kamanda Muroto alitaja chanzo cha Mkazi wa Mlazo, Elias Warioba (30) kumwagia kumwagia mafuta ya petrol mke wake na mtoto kuwa ni mgogoro wa kimapenzi na ulevi wa kupindukia.

Muroto alisema tukio hilo lilitokea Juni 28, mwaka huu ambapo Elias anadaiwa kummwagia mafuta hayo mkewe, Mkame Wambura (28) na mtoto wake wa miezi mitatu, Fiderika Warioba, akiwa anapika, hivyo kusababisha kulipukiwa na moto.

"Majeruhi hawa walichomwa na moto baada ya kumwagiwa mafuta ya petroli. Mtuhumiwa amekamatwa na atafikishwa mahakamani," alisema Muroto.

Kamanda huyo aliongeza: "Mtuhumiwa alitoka kilabuni akiwa na lita moja ya mafuta akaingia nyumbani, lakini kabla ya hapo."

Alisema kutokana na hali hiyo, ugomvi ulizuka na kusababisha mtuhumiwa kumpiga na chupa ya mafuta kichwani huku akiwa anapika na mtoto mgongoni.



# MAN CITY WAMTWAA RODRI KWA REKODI

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imefanikiwa kuinasa saini ya kiungo wa Hispania, Rodri kutoka Atletico Madrid kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo ya pauni milioni 62.8, imesema timu hiyo ya La Liga.

Atletico imesema kwamba, mwanasheria wa mchezaji huyo pamoja wawakilishi wa City wamelipa ada ya kumruhusu mchezaji huyo kutoka La Liga juzi Jumatano.

Rodri mwenye umri wa miaka 23, alisaini mkataba na Atletico, ambao ulikuwa unamalizika Juni mwaka 2023.

Usajili huo utavunja rekodi ya usajili wa City wa pauni milioni 60 ambazo walilipa kwa ajili ya kuipata saini ya Riyad Mahrez mwaka 2018.

Rodri alijiunga na Atletico Mei mwaka 2018 baada ya miaka mitatu akiwa kule Villarreal na alicheza mechi 34 za ligi wakati walipomaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Hispania.

Alianza kuichezea timu ya Taifa ya Hispania kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Ujerumani mwaka jana na amecheza mechi sita hadi sasa.

City imefanya usajili huo wa Rodri kama usajili mkubwa zaidi kipindi hiki cha majira ya joto wakati kocha, Pep Guardiola akiwa kwenye harakati za kuimarisha kikosi chake.

# Arsenal nayo yatia mguu kwa Maguire

**LONDON,** England

HUKU Klabu ya Manchester United ikiwa imekataliwa dau lake la pauni milioni 70 kwa ajili ya kuipata saini ya beki wa Leicester City, Harry Maguire, Arsenal nayo imetia mguu.

Arsenal juzi ilitoa ofa ya pauni milioni 50 kwa ajili ya kutaka kuipata saini ya beki huyo wa timu ya Taifa ya England.

Mbali na Man United kupeleka dau hilo, Man City ilikubali kutoa pauni milioni 75, lakini kwanza inataka kutoa pauni milioni 60 na baadaye kumalizia pauni mlioni 15.

Man United na wapizani wao wa jiji moja, ManCity zinapambana katika bei ghali ya kumnasa staa huyo, lakini Arsenal imeishangaza Leicester City kwa kujaribu kumnasa staa huyo wa zamani wa Hull City kwa kiasi pungufu kuliko kile hata ambacho Man United imekataliwa.

Leicester inadaiwa kutaka kumuuza Maguire kwa dau la pauni milioni 90 ambalo litavunja rekodi ya uhamisho ya dunia kwa mabeki wa kati huku rekodi hiyo ikiendelea kushikiliwa na Virgil Van Dijk ambaye alitua Liverpool kwa dau la pauni milioni 75 Januari mwaka jana.

Mbali na Man United kupeleka dau hilo, Man City ilikubali kutoa pauni milioni 75, lakini kwanza inataka kutoa pauni milioni 60 na baadaye kutoa pauni milioni 15, ambapo bado hawajakubaliwa.







# Uefa kuzibeba zitakazofika robo fainali

**PARIS,** Ufaransa

SHIRIKISHO la Vyama vya Soka vya Ulaya (Uefa), linapanga kuzilinda timu zitakazofika robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kuzihakikishia nafasi ya kufuzu moja kwa moja kucheza mashindano hayo msimu unaofuata.

Ajax ilifika nusu fainali msimu uliopita kwenye mashindano hayo, na wameamua kuwauza wachezaji wake nyota kwa sababu hawana uhakika kama watakuwa kwenye mashindano hayo msimu ujao.

Na Afisa Mkuu wa Uefa, Aleksander Ceferin, amebainisha kwamba wameamua kupendekeza sheria hiyo mpya ambayo ipo mezani tayari kwa kujadiliwa. Ceferin ameliambia Gazeti la The Times: "Tungependa kuzilinda timu kama Ajax au kama Monaco na Leicester City.

"Ajax ilicheza nusu fainali mwaka huu na sasa watawauza wachezaji wake kwa sababu hawajui kama watafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa msimu ujao.

"Sidhani kama tutatakiwa kuzilinda timu nyingi, kwa sababu zilikaribia, lakini lazima tuangalie uwezekano wa kuzilinda klabu."

## HABARI MICHEZO

# Lampard ateuliwa rasmi kocha mpya wa Chelsea

**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea imemtangaza Frank Lampard kuwa kocha wake mpya baada ya kusaini mkataba wa miaka mitatu kuinoa klabu hiyo.

Lampard mwenye umri wa miaka 41, anaondoka katika klabu anayoinoa kwa sasa ya Derby County kuchukua hatamu katika Klabu ya Chelsea ambayo alikuwa ni mchezaji kinara kwa miaka 13.

Anarithi nafasi iliyoachwa wazi na Maurizio Sarri, ambaye ameondoka mwezi uliopita kwenda kujiunga na miamba ya Italia Klabu ya Juventus.

Lampard ameichezea Chelsea katika mechi 648, na kunyakua mataji 11 na timu hiyo.

Hata hivyo, anaenda kuingoza Chelsea katika kipindi ambacho wamepigwa marufuku ya kufanya usajili katika madirisha mawili na chombo kinachosimamia mchezo huo duniani, Fifa, lakini tayari wameshakata rufaa katika Mahakama ya Kimataifa ya Usuluhishi wa masuala ya Michezo, CAS.

"Nina furaha isiyo kifani kurejea Chelsea kama kocha mkuu," alisema Lampard.

"Kila mtu anajua mapenzi yangu kwa klabu hii na historia yangu hapa. Lakini, malengo yangu kwa sasa ni juu ya kazi hii mpya na kujipanga kwa msimu ujao."

"Nipo hapa kufanya kazi kwa bidii, na natamani kazi ianze mara moja."

Uteuzi wa Lampard unakuja siku tisa tangu klabu ya Derby ilipomruhusu kufanya mazungumzo na Chelsea na siku 18 toka Sarri alipoondoka klabuni hapo.

Lampard anakuwa kocha wa 10 kuifundisha Chelsea tangu klabu hiyo iliponunuliwa na Roman Abramovich mwaka 2003.







# BARCELONA KUMBADILISHA COUTINHO KWA NEYMAR

**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA inajua kwamba Paris Saint-Germain wanamtaka Philippe Coutinho na watamtumia kama chambo ya kumpata Neymar, kwa mujibu wa ESPN FC.

Mabingwa hao wa Hispania wanatarajia kukamilisha usajiili wa mshambuliaji wa Atletico Madrid, Antoine Griezmann wiki ijayo na ujio wake hautakuwa kikwazo cha kuipata saini ya Neymar.

Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, ameamua kuchukua jukumu la mazungumzo ya kuhakikisha Neymar anarudi Camp Nou, huku Coutinho akienda upande mwingine.

Chanzo kimoja kutoka ndani ya Barcelona kimeidokeza ESPN FC kwamba, kama watamtumia Coutinho kuwa sehemu ya usajili huo, kuna uwezekano mkubwa kwa Neymar kujiunga na Barcelona.

"PSG wanamtaka Coutinho na wanaweza kumchukua kipindi hiki cha majira ya joto," kilisema chanzo hicho kikinukuliwa na ESPN FC.

"Tunajua kwamba wameshawasiliana na watu wake wakaribu kuhusu usajili huo. Yeye ni mchezaji ambaye amewekwa kwenye rada zao kwa ajili ya usajili."

Mwezi uliopita ESPN FC iliripoti kwamba, PSG wanajiandaa kumuuza Neymar. Na watakubali kiasi cha euro milioni 200 pamoja na Coutinho.

# *Willian kuikosa Peru*

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

WINGA wa Brazil, Willian ataukosa mchezo wa fainali ya Kombe la Mataifa ya Amerika Kusini, Copa America, utakaopigwa Jumapili dhidi ya Peru baada ya kuumia misuli ya nyama za paja, timu hiyo imethibitisha jana Alhamisi.

Willian, ambaye atabakia na timu hiyo kwenye mazoezi kuelekea kweye fainali hiyo, alifunga bao la tano wakati Brazil ikiifunga Peru mabao 5-0 kwenye hatua ya makundi na alifunga penalti yake wakati wakiishinda Paraguay kwenye robo fainali.

Aliingiza kwenye mchezo wa nusu fainali dhidi ya Argentina wakati wakishinda 2-0 kuchukua nafasi ya Everton, lakini akabainisha kwamba ameumia.

Willian aliitwa dakika za mwisho kwenye kikosi hicho akichukua nafasi ya Neymar, ambaye ameikosa michuano hiyo baada ya kuumia kifundo cha mguu kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Qatar.

Willian ataukosa mchezo huo wa fainali utakaopigwa katika dimba la Maracana, huku Brazil ikitafuta taji lake la kwanza la Copa America tangu mwaka 2007.



HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# FELIX APEWA JEZI YA GRIEZMANN ATLETICO

Pia yainasa saini ya Herrera na Mbrazil Felipe, Barca sasa yasubiriwa kukamilisha dili...

**MADRID,** Hispania

ATLETICO Madrid imeinasa saini ya mshambuliaji wa kimataifa wa Ureno, Joao Felix kwa euro milioni 126 sawa na pauni milioni 113 kutoka Benfica, dau linalomfanya kuwa mchezaji wa tano ghali zaidi katika historia ya soka duniani, na atakuwa akivaa jezi namba saba iliyokuwa ikivaliwa na Antoine Griezmann.

**Benfica imethibitisha kuwa Atletico italipa kiasi hicho kwa awamu, baada ya kutoa ofa ya euro milioni sita zaidi ya dau la euro milioni 120 lililokuwa likihitajika ili kuvunja mkataba wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 19.**

Katika historia ya soka, ni Neymar, Kylian Mbappe, Philippe Coutinho na Ousmane Dembele pekee waliohama kwa dau kubwa kumshinda Felix ambaye amesaini mkataba wa miaka saba wa kuichezea Atletico.

Alianza kucheza kikosi cha kwanza kwa mara ya kwanza Agosti mwaka jana na kufunga mabao 15 wakati Benfica ikitwaa ubingwa.

Felix pia anakuwa mchezaji wa pili kinda ghali zaidi kufuatia euro milioni 180 zilizolipwa na Paris St-Germain kwa Monaco wakati ikimnunua mshambulijia Mfaransa Mbappe mwaka jana.

Kinda huyo wa zamani wa Porto alicheza mechi yake ya kwanza timu ya taifa dhidi ya Uswisi kwenye mechi ya nusu fainali ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya Juni mwaka huu.

Alifunga hat-trick dhidi ya Eintracht Frankfurt kwenye Europa League Aprili mwaka jana, na kuwa kinda mdogo zaidi Benfica na Ureno kuweza kufunga mabao matatu katika michuano hiyo Ulaya na kinda mdogo zaidi kuweza kufanya hivyo kwenye Europa League.

Straika wa Atletico, Antoine Griezmann amethibitisha kwamba ataachana na klabu hiyo majira haya ya joto, na Barcelona inatarajiwa kulipa dau la euro milioni 120 zinazohitajika ili kuvunja mkataba wake.

Jumatano pia Atletico ilithibitisha kuwasainisha wachezaji wawili kutoka Porto; kiungo Mmexico Hector Herrera, 29, ametia saini ya mkataba wa miaka mitatu baada ya kuhama kwa uhamisho huru, wakati beki wa kati, Mbrazil Felipe, 30, amejiunga kwa kiasi cha euro milioni 20 sawa na pauni milioni 17.9.

Klabu hiyo pia imethibitisha kumuuza kiungo Mhispania Rodri, 23, kwa mabingwa wa Ligi Kuu England, Manchester City kwa dau la pauni milioni 62.8.

## ZISIKUPITE

### BARCA YAIITIA ARSENAL MALCOM

ARSENAL imepewa ofa na Barcelona ya kumnunua mshambuliaji Mbrazil Malcom, lakini bado inaelekeza macho yake kwanza kwa kujaribu kuipata saini ya straika Muivory Coast Wilfred Zaha, kutoka Crystal Palace. ***(Mirror)***

### CHELSEA TATIZO FACEBOOK

FRANK Lampard alichelewa kutangazwa kuwa kocha wa Chelsea juzi Jumatano kwa sababu ya matatizo yaliyojitokeza kwenye mitandao ya Facebook na Instagram ya kuingiza na kufungua picha za video kwa kuwa klabu hiyo ilitaka mitandao hiyo ya kijamii kufanya kazi hiyo kabla ya kumtangaza. ***(Mirror)***

### POCHETTINO AMTAKA DIAZ

KOCHA wa Tottenham, Mauricio Pochettino ameitaka klabu hiyo kuhakikisha inaipata saini ya straika Mhispania Mariano Diaz, 25, kutoka Real Madrid. ***(Ok Diario via Star)***

### FERNANDES, UNITED WAKETI

MANCHESTER United inaitaka saini ya kiungo Mreno Bruno Fernandes, 24, kutoka Lisbon, na wakala wa mchezaji huyo tayari yupo England kwa ajili ya kukamilisha dili hilo. ***(Sky Sports)***

### AWANIWA ARSENAL, LIVER

ARSENAL, Liverpool na Tottenham wapo vitani kuisaka saini ya kiungo wa Real Madrid na Hispania, Dani Ceballos, 22. ***(Marca)***

### LEICESTER KWA TIELEMANS, PEREZ

LEICESTER inakaribia kuipata saini ya kiungo Mbelgiji Youri Tielemans, 22, kutoka Monaco na pia inatazama uwezekano wa kuipata huduma ya mshambuliaji Mhispania Ayoze Perez, 25, kutoka Newcastle kwa dau takriban pauni milioni 30. ***(Telegraph)***

### YAMVUTIA PUMZI LO CELSO

TOTTENHAM imesitisha kwanza mazungumza na Real Betis kuhusu saini ya kiungo Muagentina Giovani Lo Celso, 24, kutokana na klabu hizo mbili kutofikia makubaliano ya ada ya uhamisho. ***(Sky Sports)***

### YAMGEUKIA MOUNT WA DERBY

CHELSEA imefungua mazungumzo ya mkataba na Mason Mount, aliyecheza chini ya Frank Lampard katika kikosi cha Derby msimu uliopita. ***(Evening Standard)***

### KUONGEZA DAU KWA ZAHA

ARSENAL imepandisha dau na kusema pauni milioni 70 zipo ikijiandaa kutoa ofa ya pili kwa Muivory Coast Wilfred Zaha, ingawa Crystal Palace inaaminika inahitaji pauni milioni 80 kwa mshambuliaji huyo. ***(Sky Sports)***

### BAYERN YAIPIKU MAN CITY

BAYERN Munich imeipiku Manchester City katika mbio za kuinasa saini ya beki wa kulia Mreno Joao Cancelo, 25, kutoka Juventus. ***(Corriere dello Sport via Manchester Evening News)***

### INTER YAMKOMAA KWA LUKAKU

WAKALA wa Romelu Lukaku, amefanya mazungumzo mapya na Inter Milan wakati huu miamba hiyo ya Italia bado wakiwa katika mazungumzo na Manchester United kuhusu ada ya kuipata saini ya straika huyo Mbelgiji. ***(Sky Sport Italia - in Italian)***

# COULIBALY ATUA KUJIFUNGA SIMBA

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Simba ikiwa imebakiza nafasi mbili tu kabla ya kukamilisha usajili wa wachezaji 10 wa kigeni, beki ambaye mashabiki wengi hawamkubali, Muivory Coast Zana Coulibaly ametua nchini kwa mazungumzo ya mkataba mpya na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, imeelezwa.

Kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu Bara, kila klabu inaruhusiwa kusajili wachezaji wasiozidi 10 wa kigeni na tayari Simba imefikisha wachezaji nane hadi sasa.

Kuelekea msimu mpya wa 2019/20, tayari Simba imeshanasa saini za wachezaji wapya watano wa kigeni, ambao ni mabeki Wabrazil Gerson Fraga Vieira kutoka ATK ya Ligi Kuu ya India na Tairone Santos da Silva kutoka Klabu ya Atletico Cearense FC, mshambuliaji Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino, zote za Daraja la Nne nchini Brazil na viungo Msudan Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman aliyetokea Al Hilal ya Sudan pamoja na winga Deo Kanda kutoka TP Mazembe ya kwao, DR Congo.

Nyota hao wapya wanaungana na wachezaji watatu wa msimu uliopita ambao wameongezewa mikataba mipya, kiungo Mzambia Clatous Chama, straika Mnyarwanda Meddie Kagere na beki Muivory Coast Pascal Wawa, hivyo kufikisha jumla ya wachezaji wa kigeni nane.

Simba bado inahaha kuinasa saini ya mshambuliaji Mganda Emmanuel Okwi anayeitumikia timu yake ya taifa katika michuano ya Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, lakini inaonekana kama uhakika wa kumpata umefifia baada ya kumnasa kiungo Mkenya Francis Kahata.

Hivyo ni wazi sasa endapo itamwongeza mkataba Coulibaly itakuwa imekamilisha usajili wa wachezaji 10 wa kigeni na kupeperusha matarajio ya wanachama na mashabiki wa timu hiyo ya kumuona Okwi akiendelea kuitumikia Simba

Coulibaly ambaye alisaini mkataba wa miezi sita kwa lengo la kuwa mbadala wa Shomari Kapombe aliyeumia, imeelezwa kuwa uwezo wake umemkuna Kocha Mkuu, Patrick Aussems na amependekeza asiachwe msimu ujao.

"Ni kweli Coulibaly kwa sasa yupo hapa jijini tayari kwa mazungumzo na yamefikia mahali pazuri, hivyo muda wowote kuanzia sasa atatangazwa kuwa mali ya Simba kwa mkataba wa miaka miwili," chanzo chetu cha uhakika ndani ya Simba kilieleza.

Katika ukurasa wake wa Instagram, Coulibaly pia aliandika amerejea Tanzania.



Beki wa pembeni wa Simba, Muivory Coast Zana Coulibaly (kushoto), akifanya vitu vyake kwenye mechi ya SportPesa Cup dhidi ya Mbao FC, mwanzoni mwa mwaka huu. Beki huyo yupo kwenye mazungumzo ya mkataba mpya na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara. **PICHA: MAKTABA**

## Wanawake Zanzibar wajitosa riadha

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TOFAUTI na ilivyotarajiwa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma, safari hii wanawake wengi wa Zanzibar wamehamasika na kushiriki katika mashindano ya riadha ya nusu marathon.

Katika mashindano hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki visiwani hapa, wanawake wengi wa rika tofauti walijitokeza na kushiriki mbio hizo za kilomita 21, 10 na tano zilizoanzia Ngome Kongwe na kuishia Chukwani kwa kilomita 21, Mazizini katika makutano ya barabara inayoelekea ZRB kwa kilomita 10 na kilomita tano zikiishia Kilimani Chini.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Chama cha Riadha Zanzibar (ZAAA), Muhidini Yasin, alisema wamefarijika kuona idadi kubwa ya wanawake kujitokeza na kushiriki na kwamba hatua hiyo inaonyesha dhahiri kwamba lengo lao la kuwahamasisha wanawake hasa wazawa kushiriki riadha kupitia mashindano hayo limefanikiwa.

"Tunashukuru ushiriki mkubwa wa wanawake kwa kilomita zote zilizoshirikisha mbio hizo, na huu ndio mwanzo mzuri wa malengo yetu," alisema.

Katika mashindano hayo Pendo Pamba kutoka klabu ya mafunzo alishika nafasi ya kwanza kwenye kilomita 10, Rose Mary kutoka KMKM akashika nafasi ya pili na Catherina Bell kutoka Nungwi akaibuka mshindi wa tatu.

Kwa upande wa kilomita 21, Rosalia Fabian wa Klabu ya JKU aliibuka kidedea kwa kutumia muda wa saa 1:24.00.

## Bokungu arejea, ashukia KMC

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa zamani wa Klabu ya Simba Mkongomani Javier Besala Bokungu, amerejea tena nchini Tanzania na kujiunga na Klabu ya KMC inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo ni kwamba Bokungu amesaini mkataba wa mwaka mmoja, na amekuja pamoja na mchezaji mwingine kutoka Congo, Melly Sivirwa ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili akitokea Klabu ya Vital'O ya Burundi.

Bokungu anayemudu kucheza nafasi ya beki wa kulia na pia beki wa kati, amejiunga na KMC akitokea Klabu ya Groupe Bazano ya nchini Congo.

Hii ni mara ya pili sasa kwa mchezaji huyo kurejea nchini kwani aliichezea Simba mwaka 2016 na 2017, lakini aliondoka baada ya mkataba wake kumalizika.

Atakumbukwa kwa kuipa Simba ushindi dhidi ya mahasimu wao wa jadi kwenye Kombe la Mapinduzi hatua ya nusu fainali mwaka 2017 alifunga penalti ya nwisho, Simba ikiichapa Yanga kwa penalti 4-2.

Hata hivyo, Simba ikafungwa kwenye fainali dhidi ya Azam FC.

Kusajiliwa kwa wachezaji hao ni mwendelezo wa Klabu ya KMC kuboresha kikosi chake hasa kwa wachezaji wazoefu na wa kimataifa, hususan itakapokwenda kukabiliana na timu mbalimbali kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kabla ya kuichezea Simba, Bokungu aliwahi kuzichezea Klabu za TP Mazembe na Esperance kwa nyakati tofauti.

Michezo
Ijumaa Julai 5, 2019
Nipashe



Felix apewa jezi ya Griezmann Atletico UKURASA 30

MTIFUANO...



Kiungo wa Chile, Arturo Vidal (kushoto), akiwania kuucheza mpira dhidi ya mshambuliaji wa Peru, Jose Paolo Guerrero, wakati wa mechi ya nusu fainali ya Copa America, iliyopigwa Brazil juzi. Peru ilishinda mabao 3-0 hivyo sasa itakutana fainali dhidi ya Brazil Jumapili. **PICHA: MTANDAO**

## Amunike atoa msimamo Stars

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), Emmanuel Amunike, amesema matokeo waliyoyapata Cairo Misri kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019, wamejifunza mengi licha ya kupata vipigo katika mechi zote tatu za hatua ya makundi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mchana mara baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, alisema hajawafurahisha mashabiki na Watanzania kwa ujumla kutokana na matokeo hayo, lakini sasa anaelekeza nguvu zake katika mashindano ya kuwania kufuzu fainali za Wachezaji wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN) ambazo fainali zake zitafanyika mwakani nchini Cameroon.

"Naamini wachezaji wamejifunza mambo mengi Afcon kwa sababu wamekutana na timu zenye viwango vya juu, hivyo tutaanza maandalizi kwa ajili ya CHAN," alisema Amunike kwa kifupi huku akieleza kikosi kitakachoivaa Sudan kuelekea kuwania kufuzu CHAN atakiweka bayana baadaye.

Kwa upande wake Waziri mwenye dhamana ya michezo Harrison Mwakyembe, alisema kuwa wachezaji wamejitahidi kwa hatua waliyofikia na kudai baada ya miaka miwili Tanzania ina uhakika wa kushiriki kwa mara nyingine michuano kama hiyo.

Aidha, aliwataka Watanzania na wadau wa soka hapa nchini kuacha kuwazodoa wachezaji kwa matokeo waliyoyapata na badala yake waendelee kuisapoti timu hiyo ili iweze kufanya vizuri kwenye mashindano yaliyopo mbele yao.

# Kahata rasmi Simba, Okwi basi

**Na Mwandishi Wetu**

### ●●● Sasa bado nafasi moja tu ya nyota wa kimataifa, Zana Coulibaly akaribia kuiziba huku ikielezwa...

WAKATI mashabiki na wanachama wa Simba wakiwa bado na kiu ya kumuona mshambuliaji wao, Mganda Emmanuel Okwi akiitumikia klabu hiyo, uwezekano wa kusaini mkataba mpya unaelekea kuyeyuka baada ya kumnasa kiungo wa kimataifa wa Kenya Francis Kahata.

**Kahata aliyetua jana Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam, tayari ametangazwa kujiunga na mabing wa watetezi hao wa Ligi Kuu Bara na hata kabla ya kutangazwa alishaandika kwenye wiki pedia kwamba yeye ni mchezaji wa Simba kuanzia mwaka 2019.**

"Ni mchezaji mwenye uwezo mkubwa wa kucheza eneo la kiungo, kwa sasa akiwa sehemu ya wachezaji wanaounda kikosi cha timu ya Taifa ya Kenya kilichoshiriki Afcon, Francis Kahata (27), msimu ujao atavaa jezi ya mabingwa wa nchi baada ya kusaini mkataba wa miaka miwili.

"@kachikahata amejiunga Msimbazi akitokea Gor Mahia ya Kenya ambapo akiwa kwenye klabu hiyo alishinda Kombe la Ligi Kuu mara tatu, Kiungo Bora wa mwaka wa Ligi Kuu ya Kenya mara mbili na Mchezaji Bora wa msimu 2018/2019 wa Gor Mahia. #Nguvu Moja," ilieleza taarifa ya Simba kupitia ukurasa wao wa Instagram jana.

Kutua kwa Kahata aliyezaliwa Mei 4, 1992, ina maana Simba sasa imefikisha jumla ya wachezaji tisa wa kigeni, sita wapya na watatu walioongezewa mikataba yao hadi sasa kwa maana hiyo kunaifanya kubakiwa na nafasi moja tu ya nyota wa kigeni kwa mujibu wa Kanuni za Ligi Kuu Bara ambazo zinataka kila klabu kutozidisha nyota 10 wa kigeni.

Kuelekea msimu mpya wa 2019/20, tayari Simba imeshanasa saini za wachezaji wapya sita wa kigeni, ambao ni mabeki Wabrazil Gerson Fraga Vieira kutoka ATK ya Ligi Kuu ya India na Tairone Santos da Silva kutoka Klabu ya Atletico Cearense FC, mshambuliaji Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino, zote za Daraja la Nne nchini Brazil na viungo Msudan Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman aliyetokea Al Hilal ya Sudan pamoja na winga Deo Kanda kutoka TP Mazembe ya kwao, DR Congo na sasa Kahata kutoka Gor Mahia.

Nyota hao wapya sita wanaungana na wachezaji watatu wa msimu uliopita ambao wameongezewa mikataba mipya, kiungo Mzambia Clatous Chama, straika Mnyarwanda Meddie Kagere na beki Muivory Coast Pascal Wawa, hivyo kufikisha jumla ya wachezaji wa kigeni tisa.

Lakini kwa sasa beki wa pembeni, Zana Coulibaly, yupo nchini akifanya mazungumzo ya kuongeza mkataba na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara, hivyo kama dili hilo likikamilika ina maana Okwi ndio basi tena ndani ya kikosi hicho cha mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam.

Kahata alianza kuichezea Harambee Stars kwa mara ya kwanza mwaka 2011 na hadi sasa ameshaitumikia jumla ya mechi za kimataifa 31.

Alianzia soka lake Thika United ambapo aliichezea akiwa kinda kabla ya kuanza kucheza timu ya wakubwa mwaka 2008-2015 na kisha mwaka 2010 kutolewa kwa mkopo University of Pretoria, huku mwaka 2014 akiitumikia KF Tirana kwa mkopo kabla ya mwaka unaofuata kusaini jumla, na kuanzia mwaka 2015-2019alikuwa akikipiga Gor Mahia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >